TANGAZO LA SERIKALI NA. 371 la tarehe 26/04/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

SURA 287

# KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KITONGOJI KATIKA MAMLAKA ZA MIJI MIDOGO ZA MWAKA 2019

TANGAZO LA SERIKALI NA. 371 la tarehe 26/04/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

SURA 287

Zimetungwa chini ya Kifungu 201A

KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KITONGOJI KATIKA MAMLAKA ZA MIJI MIDOGO ZA MWAKA 2019

MPANGILIO WA KANUNI


| Kanuni | Jina | Uk |
|---|---|---|
| 1 | Jina | 3 |
| 2 | Eneo la matumizi na tarehe ya kuanza kutumika | 3 |
| 3 | Tafsiri | 3 |
| 4 | Tangazo la uchaguzi kwa umma | 4 |
| 5 | Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji | 5 |
| 6 | Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi | 5 |
| 7 | Kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo | 5 |
| 8 | Maelekezo kuhusu Uchaguzi | 6 |
| 9 | Orodha ya Wapiga Kura | 6 |
| 10 | Uandikishaji wa wapiga kura | 6 |
| 11 | Pingamizi kuhusu uandikishaji | 7 |
| 12 | Sifa za mpiga kura | 8 |
| 13 | Kupoteza sifa ya kupiga kura | 8 |
| 14 | Sifa za Mgombea | 8 |
| 15 | Kupoteza sifa ya kuwa Mgombea | 9 |
| 16 | Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi | 10 |
| 17 | Utaratibu wa uteuzi wa Wagombea | 10 |
| 18 | Kupita bila kupingwa | 11 |
| 19 | Kujitoa kwa Mgombea | 11 |
| 20 | Kufariki kwa Mgombea | 11 |
| 21 | Ukomo wa kuwa madarakani | 11 |
| 22 | Pingamizi kuhusu uteuzi | 11 |

| | | |
|---|---|---|
| 23 | Kamati ya Rufaa | 12 |
| 24 | Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Rufaa | 12 |
| 25 | Majukumu ya Kamati ya Rufaa | 12 |
| 26 | Kampeni za Uchaguzi | 13 |
| 27 | Wajibu wa Jeshi la Polisi | 13 |
| 28 | Mabadiliko ya ratiba | 14 |
| 29 | Masharti ya Kampeni | 14 |
| 30 | Mahali, vituo na muda wa kupigia kura | 14 |
| 31 | Masanduku ya kura | 15 |
| 32 | Karatasi za kupigia kura | 15 |
| 33 | Utambulisho wa mpiga kura | 15 |
| 34 | Upigaji kura | 16 |
| 35 | Usaidizi kwa wenye mahitaji maalum | 16 |
| 36 | Kuahirisha upigaji Kura | 17 |
| 37 | Kuhesabu kura | 17 |
| 38 | Matokeo ya Mwenyekiti wa Kitongoji | 18 |
| 39 | Taratibu za kurudia Uchaguzi | 18 |
| 40 | Masuala yasiyobatilisha matokeo | 18 |
| 41 | Malalamiko kuhusu uendeshaji wa Uchaguzi | 18 |
| 42 | Nafasi wazi | 19 |
| 43 | Uchaguzi Mdogo | 19 |
| 44 | Kiapo | 20 |
| 45 | Makosa ya Uchaguzi | 20 |
| 46 | Kinga | 21 |
| 47 | Waangalizi wa Ndani wa Uchaguzi | 22 |
| 48 | Taratibu za Maadili | 22 |
| 49 | Miongozo | 22 |
| 50 | Elimu ya Mpiga Kura | 22 |
| 51 | Kufutwa kwa Kanuni za Uchaguzi Tangazo la Serikali Na. 320 la Mwaka 2014 | 22 |

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo za Mwaka 2019.

Eneo la matumizi na Tarehe ya kuanza kutumika

2. Kanuni hizi zitatumika katika Vitongoji vyote vilivyomo katika maeneo ya Mamlaka za Miji Midogo na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi isipokuwa pale itakavyoelezwa vinginevyo:-

Sura 258

"Chama cha Siasa" maana yake ni Chama cha Siasa kilichopata usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa;

Sura 287

"Kitongoji" maana yake ni sehemu ya eneo la utawala katika eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya);

"Mamlaka ya Uchaguzi maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa;"

"mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye anaishi kwenye eneo la Kitongoji na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Kitongoji;

"Msimamizi wa Uchaguzi" maana yake ni Mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa na Mamlaka ya Uchaguzi kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi" maana yake ni mtumishi yeyote wa umma aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi;

"Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa shughuli za Serikali katika Mamlaka ya Mji Mdogo na ni pamoja na mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mtendaji wa

Mamlaka ya Mji Mdogo kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"mtumishi wa umma" maana yake ni mtu yeyote aliyeajiriwa katika utumishi wa umma;

"Orodha ya Wapiga Kura" maana yake ni orodha ya majina ya wapiga kura iliyoandaliwa chini ya Kanuni hizi;

Sura 357

"raia" maana yake ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia;

"sehemu ya matangazo ya uchaguzi" maana yake ni sehemu maalum iliyoteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa ajili ya kutolea matangazo au taarifa mbalimbali za Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi

"siku ya uteuzi" maana yake ni siku ya kutangaza majina ya wanaostahili na wasiostahili kugombea nafasi za uongozi chini ya Kanuni hizi;

"Uchaguzi" maana yake ni Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo;

"Uchaguzi Mdogo" maana yake ni uchaguzi ambao utafanyika baada ya kuwepo kwa nafasi wazi ya Mwenyekiti wa Kitongoji;

"wakati wa uchaguzi" maana yake ni muda ambao uchaguzi wa kawaida au Uchaguzi Mdogo unafanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi na unaanzia tarehe ya tangazo la uchaguzi hadi matokeo ya uchaguzi yanapotangazwa;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA PILI
## TANGAZO LA UCHAGUZI

Tangazo la uchaguzi kwa umma

4. (1) Kutakuwa na uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji ambao utafanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi baada ya Waziri kutoa Tangazo la Uchaguzi kwa umma.

(2) Tangazo la Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni Ndogo

ya (1) litatolewa katika magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa nchi nzima na katika vyombo mbalimbali vya habari si chini ya siku tisini kabla ya siku ya uchaguzi.

(3) Tangazo litakalotolewa na Waziri litaelekeza mambo yafuatayo:

(a) ratiba ya uchaguzi na shughuli zinazohusika; na

(b) masharti muhimu ya uchaguzi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi.

Majina na mipaka ya Vitongoji

5. Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza katika sehemu ya matangazo ya uchaguzi majina na mipaka ya Vitongoji vilivyomo katika eneo la Halmashauri husika siku sabini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji.

Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi

6. (1) Kutakuwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo au mtumishi wa umma atakayeteuliwa kusimamia uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Mtu hatateuliwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi endapo ni:

(a) kiongozi wa chama cha siasa;

(b) Mgombea;

(c) Hakimu au Jaji;

(d) kiongozi wa dini;

(e) askari wa jeshi lolote;

(f) Katibu Tawala wa Wilaya;

(g) Katibu Tawala wa Mkoa;

(h) Mkuu wa Wilaya; au

(i) Mkuu wa Mkoa.

Kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo

7. Kila Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Wajumbe wa Kamati ya Rufaa au mtumishi wa umma atakayeteuliwa kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi atasimamia Uchaguzi kwa kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo yatakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TATU
## MAELEKEZO YA UCHAGUZI

Maelekezo kuhusu uchaguzi

**8.** (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya Uchaguzi siku sitini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.

(2) Maelekezo ya Uchaguzi, kwa mujibu wa Kanuni hizi, yataelekeza mambo yafuatayo:

(a) tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi;
(b) muda na sehemu ya kuandikisha wapiga kura;
(c) muda na mahali pa kufanyia Uchaguzi;
(d) kuwataka wakazi wote wenye sifa za kupiga kura washiriki uchaguzi;
(e) kuwataka wakazi wenye umri wa miaka ishirini na moja au zaidi wanaotaka kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji kuchukua fomu za kugombea zitakazopatikana kwenye ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(f) tarehe na muda wa kuchukua na kurudisha fomu za maombi ya kugombea uenyekiti Kitongoji kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(g) siku ambayo uteuzi utafanyika na sehemu ya matangazo ya uchaguzi ambapo fomu za wagombea zitabandikwa;
(h) muda wa kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi na kusikilizwa kwa pingamizi;
(i) tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(j) kipindi cha kuendesha mikutano ya kampeni za Uchaguzi; na
(k) masuala mengine yanayohusu uchaguzi.

Orodha ya Wapiga Kura

**9.** (1) Kutakuwa na Orodha ya Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni Ndogo ya (1), Msimamizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa watumishi wa umma watakaoandikisha na kuandaa Orodha ya Wapiga Kura katika Vitongoji siku hamsini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.

(3) Watendaji wa Vijiji, Mitaa na Kata hawatateuliwa wala hawataruhusiwa kuandikisha au kuandaa orodha ya wapiga kura.

Uandikishaji wa Wapiga Kura

**10.** (1) Uandikishaji na uandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura utaanza siku ya arobaini na saba kabla ya siku ya Uchaguzi na utafanyika kwa muda wa siku saba kwa

kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi katika majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na Viongozi wa Vyama vya Siasa;

(2) Vituo vya uandikishaji wa wapiga kura vitafunguliwa saa mbili kamili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili kamili jioni.

(3) Chama cha Siasa kitaruhusiwa kuteua wakala wake kwa kila kituo cha uandikishaji wa wapiga kura wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.

(4) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika sehemu ya matangazo ya uchaguzi nakala ya Orodha ya Wapiga Kura siku moja baada ya kukamilika kwa uandikishaji wa wapiga kura na atatunza nakala halisi ya Orodha hiyo.

(5) Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya Wapiga Kura atakuwa na haki ya kukagua Orodha ya Wapiga Kura katika muda wa siku saba tangu tarehe ya Orodha hiyo kubandikwa sehemu ya matangazo ya uchaguzi ili:

(a) kuweka pingamizi kuhusu usahihi wa Orodha hiyo;

(b) kuomba Orodha irekebishwe kwa:-

(i) kuongeza jina lake;

(ii) kubadilisha taarifa zilizoko katika Orodha hiyo; au

(iii) kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa amefariki.

Pingamizi kuhusu uandikishaji

**11.** (1) Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya Wapiga Kura anaweza kuweka pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura kabla ya kumalizika kwa muda wa kukagua Orodha ya Wapiga Kura.

(2) Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atatakiwa kutoa uamuzi kuhusu pingamizi lililowekwa ndani ya siku mbili tangu tarehe ya mwisho ya ukaguzi wa Orodha ya Wapiga Kura.

(3) Endapo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataridhika na pingamizi lililowekwa chini ya Kanuni hii, atarekebisha Orodha ya Wapiga Kura iliyotangazwa katika muda wa siku mbili isipokuwa kama uamuzi

wake umekatiwa rufaa.

(4) Endapo mtu aliyeweka pingamizi au aliyewekewa pingamizi hatoridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi lililowasilishwa kwake, mtu huyo atawasilisha rufaa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ndani ya muda wa siku mbili tangu kutolewa kwa uamuzi wa pingamizi.

(5) Msimamizi wa Uchaguzi, baada ya kupokea rufaa hiyo, ataishughulikia na kuitolea uamuzi ndani ya muda wa siku nne tangu siku ya kupokea rufaa hiyo.

(6) Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni Ndogo ya (4) utakuwa wa mwisho.

Sifa za mpiga kura

**12.** Mkazi yeyote wa Kitongoji atakuwa na haki ya kupiga kura endapo atakuwa na sifa zifuatazo:

(a) ni raia wa Tanzania;
(b) ana umri wa miaka kumi na nane au zaidi;
(c) ni mkazi wa eneo la Kitongoji;
(d) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu; na
(e) awe amejiandikisha kupiga kura katika Kitongoji husika.

Kupoteza sifa ya kupiga kura

**13.** Mtu hatakuwa na haki ya kupiga kura endapo:

(a) hana mojawapo ya sifa zilizoainishwa katika Kanuni ya 12; au
(b) amejiandikisha kupiga kura katika kituo zaidi ya kimoja.

Sifa za Mgombea

**14.** Mkazi yeyote wa Kitongoji anaweza kugombea uenyekiti wa Kitongoji endapo:-

(a) ni raia wa Tanzania;
(b) ana umri wa miaka ishirini na moja au zaidi;
(c) ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
(d) ana shughuli halali ya kumwezesha kuishi;
(e) ni mkazi wa eneo la Kitongoji;
(f) ni mwanachama wa Chama cha Siasa na amedhaminiwa na Chama hicho;
(g) hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya Uchaguzi; na
(h) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na

Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

Kupoteza sifa ya kuwa mgombea

15. (1) Mtu hatakuwa na sifa za kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji endapo:

(a) amepoteza au hana sifa za mgombea zilizoainishwa katika Kanuni ya 14;

(b) amehukumiwa hukumu ya kifo na Mahakama za Tanzania au anatumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita jela;

(c) ana mkataba au maslahi kwenye kampuni ambayo ina mkataba na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo anagombea nafasi ya uongozi na hajatangaza kuwepo kwa mkataba au maslahi yake kupitia kwenye gazeti linalopatikana katika eneo husika au mbao za matangazo katika ofisi ya Kitongoji;

(d) amepoteza sifa ya kupiga kura chini ya Kanuni hizi au kwa mujibu wa Sheria yeyote inayohusu makosa ya uchaguzi;

(e) hatojaza fomu ya tamko la kuheshimu taratibu za maadili; au

(f) ataajiriwa au kuteuliwa katika wadhifa wowote katika Utumishi wa Umma au kuchaguliwa katika nafasi ya udiwani, ubunge, uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umakamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni ya 15(1)(b):

(a) adhabu mbili au zaidi za kifungo zinatotakiwa kutumikiwa kwa kufuatana zitachukuliwa kuwa ni adhabu tofauti iwapo kati ya adhabu hizo hakuna inayozidi miezi sita jela lakini endapo kati ya adhabu hizo kuna inayozidi miezi sita jela itachukuliwa kuwa ni adhabu moja; au

(b) kifungo cha jela kilichosababishwa na kushindwa kulipa faini hakitohesabiwa kuwa ni adhabu ya kifungo.

SEHEMU YA NNE
UTEUZI WA WAGOMBEA

Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi

16. (1) Mtu yeyote anayekusudia kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji atatakiwa kuchukua fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi husika siku zisizopungua ishirini na sita kabla ya siku ya uchaguzi kwa kadri itakavyoelekezwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(2) Mtu aliyechukua fomu kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) atatakiwa kurejesha fomu husika ndani ya muda wa siku saba tangu siku ya kwanza ya uchukuaji wa fomu iliyotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(3) Fomu za uteuzi wa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji zitatolewa na kupokelewa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

(4) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hatoruhusiwa kupokea kutoka kwa mtu yeyote fomu za uteuzi zitakazowasilishwa baada ya saa kumi kamili jioni ya siku ya mwisho ya kurejesha fomu.

(5) Fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji zitakuwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

Utaratibu wa uteuzi wa Wagombea

17. (1) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji siku kumi na tisa kabla ya tarehe ya Uchaguzi kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni

(2) Baada ya uteuzi kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika majina ya wagombea wenye sifa na wasio na sifa za kugombea nafasi ya uenyekiti wa kitongoji sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

(3) Endapo baada ya saa kumi kamili jioni ya siku ya uteuzi kutakuwa hakuna mwombaji aliyejitokeza au kama waombaji wote waliojitokeza hawana sifa zinazostahili, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atavitaarifu Vyama vya Siasa na wakazi wa Kitongoji kuhusu kukosekana kwa waombaji au kutokuwepo kwa waombaji wenye sifa.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni Ndogo ya (3), Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atavitaarifu Vyama vya Siasa na wakazi wa Kitongoji husika kuhusu kurudiwa kwa mchakato wa uchaguzi baada ya siku arobaini kuanzia tarehe ya uteuzi.

Kupita bila kupingwa

18. Endapo siku ya uteuzi kutakuwa na mwombaji mmoja aliyejitokeza katika nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji na mwombaji huyo akateuliwa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mwombaji huyo kuwa ni mshindi wa nafasi aliyoomba kugombea kwa kupita bila kupingwa.

Kujitoa kwa mgombea

19. (1) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea aliyeteuliwa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji atajitoa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi wa mgombea huyo na wagombea waliobaki watapigiwa kura ili kupata mshindi.

(2) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea aliyeteuliwa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji atajitoa na kubaki mgombea mmoja wa nafasi hiyo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyebaki kuwa mshindi wa nafasi iliyoombwa kwa kupita bila kupingwa.

Kufariki kwa mgombea

20. Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji atafariki, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha Uchaguzi wa nafasi hiyo na Chama cha Siasa kilichotoa mgombea aliyefariki kinaweza kuwasilisha jina la mwombaji mwingine ndani ya siku arobaini tangu kuahirishwa kwa Uchaguzi ili hatua za uteuzi wa mgombea huyo zifanyike.

Ukomo wa kuwa madarakani

21. Mwenyekiti wa Kitongoji atakoma kushika nafasi hiyo siku saba kabla ya siku ya kuchukua fomu za kugombea uongozi chini ya Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TANO
## UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA PINGAMIZI NA RUFAA

Pingamizi kuhusu uteuzi

22. (1) Mtu yeyote aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au anapinga uteuzi wa mgombea yeyote, anaweza kuwasilisha pingamizi na kumwomba Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kupitia upya uamuzi

uliofanyika ili amteue kuwa mgombea au atengue uteuzi anaoupinga na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kupitia pingamizi husika, anaweza kukubali au kulikataa pingamizi hilo.

(2) Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) litawasilishwa kwa maandishi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika muda wa siku mbili tangu uamuzi au uteuzi ulipofanyika na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili kuanzia siku ya kupokea pingamizi hilo.

(3) Mwombaji au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa iliyoanzishwa chini ya Kanuni ya 23 katika muda usiozidi siku nne kuanzia tarehe ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Kamati ya Rufaa

**23.** (1) Kutakuwa na Kamati ya Rufaa katika kila Wilaya ambayo itasikiliza mapingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea wa Uchaguzi katika Wilaya husika.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Rufaa watateuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa, siku saba kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea, kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Kanuni ya 24.

(3) Kamati ya Rufaa itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Katibu Tawala wa Wilaya ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) watumishi wanne wa umma kutoka taasisi za umma zilizopo katika Wilaya husika; na

(c) mtumishi mmoja wa umma ambaye atakuwa Katibu na hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Rufaa

**24.** Mtu yeyote hatateuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Rufaa endapo:

(a) anahusika na uteuzi wa wagombea

(b) ni Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo;

(c) ni mtumishi wa Halmashauri; au

(d) Kiongozi wa Chama cha Siasa katika ngazi yoyote.

Majukumu ya Kamati ya Rufaa

**25.** (1) Kamati ya Rufaa itakuwa na majukumu ya kupokea, kusikiliza na kutoa uamuzi wa rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni ya 22(3).

(2) Kamati ya Rufaa itatoa uamuzi wa rufaa ndani ya muda wa siku nne kuanzia siku ya kupokea rufaa na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(3) Mtu aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamati ya Rufaa atakuwa na haki ya kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya muda wa siku thelathini baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa.

## SEHEMU YA SITA
## KAMPENI ZA UCHAGUZI

Kampeni za Uchaguzi

**26.** (1) Kampeni za Uchaguzi zitafanyika siku saba kabla ya siku ya Uchaguzi.

(2) Kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi kitawasilisha ratiba yake ya mikutano ya kampeni ya Uchaguzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si chini ya siku saba kabla ya kuanza kwa kampeni.

(3) Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha ratiba za mikutano ya kampeni zilizowasilishwa na Vyama vya Siasa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (2) baada ya maridhiano na Vyama vya Siasa vinavyoshiriki Uchaguzi na atatakiwa kuwasilisha ratiba ya mikutano ya kampeni za Uchaguzi iliyounganishwa siku tatu kabla ya kampeni kuanza kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

(4) Endapo Vyama vya Siasa vitashindwa kuridhiana wakati wa uunganishaji wa ratiba za mikutano ya kampeni, Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha ratiba za mikutano ya kampeni na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(5) Mgombea au mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kinaweza kuitisha na kuhutubia mikutano ya kampeni kwa mujibu wa ratiba ya mikutano ya kampeni iliyoandaliwa na kuwasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya na mikutano hiyo itaratibiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Wajibu wa Jeshi la Polisi

**27.** (1) Mkuu wa Polisi wa Wilaya atakuwa na wajibu wa kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwepo katika mikutano ya kampeni.

(2) Ratiba ya mikutano ya kampeni za Uchaguzi itakayowasilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya chini ya Kanuni ya 26(3)

itakuwa ni taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni na mgombea au Chama chake hakitowajibika kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi.

(3) Mikutano ya kampeni za Uchaguzi kwa mujibu wa ratiba iliyopitishwa itaanza saa mbili asubuhi na itamalizika saa kumi na mbili kamili jioni ya kila siku ya kampeni.

Mabadiliko ya ratiba

**28.** (1) Endapo Mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kitakusudia kufanya mabadiliko ya ratiba ya mikutano ya kampeni, mgombea au chama hicho kitafanya hivyo baada ya kuwasilisha kwa maandishi mapendekezo ya mabadiliko hayo kwa Msimamizi wa Uchaguzi na mapendekezo hayo kuridhiwa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (2).

(2) Msimamizi wa Uchaguzi ataitisha kikao na Vyama vya Siasa vinavyoshiriki uchaguzi ili kujadili maombi ya mabadiliko ya ratiba na mabadiliko yatakayokubaliwa yatawasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya kwa ajili ya kupatiwa ulinzi siku ya mkutano wa kampeni.

Masharti ya kampeni

**29.** (1) Mgombea, mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kitatakiwa kuendesha mikutano ya kampeni za uchaguzi kwa mujibu wa ratiba na kwa kuzingatia muda uliowekwa chini ya Kanuni hizi.

(2) Mgombea au mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea hakitaruhusiwa kuendesha kampeni za uchaguzi kwa:

(a) kutumia rushwa;

(b) kutoa maneno ya kashfa au lugha za matusi;

(c) kufanya ubaguzi wa jinsia, maumbile, ulemavu, dini, rangi, kabila au ubaguzi mwingine wa aina yoyote; au

(d) kutoa maneno ambayo yanaweza kusababisha uvunjifu wa amani au kusababisha vurugu.

## SEHEMU YA SABA
## TARATIBU ZA UPIGAJI KURA

Mahali, vituo na muda wa kupigia kura

**30.** (1) Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji utafanyika katika Vitongoji vilivyomo katika Mamlaka ya Mji Mdogo.

(2) Vituo vya kupigia kura vitakuwa katika majengo ya

umma yaliyopo katika Kitongoji husika na endapo Kitongoji hakina majengo ya umma, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kushauriana na wagombea au vyama vya siasa vyenye wagombea, atateua eneo lingine kuwa kituo cha kupigia kura.

(3) Kura zitapigwa kuanzia saa mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi kamili jioni.

(4) Baada ya saa kumi kamili, askari atakaa nyuma ya mpiga kura wa mwisho ili kuzuia watu waliochelewa kupiga kura.

Masanduku ya kura

**31.** (1) Kutakuwa na sanduku maalum la kupigia kura lililotengenezwa kwa namna itakayomwezesha mpiga kura kutumbukiza kura yake kwa urahisi kwa kila ngazi itakayopigiwa kura bila ya kuruhusu kura hiyo kutolewa ndani ya sanduku hilo.

(2) Kabla ya kuanza kupiga kura, Msimamizi wa Kituo atawaonesha wapiga kura sanduku la kupigia kura lililo wazi na atalifunga kwa lakiri kwa namna ambayo itazuia kufunguliwa bila kukata lakiri.

Karatasi za kupigia kura

**32.** Kutakuwa na karatasi za kupigia kura kwa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji ambazo zitakuwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Utambulisho wa mpiga kura

**33.** (1) Msimamizi wa Kituo atatakiwa, kabla ya kumpatia mpiga kura karatasi za kupigia kura, kujiridhisha kama jina la mpiga kura huyo limeorodheshwa katika Orodha ya Wapiga Kura.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni Ndogo ya (1), Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura aoneshe kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye Orodha ya Wapiga Kura.

(3) Aina ya kitambulisho ambacho Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura kuonesha ni pamoja na:

(a) kitambulisho cha mpiga kura;

(b) kitambulisho cha kazi;

(c) hati ya kusafiria;

(d) kadi ya bima ya afya;

(e) kitambulisho cha shule au chuo;

(f) kitambulisho cha mifuko ya hifadhi ya jamii;

(g) leseni ya udereva; au
(h) kitambulisho cha taifa.

(4) Endapo mpiga kura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote kati ya vilivyotajwa chini ya Kanuni Ndogo ya (3) lakini jina lake limo kwenye orodha ya wapiga kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi wa Kituo atamruhusu mtu huyo kupiga kura baada ya kutambuliwa na wakazi wa eneo husika.

Upigaji kura

**34.** (1) Kura zitapigwa katika namna itakayozingatia usiri.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 33, Msimamizi wa Kituo atampatia mpiga kura karatasi moja ya kupigia kura kwa nafasi ya mwenyekiti wa Kitongoji.

(3) Mpiga kura, baada ya kupewa karatasi ya kupigia kura, atapiga kura moja kwa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji.

(4) Baada ya kupiga kura, mpiga kura atatakiwa kuchovya kidole cha mkono katika kidau cha wino.

(5) Wakati wa kupiga kura watu wafuatao wataruhusiwa kushuhudia kura zinavyopigwa:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;
(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(c) askari au afisa wa polisi, mgambo mwenye sare au afisa yeyote anayesimamia ulinzi ambaye atatambuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(d) Wakala wa Chama cha Siasa chenye mgombea; na
(e) mwangalizi wa Uchaguzi mwenye kitambulisho.

(6) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, mtu yeyote hatoruhusiwa kubaki katika eneo la Kituo cha Kupigia Kura baada ya kupiga kura.

Usaidizi kwa wenye mahitaji maalum

**35.** (1) Mpiga kura ambaye:

(a) kwa sababu ya ulemavu wa macho au ulemavu mwingine wowote; au
(b) hajui kusoma na kuandika,

anaweza kumwomba mtu yeyote kumsaidia kupiga kura; isipokuwa mpiga kura huyo hataruhusiwa kumchagua Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, mgombea au wakala wake.

(2) Bila kuathiri masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), mtu mmoja hataruhusiwa kumsaidia mpiga kura zaidi ya mmoja.

Kuahirisha upigaji kura

**36.** Endapo siku ya kupiga kura kutatokea jambo lolote litakalozuia upigaji kura kuendelea kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada ya kuwasiliana na Msimamizi wa Uchaguzi ataahirisha upigaji kura hadi siku inayofuata au siku nyingine anayoona inafaa ambayo haitazidi siku saba tangu siku ya Uchaguzi ulipoahirishwa.

## SEHEMU YA NANE
## KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

Kuhesabu kura

**37.** (1) Kura zitahesabiwa na Msimamizi wa Kituo kwenye kituo cha kupigia kura mbele ya wagombea au mawakala wao.

(2) Msimamizi wa Kituo, kabla ya kuanza kuhesabu kura, atafanya yafuatayo mbele ya wagombea au mawakala wao:

(a) atahakiki idadi ya wakazi waliopiga kura;
(b) atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka katika bahasha maalum;
(c) atakagua lakiri na kuona kama haijafunguliwa;
(d) atakata lakiri; na
(e) atafungua sanduku la kupigia kura.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), wakati wa kuhesabu kura watu wafuatao wataruhusiwa kushuhudia kura zinavyohesabiwa:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;
(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(c) askari au Afisa wa Polisi, Mgambo wenye sare au Afisa yeyote anayesimamia ulinzi; na
(d) mwangalizi wa Uchaguzi mwenye kitambulisho.

Matokeo ya Mwenyekiti wa Kitongoji

**38.** (1) Msimamizi wa Kituo atamtangaza mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Kitongoji.

(2) Endapo idadi ya kura kwa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji italingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi wa Kituo atatangaza matokeo hayo na kuwasilisha taarifa ya uchaguzi huo kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atapanga tarehe nyingine ya Uchaguzi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uchaguzi.

(3) Matokeo ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji yatajazwa kwenye fomu ya matokeo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi ambayo itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi wa Kituo na kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo ya Uchaguzi.

Taratibu za kurudia Uchaguzi

39. (1) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, Uchaguzi wa marudio unaotokana na kulingana kwa idadi ya kura utahusisha wagombea ambao idadi ya kura zao zimelingana na itachukuliwa kuwa wagombea hao wameshateuliwa kuwa wagombea kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Wagombea wanaoshiriki katika Uchaguzi wa marudio au Vyama vyao vya Siasa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) havitaruhusiwa kufanya kampeni za Uchaguzi wa marudio.

Masuala yasiyobatilisha matokeo

40. Masuala yafuatayo hayatobatilisha matokeo ya uchaguzi au utekelezaji wa shughuli yoyote ya Uchaguzi:

(a) kutokuwepo kwa mgombea au wakala wa mgombea wakati wa kupiga kura, kuhesabu kura au kutangaza matokeo; au

(b) mgombea au wakala wa mgombea kukataa kusaini fomu ya matokeo.

Malalamiko kuhusu uendeshaji wa Uchaguzi

41. Mgombea yeyote ambaye hakuridhika na matokeo ya Uchaguzi au uendeshaji wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya siku thelathini tangu siku ya kutangaza matokeo ya Uchaguzi.

SEHEMU YA TISA
NAFASI WAZI NA UCHAGUZI MDOGO

Nafasi wazi

42. (1) Nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji itakuwa wazi endapo yatatokea mambo yafuatayo:
(a) kifo cha Mwenyekiti;
(b) Mwenyekiti kujiuzulu wadhifa wake;
(c) Mwenyekiti kukosa sifa za kuwa mgombea;
(d) kubatilishwa kwa matokeo ya Uchaguzi;
(e) Mwenyekiti kukoma kuwa mwanachama wa Chama cha Siasa kilichomdhamini;
(f) Mwenyekiti kuhama Kitongoji;
(g) Mwenyekiti kutoitisha mikutano mitatu ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu za msingi;
(h) Mwenyekiti kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya kawaida bila kuwa na sababu ya msingi;
(i) kugawanywa Kitongoji; au
(j) Mwenyekiti au Mjumbe kuvuliwa madaraka kwa mujibu wa Sheria.

(2) Endapo litatokea jambo lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii, Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo atatoa taarifa kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika kipindi kisichozidi siku saba tangu kutokea kwa jambo hilo.

Uchaguzi Mdogo

43. (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza kuwepo kwa nafasi wazi ya uenyekiti wa Kitongoji ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo juu ya kuwepo kwa nafasi iliyoachwa wazi.

(2) Nafasi wazi ya uenyekiti wa Kitongoji itajazwa kwa kufanya Uchaguzi Mdogo kwa utaratibu uliopo katika Kanuni hizi.

(3) Nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji itajazwa katika muda wa siku sitini baada ya kutangazwa kuwa wazi.

(4) Uchaguzi Mdogo hautafanyika chini ya Kanuni hizi endapo muda uliosalia kabla ya Uchaguzi wa kawaida ni miezi sita au pungufu yake.

## SEHEMU YA KUMI
## UTARATIBU WA KUAPISHWA

Kiapo

**44.** (1) Wafuatao watatakiwa kuapa kiapo cha uaminifu na kutunza siri mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao chini ya Kanuni hizi:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;
(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(c) Msimamizi wa kituo;
(d) Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Rufaa;
(e) Mawakala wa Vyama vya Siasa; na
(f) Mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa kusimamia shughuli za uchaguzi chini ya Kanuni hizi.

(2) Endapo Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya hawezi kupatikana, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza kuwaapisha watu waliotajwa katika aya za (c), (d), (e) na (f) za Kanuni Ndogo ya (1).

(3) Wenyeviti wa Vitongoji, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao, wataapa kiapo cha utii na uadilifu mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya katika tarehe na sehemu itakayopangwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(4) Viapo vilivyotajwa katika Kanuni hii vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Tano la Kanuni hizi na watakaoapishwa watapewa nakala za viapo.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa ya Uchaguzi

**45.** (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa la uchaguzi endapo:

(a) ataharibu orodha ya wapiga kura au nyaraka zozote zinazohusiana na Uchaguzi;
(b) atatoa taarifa za uongo ili aweze kupiga kura au kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji;
(c) atajiandikisha au kupiga kura zaidi ya mara moja kwa wagombea wa nafasi moja;
(d) atatishia wapiga kura au wagombea ili kuvuruga Uchaguzi;
(e) atafanya kampeni siku ya Uchaguzi;

(f) ataonyesha ishara au kuvaa mavazi yanayoashiria kumtambulisha mgombea au Chama cha Siasa katika eneo la mita mia mbili kutoka kwenye kituo cha kupigia kura;

(g) atamzuia Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Mjumbe wa Kamati ya Rufaa au afisa wa umma aliyeteuliwa kusimamia Uchaguzi kutekeleza majukumu yake;

(h) atakiuka masharti ya kiapo chake chini ya Kanuni ya 44(1);

(i) atapatikana na karatasi za kupigia kura zaidi ya moja kwa nafasi moja inayogombewa;

(j) atavuruga ratiba ya mikutano ya kampeni ya Uchaguzi au atavunja masharti ya kampeni za Uchaguzi;

(k) atafanya jambo lolote kinyume cha Kanuni hizi;

(l) atakutwa na silaha kinyume cha Sheria kwenye eneo la uteuzi wa wagombea, mikutano ya kampeni, eneo la usikilizaji wa rufaa za wagombea, kituo cha kuandikisha wapiga kura au kituo cha kupigia na kuhesabu kura; au

(m) atatangaza matokeo ya Uchaguzi kabla hayajatangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kosa lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kinga

46. Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Wajumbe wa Kamati ya Rufaa au mtumishi yeyote wa umma aliyehusika na usimamizi wa Uchaguzi hatowajibika kwa jinai au madai au kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kiutawala kwa jambo lolote alilolifanya au kuacha kufanya kwa nia njema wakati wa kutekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MASUALA MENGINEYO

Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi

**47.** (1) Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi wataruhusiwa kuangalia uchaguzi baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

(2) Maombi ya kibali cha uangalizi wa Uchaguzi yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa ndani ya muda wa siku ishirini na moja baada ya Tangazo la Uchaguzi kutolewa.

(3) Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi watafanya shughuli za uangalizi kwa gharama zao wenyewe na watatakiwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi na miongozo itakayotolewa ikiwa ni pamoja na kutoingilia kwa namna yoyote shughuli ya Uchaguzi.

Taratibu za Maadili

**48.** Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi, kutakuwa na Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zilizoainishwa katika Jedwali la Sita la Kanuni hizi ambazo zitatakiwa kufuatiwa na wadau wa Uchaguzi walioainishwa katika Taratibu hizo.

Miongozo

**49.** Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi, Waziri anaweza kutoa miongozo mbalimbali kuhusu Uchaguzi.

Elimu ya Mpiga Kura

**50.** (1) Taasisi yoyote inayotaka kutoa elimu ya mpiga kura katika Uchaguzi itatakiwa kuwasilisha maombi ya kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya serikali za mitaa kwa kuzingatia miongozo itakayotolewa.

(2) Taasisi zitakazotoa elimu ya mpiga kura zitatoa elimu hiyo kwa gharama zao.

Kufutwa kwa Kanuni za Uchaguzi Tangazo la Serikali Na. 320 la Mwaka 2014

**51.** (1) Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo za Mwaka 2014 zinafutwa.

(2) Bila kujali masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), matangazo, machapisho, miongozo, taratibu au kitu chochote kinachohusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambacho kilikuwa kinatumika kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, kitaendelea

kutumika hadi pale kitakapofutwa na matangazo, machapisho, miongozo, taratibu au kitu chochote kitakachotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi isipokuwa tu kama machapisho, miongozo, taratibu au kitu hicho kinakinzana na Kanuni hizi.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 10(1))*

**FOMU Na. 1**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**ORODHA YA WAPIGA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2019**

**MAMLAKA YA MJI MDOGO……………………………**
**HALMASHAURI………………………………………….**
**KITONGOJI………………………………………………**

| Na. | Jina la Mpiga Kura *(Majina matatu)* | Jinsi (Me/Ke) | Umri | Tarehe ya kuandikishwa | Saini/Dole gumba la aliyeandikishwa | Saini ya Mwandikishaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |
| 5. | | | | | | |
| 6.. | | | | | | |
| 7. | | | | | | |
| 8. | | | | | | |
| 9. | | | | | | |
| 10. | | | | | | |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 16 (5)*

**FOMU Na. II**

**FOMU YA MAOMBI YA UTEUZI KUGOMBEA UENYEKITI WA KITONGOJI MWAKA 2019**

| **NEMBO YA HALMASHAURI** |
|---|

**MAMLAKA YA MJI MDOGO.........................**
**HALMASHAURI ..........................................**
**KITONGOJI.........................................................**

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**
(*Ijazwe na anayeomba kugombea*)

1. Jina la Ukoo...............................................
2. Jina la Kati...............................................
3. Jina la Mwanzo.............................................
4. Jinsi (Me/Ke).............................................
5. Uraia .......................................................
6. Tarehe ya kuzaliwa........................................
7. Mahali unapoishi Kitongoji.............................
8. Namba ya Simu (kama ipo) ................................
9. Kazi/shughuli yako .........................................
10. Uwezo wa Kusoma na Kuandika
    (a) Kusoma Kiswahili Ndiyo ☐ Hapana ☐
    (b) Kuandika Kiswahili Ndiyo ☐ Hapana ☐
    (c) Kusoma Kiingereza Ndiyo ☐ Hapana ☐
    (d) Kuandika Kiingereza Ndiyo ☐ Hapana ☐

11. Jina la Chama cha Siasa kinachomdhamini.......................................

12. Namba ya Kadi ya Uanachama..................................................
    tarehe ilipotolewa........................mahali ilipotolewa.........................

13. Nafasi anayoomba kugombea...................................................

Nathibitisha kwamba taarifa zote zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo.

Saini ya Mgombea ............................Tarehe .......................................

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

(*Ijazwe na Chama cha Siasa*)

Hii ni kuthibitisha kuwa ......................................(*Taja jina la Mgombea*) ni Mwanachama na amedhaminiwa na ..................................................(*Taja jina la Chama*)

1. Jina: ................................................
2. Saini:...... .........................................
3. Wadhifa: ..........................................
4. Tarehe: ..............................................
5. Anwani:..........................................
6. Muhuri wa Chama cha Siasa:...............

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu.....................................................
2. Muda (saa)..............................................................................
3. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi................................
4. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi..................................
5. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ...........................

**SEHEMU D: UTEUZI**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa........................................kugombea nafasi

   ya .....................................................

2. Sababu……………………………………………………………………

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………………………

4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi …………………………

5. Tarehe……………………………………………………………………

6. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ………………………

**FOMU Na. III**

**TAMKO LA MGOMBEA LA KUHESHIMU NA KUTEKELEZA TARATIBU ZA MAADILI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2019**

***(Fomu hii ijazwe na kurudishwa pamoja na Fomu ya Uteuzi )***

Mimi……………………………………………ambaye ninatarajia kuwa mgombea wa nafasi ya ……………………………………………………………niliyependekezwa na Chama cha…………………………………………………… kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 ninatamka kuwa nitaheshimu na kutekeleza Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 wakati wote wa uchaguzi.

Ninatoa Tamko hili nikiamini kuwa yote niliyoeleza hapo juu ni kweli kwa kadri ya ufahamu wangu.

Saini ya Mgombea………………………………
Anwani……………………………………………
Namba ya Simu……………………………………

Tamko hili limetolewa mbele yangu saa…………………… tarehe………… mwezi…………
Mwaka 20…………

Saini……………………………………………
Jina………………………………………………
Wadhifa MSIMAMIZI WA UCHAGUZI/MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI*
*futa isiyohitajika.

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 32)*

**FOMU Na. IV**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA NAFASI YA MWENYEKITI WA KITONGOJI MWAKA 2019**

| |
|---|
| **NEMBO YA HALMASHAURI** |

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 38(3))*

**FOMU Na. V**

**FOMU YA MATOKEO YA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KITONGOJI**

| **NEMBO YA HALMASHAURI** |
|---|

| **Na.** | **JINA LA MGOMBEA** | **CHAMA CHA SIASA** | **KURA ALIZOPATA** | **JINSI(KE/ME)** | **SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| 5. | | | | | |
| 6. | | | | | |
| 7. | | | | | |
| 8. | | | | | |
| 9. | | | | | |
| 10. | | | | | |

| | |
|---|---|
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | |
| Idadi ya waliopiga kura | |
| Idadi ya kura halali | |
| Idadi ya kura zilizoharibika | |
| Jina la Msimamizi wa Kituo | |

Saini……………………………………………………………tarehe………. ……
Muhuri wa Msimamizi wa Kituo…………………………………………………..

## JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 44(4))*

### VIAPO

*(a) Kiapo cha Uaminifu*

"Mimi ………………………………. naapa/natamka kwa dhati kwamba nitaitumikia vyema na kwa moyo thabiti Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi yangu kama …………………………………katika Halmashauri ya …………………… na katika kutimiza wajibu wa nafasi hiyo nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kwa vyovyote vile sitatoa siri zinazohusu majukumu yangu isipokuwa kwa mujibu wa sheria. Ewe Mwenyezi Mungu, nisaidie."

**Kiapo/Tamko hili limetolewa hapa: …………………………………………**

na………………………………………………………………………………

**Leo tarehe…………………… Mwezi wa…………………..Mwaka 20…………....**

Mbele ya:

**Jina:…………………………………………………**

**Saini:…………………………………………………**

**Wadhifa:……………………………………………**

**Anuani…………………………………………………**

*(b) Kiapo cha Utii na Uadilifu*

Mimi ……………………………………………………………… naapa/natamka kwa dhati kwamba nitaitumikia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wadhifa wangu wa …………………………………………… kwa uaminifu, kwa uwezo na moyo wangu wote na kwamba nitahifadhi, nitalinda na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria za Tanzania na Maadili ya Viongozi wa Umma kama yalivyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie"

**Kiapo/Tamko hili limetolewa hapa: …………………………………………**

na………………………………………………………………………………

Leo tarehe…………………… Mwezi wa…………………..Mwaka 20………

Mbele ya:…………………………………………………

**Jina:**…………………………………………………

**Cheo:**…………………………………………………

**Saini:**………………………………………………

**Anuani**………………………………………………

JEDWALI LA SITA

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 48)*

**TARATIBU ZA MAADILI**

**1.0 Jina, Matumizi, Wahusika wa Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019**

**1.1 Jina na Tarehe ya kuanza kutumika**

Taratibu hizi zitajulikana kama Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019.

**1.2 Wahusika wa Taratibu za Maadili**

Wahusika wa taratibu za Maadili hizi watakuwa wafuatao:-

(a) Vyama vya Siasa;

(b) Wagombea;

(c) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(d) Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi.

**2.0 Taratibu za Maadili**

**2.1 Wajibu wa Vyama vya Siasa na Wagombea**

Kila Chama cha Siasa na Wagombea watatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

(a) kuheshimu na kutekeleza Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi itakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni pamoja na kuzingatia matakwa ya Sheria nyingine za nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi;

(b) kuelimisha, kuhamasisha na kuwasisitiza wanachama na wafuasi wao kuheshimu Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi itakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni pamoja na Sheria nyingine za nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi;

(c) kuzingatia ratiba ya mikutano ya kampeni;

(d) kwa kushirikiana na wanachama na wafuasi wa Vyama vingine vya Siasa kuhakikisha kuwa wanachukua hatua za makusudi ili:-

(i) kufanya Uchaguzi uwe huru na wa haki;

(ii) kuzuia vitendo vya vurugu na vitisho;

(iii) kukataa aina yoyote ya ubaguzi katika misingi ya jinsia, maumbile, ulemavu, ukabila, dini au rangi; na

(iv) kueneza taarifa sahihi kuhusu mchakato wa Uchaguzi;

(e) kuchapisha vijitabu, vipeperushi, vitini, mabango na machapisho ya aina yoyote yanayoelezea sera zao baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa Uchaguzi;
(f) kutumia vyombo vya habari kutangaza sera zao kwa kuzingatia sheria zinazosimamia vyombo vya habari na Miongozo ya Uchaguzi;
(g) kujenga mazingira ambayo yatawezesha Uchaguzi kufanyika kwa uhuru na haki, ikiwa ni pamoja na kuwezesha makundi maalum kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi;
(h) kuhakikisha hifadhi na usafi wa mazingira katika kusambaza matangazo ya kampeni;
(i) kuondoa mabango, matangazo na machapisho ya aina yoyote ile yaliyotumika wakati wa kampeni katika sehemu za wazi baada ya Uchaguzi;
(j) kutoa taarifa mara moja kwa mamlaka husika wanapofahamu au wanapoona tukio linaloweza kusababisha vurugu au uvunjifu wa amani;
(k) kuhakikisha kuwa wanafanya kampeni kwa kuzingatia misingi inayolenga kutangaza sera za Vyama vyao pasipo kujenga chuki, kusababisha mifarakano na migawanyiko katika jamii;
(l) kuchukua hatua za lazima kuhakikisha kuwa hakuna migongano ya mikutano ya kampeni na Vyama vingine;
(m) kukataza wanachama au wafuasi kutamka kauli mbiu, kuonesha ishara za Vyama vyao, au kuvaa sare zenye rangi ya Chama chao katika mikutano ya hadhara ya Vyama vingine; na
(n) kuwaelekeza Mawakala wao watakaokuwepo katika Vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi.

**2.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Vyama vya Siasa na Wagombea**

Kila Chama cha Siasa au Mgombea hatatakiwa kufanya yafuatayo:-

(a) kusababisha au kufanya fujo au vurugu ya aina yoyote katika Mkutano wake au wa Chama kingine;
(b) kutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji na vitisho au lugha inayochochea uvunjifu wa amani au kuashiria ubaguzi wa kijinsia, dini, rangi, ulemavu au maumbile kwenye mikutano ya kampeni;
(c) kubeba sanamu, kinyago au kitu chochote ambacho kinaonyesha kudhalilisha, kukebehi, kufedhehesha au kukejeli Chama kingine cha Siasa au Mgombea au Kiongozi wa Chama kingine cha Siasa au Serikali katika mkutano wowote wa kampeni za Uchaguzi;
(d) kutumia vipaza sauti vya aina yoyote kwa shughuli za kisiasa mara baada ya muda wa kampeni za Uchaguzi kumalizika;
(e) kuchafua, kubandua au kuharibu kwa namna yoyote ile matangazo ya kampeni ya Vyama vingine vya Siasa na matangazo mengine yanayotolewa na Mamlaka za Uchaguzi;

(f) kubandika mabango ya kampeni, matangazo au mchoro wowote kwenye nyumba, majengo au vyombo vya usafiri vya watu binafsi au taasisi mbalimbali bila idhini ya wamiliki husika;
(g) kubandika mabango ya kampeni, matangazo au mchoro wowote kwenye nyumba za ibada, taasisi za dini na majengo ya Serikali na taasisi zake;
(h) kutoa rushwa ili kumshawishi mtu yeyote kupiga kura, kugombea au kujitoa katika kugombea nafasi ya uongozi;
(i) kuzuia mtu yeyote, watu au wafuasi wa vyama vingine kuhudhuria mikutano ya kampeni au kupiga kura;
(j) kukodi au kutumia usafiri wa aina yoyote kubeba na kusafirisha wapiga kura kwa madhumuni ya kushawishi kupigiwa kura.

**2.3 Maadili wakati wa kupiga, kuhesabu, kujumlisha kura na kutangaza matokeo ya Uchaguzi**

**2.3.1. Yanayotakiwa Kufanywa**

(a) Vyama vya Siasa na Wagombea watahakikisha kuwa Mawakala wao wanakula kiapo na kukiwasilisha kwa Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kabla ya siku ya Uchaguzi;
(b) Mawakala wa Vyama vya Siasa, Vyama vya Siasa na Wagombea watakuwa na wajibu wa kushirikiana na Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo katika vituo vya kupigia kura kwa kuzingatia Kanuni za Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi;
(c) Viongozi wa Vyama vya Siasa watakuwa na wajibu wa kuwaelimisha wanachama na wafuasi wao kuwa, watatakiwa kuondoka eneo la kupigia Kura mara tu wamalizapo kupiga kura na kama itawalazimu kubakia katika eneo hilo watatakiwa kukaa umbali wa mita mia mbili kutoka kituo cha kupigia kura.

**2.3.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa**

(a) Kampeni za uchaguzi haziruhusiwa siku ya upigaji kura. Hii ni pamoja na kuvaa vazi lolote au kuwa na kitu chochote kinachoashiria kushawishi watu kumpigia kura Mgombea fulani au utambuzi wa Mgombea fulani au matumizi ya chombo cha usafiri kinachoashiria utambuzi wa Chama au Mgombea wa Chama chochote;
(b) Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wagombea na wafuasi wao watatakiwa kujiepusha na vitendo vinavyoweza kusababisha fujo au vurugu katika vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura;
(c) Hakuna mtu atakayeruhusiwa kutumia simu ya kiganjani ndani ya kituo cha kuhesabu na kujumlishia kura isipokuwa Msimamizi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na mlinzi wa kituo cha kupigia kura ambao watatumia simu zao pale itakapobidi kwa shughuli za Uchaguzi

tu na simu hizo wakati wote ziwe zimeondolewa mlio na ziwe kwenye mtetemo;

(d) Kiongozi au Mtendaji au mwanachama au mfuasi wa Chama cha Siasa hatatakiwa:

(i) kuvamia au kukaa kwa nguvu ndani ya kituo cha kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura;

(ii) kuwahamasisha wanachama au wafuasi kupiga kura zaidi ya mara moja katika Uchaguzi mmoja;

(iii)kununua kura au kutoa rushwa au aina yoyote ya malipo ya fedha au vifaa kwa mpiga kura au Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(iv)kutumia lugha ya matusi kwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo katika kituo cha kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura.

**3.0 Wajibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Serikali itakuwa na Wajibu wa:**

(a) kutoa fursa sawa kwa wadau wote wa Uchaguzi hususan Vyama vya Siasa na Wagombea ili kuendesha shughuli zao za kisiasa wakati wa Uchaguzi kwa uhuru na kuzingatia sheria za nchi;

(b) kuhakikisha hali ya usalama, amani na utulivu wakati wote wa Uchaguzi;

(c) kuhakikisha kuwa viongozi na watendaji wake wanazingatia ipasavyo ukomo wa madaraka yao katika shughuli za Uchaguzi.

**4.0 Taratibu za Maadili kwa Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi**

**4.1 Mambo wanayotakiwa Kufanya**

Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi watakuwa na wajibu wa kupanga, kusimamia na kuendesha Uchaguzi katika misingi inayowezesha Uchaguzi kuwa huru na wa haki kwa kufanya yafuatayo:-

(a) kuzingatia Katiba ya Nchi, Kanuni za Uchaguzi na Sheria nyingine za nchi; kuvipatia Vyama vya Siasa ratiba na taarifa za Uchaguzi mapema;

(b) kutoa Elimu ya Mpiga Kura, kusimamia na kuratibu taasisi na watu wanaotoa Elimu ya Mpiga Kura;

(c) kutoa mafunzo kwa wanaohusika na Uchaguzi ili kuwawezesha kuendesha uchaguzi kwa ufanisi;

(d) kuvipatia Vyama vya Siasa Kanuni, Miongozo ya Uchaguzi na Nyaraka nyingine zinazohusiana na Uchaguzi;

(e) kukemea vitendo vyenye nia ya kuharibu Uchaguzi vinavyoweza kufanywa na Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wagombea au wafuasi wao;

(f) kuendesha na kuziwezesha Kamati za kusimamia Maadili ya Uchaguzi na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yanayotolewa na Kamati hizo;

(g) kukutana na Vyama vya Siasa pale inapohidi kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Kampeni za Uchaguzi na Uchaguzi wenyewe;
(h) kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote atakayefanyiwa uonevu au kukoseshwa haki wakati wa shughuli za Uchaguzi;
(i) kutambua majukumu ya Vyama vya Siasa, Wagombea na Mawakala wao;
(j) kuandaa na kupeleka kwa wakati vifaa kwenye vituo vya kupigia kura;
(k) kuendesha zoezi la Uchaguzi kwa uwazi, haki na uadilifu.

**4.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi**

(a) kupendelea Chama chochote cha Siasa au Mgombea yeyote;
(b) kubadili ratiba za Kampeni za Uchaguzi bila kuvishirikisha Vyama vya Siasa;
(c) kuchelewa au kupeleka vifaa pungufu katika vituo vya kupigia kura bila sababu za msingi;
(d) kuchelewa kutangaza Matokeo ya Uchaguzi bila sababu za msingi.

**5.0 Usimamizi wa Utekelezaji waTaratibu za Maadili ya Uchaguzi**

5.1 Kamati za Maadili za kusimamia Utekelezaji wa Taratibu za Maadili ya Uchaguzi
Kutakuwa na Kamati za Maadili zifuatazo zitakazoundwa na Msimamizi wa Uchaguzi:-
(a) Kamati ya Maadili ya Halmashauri; na
(b) Kamati ya Maadili ya Kata.

**5.2 Muundo wa Kamati za Taratibu za Maadili ya Uchaguzi**

**5.2.1 Kamati ya Maadili ya Halmashauri**

Kamati ya Maadili ya Halmashauri itakuwa na wajumbe wafuatao:-
(a) Msimamizi wa Uchaguzi katika Halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
(b) Mjumbe mmoja kutoka kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi katika Halmashauri;
(c) Mjumbe mmoja atakayewakilisha Serikali ambaye atateuliwa kwa maandishi na Katibu Tawala wa Wilaya husika; na
(d) Afisa Uchaguzi ambaye atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi.

**5.2.2 Kamati ya Maadili ya Kata**

Kamati ya Maadili ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao:-
(a) Msimamizi Msaidizi ngazi ya Kata husika ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
(b) Mjumbe mmoja kutoka kila Chama cha Siasa kinachoshiriki katika Uchaguzi kwenye Kata;

(c) Mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali atakayeteuliwa kwa maandishi na Katibu Tawala wa Wilaya husika; na

(d) Katibu ambaye ni Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kijiji atakayeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

**5.2.3 Utoaji wa taarifa za Kamati za Maadili**

Itakuwa ni marufuku kwa mtu, mgombea, Chama cha Siasa au mjumbe wa Kamati ya Maadili ambaye sio Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili kutoa taarifa yoyote kuhusu maamuzi ya Kamati au suala lolote lililopo mbele ya Kamati.

**5.3 Uwasilishaji wa Malalamiko**

Mgombea yeyote, Wasimamizi au Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, Serikali au Chama chenye Mgombea kinachoamini kwamba Maadili ya Uchaguzi yamekiukwa kitawasilisha malalamiko kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Kata kwa maandishi.

**5.4 Muda wa kuwasilisha Malalamiko**

Malalamiko yoyote yatatakiwa kuwasilishwa ndani ya siku tatu tangu kutokea kwa tukio linalolalamikiwa.

**5.5 Kuitisha kikao cha Kamati ya Maadili ya Uchaguzi**

Mwenyekiti wa Kamati husika baada ya kupokea malalamiko na kujiridhisha kuwa Taratibu za Maadili zimekiukwa atatakiwa kuitisha kikao ndani ya siku mbili.

**5.6 Namna ya kushughulikia Malalamiko**

(a) Malalamiko yote yatajadiliwa na kuamuliwa katika kikao cha Kamati ya Maadili ya Kata husika;

(b) Kamati itashughulikia malalamiko na kutoa uamuzi wake mapema iwezekanavyo;

(c) Baada ya kupokea malalamiko, Kamati itamtaka aliyelalamikiwa kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku mbili tangu kupokea malalamiko;

(d) Katika kushughulikia malalamiko, Kamati inaweza kumwita mtu yeyote kutoa maelezo ili kusaidia Kamati kufikia maamuzi ya haki;

(e) Akidi ya Kikao cha Kamati husika itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa Kamati;

(f) Kamati ya Maadili ya Uchaguzi itaamua malalamiko yote baada ya kusikiliza au kupata maelezo ya utetezi kutoka kwa pande zote mbili ambazo ni mlalamikaji na mlalamikiwa ndani ya siku mbili isipokuwa kama upande unaolalamikiwa utashindwa kuwasilisha maelezo ya utetezi katika muda uliopangwa Kamati inaweza kufanya uamuzi;

(g) Maamuzi yatakayofikiwa na Kamati ya Maadili ya Kata yatatekelezwa na pande zinazohusika na maamuzi hayo;

(h) Ikitokea kuna umuhimu wa kufanya maamuzi kwa kupiga kura, wawakilishi wa Mlalamikaji na Mlalamikiwa hawataruhusiwa kupiga kura;
(i) Malalamiko yatakayoshughulikiwa na Kamati za Maadili ni yale tu yaliyotokea katika kipindi cha Kampeni;
(j) Malalamiko yatakayotokea siku ya Upigaji Kura yatashughulikiwa kwa kuzingatia Kanuni za Uchaguzi;
(k) Kamati itakuwa na mamlaka ya kuchunguza malalamiko yote yatakayowasilishwa kabla ya kufanya maamuzi;
(l) Kamati inaweza kuelekeza malalamiko mengine kwenye mamlaka zinazohusika kama itakavyoona inafaa kwa hatua zinazostahili.

**5.7 Rufaa Dhidi ya Maamuzi**

(a) Upande ambao hautaridhika na uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Kata, utakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Kamati ya Maadili ya Halmashauri ndani ya siku mbili tangu uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Kata ulipotolewa; na
(b) Uamuzi utakaotolewa na Kamati ya Maadili ya Halmashauri utakuwa ni wa mwisho.

**5.8 Malalamiko dhidi ya Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi**

(a) Pale ambapo malalamiko yaliyowasilishwa ni dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi, Msimamizi au Msimamizi Msaidizi, Msimamizi wa Uchaguzi hataendesha Kikao hicho, isipokuwa Katibu Tawala wa Mkoa atateua Afisa yeyote wa Umma Mwandamizi kutoka Sekretarieti ya Mkoa kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho;
(b) Iwapo Kamati itaona kuwa Msimamizi amekosea Kamati itamtaka Msimamizi wa Uchaguzi kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo.

**5.9 Malalamiko dhidi ya Serikali**

Kamati ya Maadili ya Kata itapokea malalamiko yatakayotolewa dhidi ya Serikali na iwapo Kamati itaona kuwa Serikali imekosea itaitaka Serikali kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo.

**5.10 Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Halmashauri na Kata katika kushughulikia Malalamiko na kutoa adhabu**

**Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Halmashauri na Kata zinaweza kuchukua hatua zifuatazo:-**

(a) kuagiza upande uliokiuka maadili kusahihisha kosa au makosa yaliyotendeka na iwapo italazimu, kuomba msamaha hadharani;
(b) kutoa onyo au karipio kwa maandishi;
(c) kutangaza jina la Chama au Mgombea aliyekiuka Maadili na kueleza kosa au makosa yake kwa njia za Taarifa kwa Umma, redio, televisheni, magazeti na njia nyingine za mawasiliano;

(d) Kamati inaweza kukisimamisha Chama au Mgombea kuendelea kufanya Kampeni za Uchaguzi kwa muda itakavyoona inafaa.

**5.11 Kushindwa Kutekeleza Maamuzi ya Kamati za Maadili**

Pale ambapo Mgombea au Chama kitashindwa kutekeleza maamuzi ya Kamati husika, Kamati ya Maadili ya Uchaguzi inaweza kukisimamisha Chama husika kufanya kampeni za Uchaguzi.

DODOMA
25/04/2019

SELEMANI S. JAFO (Mb)
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 372 la tarehe 26/04/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

SURA 288

# KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA MTAA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MTAA KATIKA MAMLAKA ZA MIJI ZA MWAKA 2019

TANGAZO LA SERIKALI NA. 372 la tarehe 26/04/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

SURA 288

Zimetungwa chini ya Kifungu 87A

KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA MTAA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MTAA KATIKA MAMLAKA ZA MIJI ZA MWAKA 2019

MPANGILIO WA KANUNI


| Kanuni | Jina | Uk |
|---|---|---|
| 1 | Jina | 43 |
| 2 | Eneo la matumizi na Tarehe ya kuanza kutumika | 43 |
| 3 | Tafsiri | 43 |
| 4 | Tangazo la uchaguzi kwa umma | 44 |
| 5 | Majina na mipaka ya Mitaa | 45 |
| 6 | Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa | 45 |
| 7 | Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi | 45 |
| 8 | Kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo | 45 |
| 9 | Maelekezo kuhusu Uchaguzi | 46 |
| 10 | Orodha ya Wapiga Kura | 46 |
| 11 | Uandikishaji wa Wapiga Kura | 47 |
| 12 | Pingamizi kuhusu uandikishaji | 47 |
| 13 | Sifa za mpiga kura | 48 |
| 14 | Kupoteza sifa ya kupiga kura | 48 |
| 15 | Sifa za Mgombea | 48 |
| 16 | Kupoteza sifa ya kuwa Mgombea | 49 |
| 17 | Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi | 50 |
| 18 | Utaratibu wa uteuzi wa Wagombea | 50 |
| 19 | Kupita bila kupingwa | 51 |
| 20 | Kujitoa kwa Mgombea | 51 |
| 21 | Kufariki kwa Mgombea | 52 |

| | | |
|---|---|---|
| 22 | Ukomo wa kuwa madarakani | 52 |
| 23 | Pingamizi kuhusu uteuzi | 52 |
| 24 | Kamati ya Rufaa | 53 |
| 25 | Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Rufaa | 53 |
| 26 | Majukumu ya Kamati ya Rufaa | 53 |
| 27 | Kampeni za Uchaguzi | 54 |
| 28 | Wajibu wa Jeshi la Polisi | 54 |
| 29 | Mabadiliko ya ratiba | 55 |
| 30 | Masharti ya Kampeni | 55 |
| 31 | Mahali vituo na muda wa kupiga kura | 55 |
| 32 | Masanduku ya kura | 56 |
| 33 | Karatasi za kupigia kura | 56 |
| 34 | Utambulisho wa mpiga kura | 56 |
| 35 | Upigaji kura | 57 |
| 36 | Usaidizi kwa wenye mahitaji maalum | 57 |
| 37 | Kuahirisha upigaji kura | 58 |
| 38 | Kuhesabu kura | 58 |
| 39 | Matokeo ya Wajumbe wa Kamati ya Mtaa | 59 |
| 40 | Matokeo ya Mwenyekiti wa Mtaa | 60 |
| 41 | Taratibu za kurudia Uchaguzi | 60 |
| 42 | Masuala yasiyobatilisha matokeo | 60 |
| 43 | Malalamiko kuhusu uendeshaji wa Uchaguzi | 61 |
| 44 | Nafasi wazi | 61 |
| 45 | Uchaguzi Mdogo | 61 |
| 46 | Kiapo | 62 |
| 47 | Makosa ya Uchaguzi | 62 |
| 48 | Kinga | 63 |
| 49 | Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi | 64 |
| 50 | Taratibu za maadili | 64 |
| 51 | Miongozo | 64 |
| 52 | Elimu ya Mpiga Kura | 64 |
| 53 | Kufutwa kwa Kanuni za Uchaguzi Tangazo la Serikali Na.322 la Mwaka 2014 | 64 |

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2019.

Eneo la matumizi na Tarehe ya kuanza kutumika

**2.** Kanuni hizi zitatumika katika Mitaa yote ilivyomo katika maeneo ya Mamlaka za Miji na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

**3.** Katika Kanuni hizi isipokuwa pale itakavyoelezwa vinginevyo:-

Sura 258

"Chama cha Siasa" maana yake ni Chama cha Siasa kilichopata usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa;

"Mamlaka ya Uchaguzi" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa:-

"mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye kwa anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Mtaa;

"Msimamizi wa Uchaguzi" maana yake ni Mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa na Mamlaka ya Uchaguzi kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi" maana yake ni afisa yeyote wa umma aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi;

Sura ya 288

"Mtaa" maana maana yake ni sehemu ya eneo la utawala katika Kata iliyoko kwenye eneo la Mamlaka ya Mji kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Mji);

"Mtendaji wa Mtaa" maana yake ni mtendaji mkuu wa shughuli za Serikali katika Mtaa na ni pamoja na mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mtendaji wa Mtaa kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"mtumishi wa umma" maana yake ni mtu yeyote aliyeajiriwa katika utumishi wa umma;

"Orodha ya Wapiga Kura" maana yake ni orodha ya majina ya wapiga kura iliyoandaliwa chini ya Kanuni hizi;

Sura 357

"raia" maana yake ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia; "

"sehemu ya matangazo ya uchaguzi" maana yake ni sehemu maalum iliyoteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa ajili ya kutolea matangazo au taarifa mbalimbali za uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"siku ya uteuzi" maana yake ni siku ya kutangaza majina ya wanaostahili na wasiostahili kugombea nafasi za uongozi chini ya Kanuni hizi;

"Uchaguzi" maana yake ni uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji;

"Uchaguzi Mdogo" maana yake ni uchaguzi ambao utafanyika baada ya kuwepo kwa nafasi wazi ya Mwenyekiti wa Mtaa au Mjumbe wa Kamati ya Mtaa;

"wakati wa uchaguzi" maana yake ni muda ambao uchaguzi wa kawaida au uchaguzi mdogo unafanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi na unaanzia tarehe ya tangazo la uchaguzi hadi matokeo ya uchaguzi yanapotangazwa;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA PILI
## TANGAZO LA UCHAGUZI

Tangazo la uchaguzi kwa umma

4. (1) Kutakuwa na uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa ambao utafanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi baada ya Waziri kutoa Tangazo la Uchaguzi kwa umma.

(2) Tangazo la Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) litatolewa katika magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa nchi nzima na katika vyombo mbalimbali vya habari si chini ya siku tisini kabla ya siku ya uchaguzi.

(3) Tangazo litakalotolewa na Waziri litaelekeza mambo yafuatayo:

(a) ratiba ya uchaguzi na shughuli zinazohusika; na

(b) masharti muhimu ya uchaguzi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi.

Majina na mipaka ya Mitaa

5. Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza katika sehemu ya matangazo ya uchaguzi majina na mipaka ya Mitaa iliyomo katika eneo la Halmashauri husika kwa kuzingatia orodha ya Mitaa iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali siku sabini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa.

Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa

6. Kamati ya Mtaa itakuwa na Wajumbe wasiozidi sita ambao ni:

(a) Mwenyekiti wa Mtaa;

(b) Wajumbe wengine watano ambao kati yao Wajumbe wawili watakuwa wanawake.

Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi

7. (1) Kutakuwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo au mtumishi wa umma atakayeteuliwa kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Mtu hatateuliwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi endapo ni:

(a) Kiongozi wa chama cha siasa;

(b) Mgombea;

(c) Hakimu au Jaji;

(d) Kiongozi wa dini;

(e) Askari wa jeshi lolote;

(f) Katibu Tawala wa Wilaya;

(g) Katibu Tawala wa Mkoa;

(h) Mkuu wa Wilaya; au

(i) Mkuu wa Mkoa.

Kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo

8. Kila Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Wajumbe wa Kamati ya

Rufaa au mtumishi wa umma atakayeteuliwa kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi atasimamia Uchaguzi kwa kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo yatakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TATU
## MAELEKEZO YA UCHAGUZI

Maelekezo kuhusu uchaguzi

9. (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya Uchaguzi siku sitini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.

(2) Maelekezo ya Uchaguzi, kwa mujibu wa Kanuni hizi, yataelekeza mambo yafuatayo:

(a) tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi;

(b) muda na sehemu ya kuandikisha wapiga kura;

(c) muda na mahali pa kufanyia Uchaguzi;

(d) kuwataka wakazi wote wenye sifa za kupiga kura washiriki Uchaguzi;

(e) kuwataka wakazi wenye umri wa miaka ishirini na moja au zaidi wanaotaka kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa kuchukua fomu za kugombea zitakazopatikana kwenye ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(f) tarehe na muda wa kuchukua na kurudisha fomu za maombi ya kugombea uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(g) siku ambayo uteuzi utafanyika na sehemu ya matangazo ya uchaguzi ambapo fomu za wagombea zitabandikwa;;

(h) muda wa kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi na kusikilizwa kwa pingamizi;

(i) tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(j) kipindi cha kuendesha mikutano ya kampeni za Uchaguzi; na

(k) masuala mengine yanayohusu Uchaguzi.

Orodha ya Wapiga Kura

10. (1) Kutakuwa na Orodha ya Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni Ndogo ya (1), Msimamizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa Watumishi wa umma watakaoandikisha na kuandaa

Orodha ya Wapiga Kura katika Mitaa siku hamsini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.

(3) Watendaji wa Mitaa na Kata hawatateuliwa wala hawataruhusiwa kuandikisha au kuandaa orodha ya wapiga kura.

Uandikishaji wa Wapiga Kura

**11.** (1) Uandikishaji na uandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura utaanza siku ya arobaini na saba kabla ya siku ya Uchaguzi na utafanyika kwa muda wa siku saba kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi katika majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na Viongozi wa Vyama vya Siasa;

(2) Vituo vya uandikishaji wa wapiga kura vitafunguliwa saa mbili kamili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili kamili jioni.

(3) Chama cha Siasa kitaruhusiwa kuteua wakala wake kwa kila kituo cha uandikishaji wa wapiga kura wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.

(4) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika sehemu ya matangazo ya uchaguzi nakala ya Orodha ya Wapiga Kura siku moja baada ya kukamilika kwa uandikishaji wa wapiga kura na atatunza nakala halisi ya Orodha hiyo.

(5) Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya Wapiga Kura atakuwa na haki ya kukagua Orodha ya Wapiga Kura katika muda wa siku saba tangu tarehe ya Orodha hiyo kubandikwa sehemu ya matangazo ya uchaguzi ili:

- (a) kuweka pingamizi kuhusu usahihi wa Orodha hiyo;
- (b) kuomba Orodha irekebishwe kwa:-
    - (i) kuongeza jina lake;
    - (ii) kubadilisha taarifa zilizoko katika Orodha hiyo; au
    - (iii) kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa amefariki.

Pingamizi kuhusu uandikishaji

**12.** (1) Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya wapiga Kura anaweza kuweka pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura kabla ya kumalizika kwa muda wa kukagua Orodha ya Wapiga Kura.

(2) Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa

Uchaguzi ambaye atatakiwa kutoa uamuzi kuhusu pingamizi lililowekwa ndani ya siku mbili tangu tarehe ya mwisho ya ukaguzi wa Orodha ya Wapiga Kura.

(3) Endapo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataridhika na pingamizi lililowekwa chini ya Kanuni hii, atarekebisha Orodha ya Wapiga Kura iliyotangazwa baada ya muda wa siku mbili isipokuwa kama uamuzi wake umekatiwa rufaa.

(4) Endapo mtu aliyeweka pingamizi au aliyewekewa pingamizi hatoridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi lililowasilishwa kwake, mtu huyo atawasilisha rufaa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ndani ya muda wa siku mbili tangu kutolewa kwa uamuzi wa pingamizi.

(5) Msimamizi wa Uchaguzi, baada ya kupokea rufaa hiyo, ataishughulikia na kuitolea uamuzi ndani ya muda wa siku nne tangu siku ya kupokea rufaa hiyo.

(6) Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni Ndogo ya (4) utakuwa wa mwisho.

Sifa za mpiga kura

**13.** Mkazi yeyote wa Mtaa atakuwa na haki ya kupiga kura endapo atakuwa na sifa zifuatazo:

(a) ni raia wa Tanzania;

(b) ana umri wa miaka kumi na nane au zaidi;

(c) ni mkazi wa eneo la Mtaa;

(d) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu; na

(e) awe amejiandikisha kupiga kura katika Mtaa husika.

Kupoteza sifa ya kupiga kura

**14.** Mtu hatakuwa na haki ya kupiga kura endapo:

(a) hana mojawapo ya sifa zilizoainishwa katika Kanuni ya 13; au

(b) amejiandikisha kupiga kura katika kituo zaidi ya kimoja.

Sifa za Mgombea

**15.** Mkazi yeyote wa Mtaa anaweza kugombea uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa endapo:-

(a) ni raia wa Tanzania;

(b) ana umri wa miaka ishirini na moja au zaidi;

(c) ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;

(d) ana shughuli halali ya kumwezesha kuishi;
(e) ni mkazi wa eneo la Mtaa;
(f) ni mwanachama wa Chama cha Siasa na amedhaminiwa na Chama hicho;
(g) hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya Uchaguzi; na
(h) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

Kupoteza sifa ya kuwa mgombea

**16.** (1) Mtu hatakuwa na sifa za kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa endapo:
(a) amepoteza au hana sifa za mgombea zilizoainishwa katika Kanuni ya 14;
(b) amehukumiwa hukumu ya kifo na Mahakama za Tanzania au anatumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita jela;
(c) ana mkataba au maslahi kwenye kampuni ambayo ina mkataba na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo anagombea nafasi ya uongozi na hajatangaza kuwepo kwa mkataba au maslahi yake kupitia kwenye gazeti linalopatikana katika eneo husika au mbao za matangazo katika ofisi ya Mtaa;
(d) amepoteza sifa ya kupiga kura chini ya Kanuni hizi au kwa mujibu wa Sheria yeyote inayohusu makosa ya uchaguzi;
(e) hatojaza fomu ya tamko la kuheshimu taratibu za maadili; au
(f) ataajiriwa au kuteuliwa katika wadhifa wowote katika Utumishi wa Umma au kuchaguliwa katika nafasi ya udiwani, ubunge, uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umakamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni ya 16(1)(b):
(a) adhabu mbili au zaidi za kifungo zinazotakiwa kutumikiwa kwa kufuatana zitachukuliwa kuwa ni adhabu tofauti iwapo kati ya adhabu hizo hakuna inayozidi miezi sita jela lakini endapo kati ya adhabu hizo kuna inayozidi miezi sita jela itachukuliwa kuwa ni adhabu moja; au

(b) kifungo cha jela kilichosababishwa na kushindwa kuiipa faini hakitohesabiwa kuwa ni adhabu ya kifungo.

SEHEMU YA NNE
UTEUZI WA WAGOMBEA

Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi

**17.** (1) Mtu yeyote anayekusudia kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa atatakiwa kuchukua fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi husika siku zisizopungua ishirini na sita kabla ya siku ya uchaguzi kwa kadri itakavyoelekezwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(2) Mtu aliyechukua fomu kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) atatakiwa kurejesha fomu husika ndani ya muda wa siku saba tangu siku ya kwanza ya uchukuaji wa fomu iliyotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(3) Fomu za uteuzi wa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa zitatolewa na kupokelewa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

(4) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hatoruhusiwa kupokea kutoka kwa mtu yeyote fomu za uteuzi zitakazowasilishwa baada ya saa kumi kamili jioni ya siku ya mwisho ya kurejesha fomu.

(5) Fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa itakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

Utaratibu wa uteuzi wa Wagombea

**18.** (1) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa Mtaa na ujumbe wa Kamati ya Mtaa siku kumi na tisa kabla ya tarehe ya Uchaguzi kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

(2) Baada ya uteuzi kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika majina ya wagombea wenye sifa na wasio na sifa za kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

(3) Endapo baada ya saa kumi kamili jioni ya siku ya uteuzi kutakuwa hakuna mwombaji aliyejitokeza au kama waombaji wote waliojitokeza hawana sifa zinazostahili, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi

atavitaarifu Vyama vya Siasa na wakazi wa Mtaa kuhusu kukosekana kwa waombaji au kutokuwepo kwa waombaji wenye sifa.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni Ndogo ya (3), Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atavitaarifu Vyama vya Siasa na wakazi wa Mtaa husika kuhusu kurudiwa kwa mchakato wa uchaguzi baada ya siku arobaini kuanzia tarehe ya uteuzi.

Kupita bila kupingwa

**19.** (1) Endapo siku ya uteuzi kutakuwa na mwombaji mmoja aliyejitokeza katika nafasi ya uenyekiti wa Mtaa na mwombaji huyo akateuliwa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mwombaji huyo kuwa ni mshindi wa nafasi aliyoomba kugombea kwa kupita bila kupingwa..

(2) Endapo idadi ya waombaji wa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Mtaa kwa kundi mchanganyiko yaani wanaume na wanawake au kwa kundi la wanawake waliojitokeza na kuteuliwa itakuwa sawa na idadi ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni ya 6 ya Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza waombaji hao kuwa ni washindi wa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Mtaa kwa kupita bila kupingwa.

(3) Endapo idadi ya waombaji wa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Mtaa kwa kundi mchanganyiko yaani wanaume na wanawake au kwa kundi la wanawake itakuwa chini ya idadi ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni ya 6 ya Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi atawatangaza waombaji hao kuwa ni washindi wa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Mtaa kwa kupita bila kupingwa na taratibu za kujaza nafasi zilizobaki zitaanza baada ya siku arobaini kuanzia tarehe ya uteuzi .

Kujitoa kwa Mgombea

**20.** (1) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea aliyeteuliwa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa atajitoa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi wa mgombea huyo na wagombea waliobaki watapigiwa kura ili kupata mshindi.

(2) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea aliyeteuliwa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa atajitoa na kubaki mgombea mmoja wa nafasi hiyo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyebaki kuwa mshindi wa nafasi iliyoombwa kwa kupita bila kupingwa.

(3) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea wa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Mtaa atajitoa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi huo na wagombea waliobaki wataendelea na hatua ya uchaguzi ili kumpata mshindi.

Kufariki kwa mgombea

**21.** (1) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Mtaa atafariki, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha Uchaguzi wa nafasi hiyo na Chama cha Siasa kilichotoa mgombea aliyefariki kinaweza kuwasilisha jina la mwombaji mwingine ndani ya siku arobaini tangu kuahirishwa kwa Uchaguzi ili hatua za uteuzi wa mgombea huyo zifanyike.

(2) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea wa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Mtaa atafariki, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha Uchaguzi wa nafasi hiyo na Chama cha Siasa kilichotoa mgombea aliyefariki kinaweza kuwasilisha jina la mwombaji mwingine ndani ya siku arobaini tangu kuahirishwa kwa Uchaguzi ili hatua ya uteuzi wa mwombaji huyo zifanyike.

Ukomo wa kuwa madarakani

**22.** Mwenyekiti wa Mtaa na Mjumbe wa Kamati ya Mtaa watakoma kushika nafasi hizo siku saba kabla ya siku ya kuchukua fomu za kugombea uongozi chini ya Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TANO
## UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA PINGAMIZI NA RUFAA

Pingamizi kuhusu uteuzi

**23.** (1) Mtu yeyote aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au anapinga uteuzi wa mgombea yeyote, anaweza kuwasilisha pingamizi na kumwomba Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kupitia upya uamuzi uliofanyika ili amteue kuwa mgombea au atengue uteuzi anaoupinga na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kupitia pingamizi husika, anaweza kukubali au kulikataa pingamizi hilo.

(2) Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii litawasilishwa kwa maandishi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika muda wa siku mbili

tangu uamuzi au uteuzi ulipofanyika na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili kuanzia siku ya kupokea pingamizi hilo.

(3) Mwombaji au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa iliyoanzishwa chini ya Kanuni ya 24 katika muda usiozidi siku nne kuanzia tarehe ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Kamati ya Rufaa

**24.** (1) Kutakuwa na Kamati ya Rufaa katika kila Wilaya ambayo itasikiliza mapingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea wa Uchaguzi katika Wilaya husika.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Rufaa watateuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa siku saba kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Kanuni ya 25.

(3) Kamati ya Rufaa itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Katibu Tawala wa Wilaya ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) watumishi wanne wa umma kutoka taasisi za umma zilizopo katika Wilaya husika; na

(c) mtumishi mmoja wa umma ambaye atakuwa Katibu na hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Rufaa

**25.** Mtu yeyote hatateuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Rufaa endapo:

(a) anahusika na uteuzi wa wagombea

(b) ni Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo;

(c) ni mtumishi wa Halmashauri; au

(d) kiongozi wa Chama cha Siasa katika ngazi yoyote.

Majukumu ya Kamati ya Rufaa

**26.** (1) Kamati ya Rufaa itakuwa na majukumu ya kupokea, kusikiliza na kutoa uamuzi wa rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni ya 23(3).

(2) Kamati ya Rufaa itatoa uamuzi wa rufaa ndani ya muda wa siku nne kuanzia siku ya kupokea rufaa na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(3) Mtu aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamati ya Rufaa atakuwa na haki ya kufungua shauri katika Mahakama ya

Wilaya ndani ya muda wa siku thelathini baada ya matokeo ya Uchaguzi kutangazwa.

SEHEMU YA SITA
KAMPENI ZA UCHAGUZI

Kampeni za Uchaguzi

**27.** (1) Kampeni za Uchaguzi zitafanyika siku saba kabla ya siku ya Uchaguzi.

(2) Kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi kitawasilisha ratiba yake ya mikutano ya kampeni ya uchaguzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si chini ya siku saba kabla ya kuanza kwa kampeni.

(3) Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha ratiba za mikutano ya kampeni zilizowasilishwa na Vyama vya Siasa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (2) baada ya maridhiano na Vyama vya Siasa vinavyoshiriki Uchaguzi na atatakiwa kuwasilisha ratiba ya mikutano ya kampeni za uchaguzi iliyounganishwa siku tatu kabla ya kampeni kuanza kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

(4) Endapo Vyama vya Siasa vitashindwa kuridhiana wakati wa uunganishaji wa ratiba za mikutano ya kampeni, Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha ratiba za mikutano ya kampeni na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(5) Mgombea au mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kinaweza kuitisha na kuhutubia mikutano ya kampeni kwa mujibu wa ratiba ya mikutano ya kampeni iliyoandaliwa na kuwasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya na mikutano hiyo itaratibiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Wajibu wa Jeshi la Polisi

**28.** (1) Mkuu wa Polisi wa Wilaya atakuwa na wajibu wa kuhakikisha ulinzi na usalama unakuwepo katika mikutano ya kampeni.

(2) Ratiba ya mikutano ya kampeni za uchaguzi itakayowasilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya chini ya Kanuni ya 27(3) itakuwa ni taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni na mgombea au Chama chake hakitowajibika kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi.

(3) Mikutano ya kampeni za uchaguzi kwa mujibu wa ratiba iliyopitishwa itaanza saa mbili asubuhi na itamalizika saa kumi na mbili kamili jioni ya kila siku ya kampeni.

Mabadiliko ya ratiba

**29.** (1) Endapo Mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kitakusudia kufanya mabadiliko ya ratiba ya mikutano ya kampeni, mgombea au chama hicho kitafanya hivyo baada ya kuwasilisha kwa maandishi mapendekezo ya mabadiliko hayo kwa Msimamizi wa Uchaguzi na mapendekezo hayo kuridhiwa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (2).

(2) Msimamizi wa Uchaguzi ataitisha kikao na Vyama vya Siasa vinavyoshiriki uchaguzi ili kujadili maombi ya mabadiliko ya ratiba na na mabadiliko yatakayokubaliwa yatawasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya kwa ajili ya kupatiwa ulinzi siku ya mkutano wa kampeni.

Masharti ya kampeni

**30.** (1) Mgombea, mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kitatakiwa kuendesha mikutano ya kampeni za uchaguzi kwa mujibu wa ratiba na kwa kuzingatia muda uliowekwa chini ya Kanuni hizi.

(2) Mgombea au mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea hakitaruhusiwa kuendesha kampeni za uchaguzi kwa:

(a) kutumia rushwa;

(b) kutoa maneno ya kashfa au lugha za matusi;

(c) kufanya ubaguzi wa jinsia, maumbile, ulemavu, dini, rangi, kabila au ubaguzi mwingine wa aina yoyote; au

(d) kutoa maneno ambayo yanaweza kusababisha uvunjifu wa amani au kusababisha vurugu.

## SEHEMU YA SABA
## TARATIBU ZA UPIGAJI KURA

Mahali, vituo na muda wa kupiga kura

**31.** (1) Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa utafanyika katika Mtaa husika.

(2) Vituo vya kupigia kura vitakuwa katika majengo ya umma yaliyopo katika Mtaa husika na endapo Mtaa hauna majengo ya umma, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kushauriana na wagombea au vyama vya siasa vyenye wagombea, atateua eneo lingine kuwa kituo cha kupigia kura.

(3) Kura zitapigwa kuanzia saa mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi kamili jioni.

(4) Baada ya saa kumi kamili, askari atakaa nyuma ya mpiga kura wa mwisho ili kuzuia watu waliochelewa kupiga kura.

Masanduku ya kura

**32.** (1) Kutakuwa na sanduku maalum la kupigia kura lililotengenezwa kwa namna itakayomwezesha mpiga kura kutumbukiza kura yake kwa urahisi kwa kila ngazi itakayopigiwa kura bila ya kuruhusu kura hiyo kutolewa ndani ya sanduku hilo.

(2) Kabla ya kuanza kupiga kura, Msimamizi wa Kituo atawaonesha wapiga kura sanduku la kupigia kura lililo wazi na atalifunga kwa lakiri kwa namna ambayo itazuia kufunguliwa bila kukata lakiri.

Karatasi za kupigia kura

**33.** Kutakuwa na karatasi za kupigia kura kwa nafasi ya uenyekiti wa Mtaa, ujumbe wa Kamati ya Mtaa na ujumbe wa Kamati ya Mtaa kupitia kundi la wanawake ambazo zitakuwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Utambulisho wa mpiga kura

**34.** (1) Msimamizi wa Kituo atatakiwa, kabla ya kumpatia mpiga kura karatasi za kupigia kura, kujiridhisha kama jina la mpiga kura huyo limeorodheshwa katika Orodha ya Wapiga Kura.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni Ndogo ya (1), Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura aoneshe kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye Orodha ya Wapiga Kura.

(3) Aina ya kitambulisho ambacho Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura kuonesha ni pamoja na:

(a) kitambulisho cha mpiga kura;
(b) kitambulisho cha kazi;
(c) hati ya kusafiria;
(d) kadi ya bima ya afya;
(e) kitambulisho cha shule au chuo;
(f) kitambulisho cha mifuko ya hifadhi ya jamii;
(g) leseni ya udereva; au
(h) kitambulisho cha taifa.

(4) Endapo mpiga kura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote kati ya vilivyotajwa chini ya Kanuni Ndogo ya (3) lakini jina lake limo kwenye orodha ya

wapiga kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi wa Kituo atamruhusu mtu huyo kupiga kura baada ya kutambuliwa na wakazi wa eneo husika.

Upigaji kura

**35.** (1) Kura zitapigwa katika namna itakayozingatia usiri.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 34, Msimamizi wa Kituo atampatia mpiga kura karatasi tatu za kupigia kura kwa nafasi zifuatazo:-

(a) mwenyekiti wa Mtaa;

(b) wajumbe wa Kamati ya Mtaa; na

(c) wajumbe wa Kamati ya Mtaa kupitia kundi la wanawake.

(3) Mpiga kura, baada ya kupewa karatasi za kupigia kura, atapiga kura kwa utaratibu ufuatao:

(a) kura moja kwa nafasi ya uenyekiti wa Mtaa;

(c) kura kwa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Mtaa kwa idadi itakayoelekezwa na Msimamizi wa kituo; na

(d) kura kwa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Mtaa kupitia kundi la wanawake.

(4) Baada ya kupiga kura, mpiga kura atatakiwa kuchovya kidole cha mkono katika kidau cha wino.

(5) Wakati wa kupiga kura watu wafuatao wataruhusiwa kushuhudia kura zinavyopigwa:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi ambaye atatambuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(c) askari au afisa wa polisi, mgambo mwenye sare au afisa yeyote anayesimamia ulinzi ambaye atatambuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi; na

(d) wakala wa Chama cha Siasa chenye mgombea;

(e) mwangalizi wa Uchaguzi mwenye kitambulisho.

(6) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, mtu yeyote hatoruhusiwa kubaki katika eneo la Kituo cha Kupigia Kura baada ya kupiga kura.

Usaidizi kwa wenye mahitaji maalum

**36.** (1) Mpiga kura ambaye:

(a) kwa sababu ya ulemavu wa macho au ulemavu mwingine wowote; au

(b) hajui kusoma na kuandika,

anaweza kumwomba mtu yeyote kumsaidia kupiga kura; isipokuwa mpiga kura huyo hataruhusiwa kumchagua Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, mgombea au wakala wake.

(2) Bila kuathiri masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), mtu mmoja hataruhusiwa kumsaidia mpiga kura zaidi ya mmoja.

Kuahirisha upigaji kura

37. Endapo siku ya kupiga kura kutatokea jambo lolote litakalozuia upigaji kura kuendelea kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada ya kuwasiliana na Msimamizi wa Uchaguzi ataahirisha upigaji kura hadi siku inayofuata au siku nyingine anayoona inafaa ambayo haitazidi siku saba tangu siku ya Uchaguzi ulipoahirishwa.

## SEHEMU YA NANE
## KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

Kuhesabu kura

38. (1) Kura zitahesabiwa na Msimamizi wa Kituo kwenye kituo cha kupigia kura mbele ya wagombea au mawakala wao.

(2) Msimamizi wa Kituo, kabla ya kuanza kuhesabu kura, atafanya yafuatayo mbele ya wagombea au mawakala wao:

(a) atahakiki idadi ya wakazi waliopiga kura;

(b) atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka katika bahasha maalum;

(c) atakagua lakiri na kuona kama haijafunguliwa;

(d) atakata lakiri; na

(e) atafungua sanduku la kupigia kura.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), wakati wa kuhesabu kura watu wafuatao wataruhusiwa kushuhudia kura zinavyohesabiwa:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;

(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(c) askari au Afisa wa Polisi, Mgambo wenye sare au Afisa yeyote anayesimamia ulinzi; na

(d) mwangalizi wa Uchaguzi mwenye kitambulisho.

Matokeo ya Wajumbe wa Kamati ya Mtaa

39. (1) Matokeo ya uchaguzi wa Wajumbe wa Kamati ya Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa kupitia kundi la wanawake yatajazwa kwenye fomu ya matokeo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi ambayo itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi wa Kituo na nakala kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo ya uchaguzi na nakala halisi kuwasilishwa ofisi ya Serikali ya Mtaa kwa ajili ya kujumlishwa na kutangaza mshindi au washindi wa kila nafasi iliyogombewa.

(2) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Wajumbe wa Kamati ya Mtaa wa kundi la wagombea mchanganyiko yaani wanawake na wanaume utakuwa kama ifuatavyo:

(a) endapo idadi ya wagombea ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa wajumbe wa Kamati ya Mtaa;

(b) endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea ambao wamepata kura nyingi kuwa washindi wa nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Mtaa; au

(c) endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea lakini anahitajika mgombea mmoja kati yao ili kupata idadi ya jumla ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo hayo na kupanga tarehe nyingine ya Uchaguzi katika muda usiozidi siku kumi na nne tangu siku ya Uchaguzi.

(3) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya wajumbe wa Kamati ya Mtaa kwa kundi la wagombea wa kundi la wanawake utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) endapo idadi ya wajumbe ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa wajumbe wa Kamati ya Mtaa;

(b) endapo idadi ya kura italingana kwa wagombea au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea ambao wamepata kura nyingi kuwa ni washindi wa nafasi ya ujumbe wa

Kamati ya Mtaa; au

(c) endapo idadi ya kura italingana kwa wagombea lakini anahitajika mgombea mmoja kati yao ili kupata idadi ya jumla ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo hayo na kupanga tarehe nyingine ya Uchaguzi katika muda usiozidi siku kumi na nne tangu siku ya Uchaguzi.

Matokeo ya Mwenyekiti wa Mtaa

**40.** (1) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kupokea fomu za matokeo ya kura za nafasi ya uenyekiti wa Mtaa kutoka kwa wasimamizi wa vituo vya kupigia kura, atajumlisha idadi ya kura kwa kila mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Mtaa na kujaza matokeo katika fomu ya matokeo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi na fomu hiyo itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(2) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Mtaa na kubandika matokeo hayo kwenye sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

(3) Endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo na kupanga tarehe nyingine ya Uchaguzi wa marudio utakaofanyika ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uchaguzi.

Taratibu za kurudia uchaguzi

**41.** (1) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, Uchaguzi wa marudio unaotokana na kulingana kwa idadi ya kura utahusisha wagombea ambao idadi ya kura zao zimelingana na itachukuliwa kuwa wagombea hao wameshateuliwa kuwa wagombea kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Wagombea wanaoshiriki katika Uchaguzi wa marudio au Vyama vyao vya Siasa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) havitaruhusiwa kufanya kampeni za Uchaguzi wa marudio.

Masuala yasiyobatilisha matokeo

**42.** Masuala yafuatayo hayatobatilisha matokeo ya Uchaguzi au utekelezaji wa shughuli yoyote ya Uchaguzi:

(a) kutokuwepo kwa mgombea au wakala wa mgombea wakati wa kupiga kura, kuhesabu kura au kutangaza matokeo; au

(b) mgombea au wakala wa mgombea kukataa kusaini fomu ya matokeo.

Malalamiko kuhusu uendeshaji wa Uchaguzi

**43.** Mgombea yeyote ambaye hakuridhika na matokeo ya Uchaguzi au uendeshaji wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya siku thelathini tangu siku ya kutangaza matokeo ya uchaguzi.

SEHEMU YA TISA
NAFASI WAZI NA UCHAGUZI MDOGO

Nafasi wazi

**44.** (1) Nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa itakuwa wazi endapo yatatokea mambo yafuatayo:

(a) kifo cha Mwenyekiti au Mjumbe;
(b) Mwenyekiti au Mjumbe kujiuzulu wadhifa wake;
(c) Mwenyekiti au Mjumbe kukosa sifa za kuwa mgombea;
(d) kubatilishwa kwa matokeo ya Uchaguzi;
(e) Mwenyekiti au Mjumbe kukoma kuwa mwanachama wa Chama cha Siasa kilichomdhamini;
(f) Mwenyekiti au Mjumbe kuhama Mtaa;
(g) Mwenyekiti kutoitisha mikutano mitatu ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu za msingi;
(h) Mwenyekiti au Mjumbe kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya kawaida bila kuwa na sababu ya msingi;
(i) kugawanywa kwa Mtaa;
(j) kufutwa kwa Mtaa;
(l) Mwenyekiti au Mjumbe kuvuliwa madaraka kwa mujibu wa Sheria.

(2) Endapo litatokea jambo lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) ya Kanuni hii, Mtendaji wa Mtaa atatoa taarifa kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika kipindi kisichozidi siku saba tangu kutokea kwa jambo hilo.

Uchaguzi Mdogo

**45.** (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza kuwepo kwa nafasi wazi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Mtendaji wa Mtaa juu ya kuwepo kwa nafasi iliyoachwa wazi.

(2) Nafasi wazi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa itajazwa kwa kufanya Uchaguzi Mdogo kwa utaratibu uliopo katika Kanuni hizi.

(3) Nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa itajazwa katika muda wa siku sitini baada ya kutangazwa kuwa wazi.

(4) Uchaguzi Mdogo hautafanyika kwa nafasi yoyote ile chini ya Kanuni hizi endapo muda uliosalia kabla ya uchaguzi wa kawaida ni miezi sita au pungufu yake.

## SEHEMU YA KUMI
## UTARATIBU WA KUAPISHWA

Kiapo

**46.** (1) Wafuatao watatakiwa kuapa kiapo cha uaminifu na kutunza siri mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao chini ya Kanuni hizi:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;
(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(c) Msimamizi wa kituo;
(d) Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Rufaa;
(e) mawakala wa Vyama vya Siasa; na
(f) Mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa kusimamia shughuli za uchaguzi chini ya Kanuni hizi.

(2) Endapo Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya hawezi kupatikana, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza kuwaapisha watu waliotajwa katika aya za (c), (d), (e) na (f) za Kanuni Ndogo ya (1).

(3) Wenyeviti wa Mitaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao, wataapa kiapo cha utii na uadilifu mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya katika tarehe na sehemu itakayopangwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(4) Viapo vilivyotajwa katika Kanuni hii vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Tano la Kanuni hizi na watakaoapishwa watapewa nakala za viapo.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa ya Uchaguzi

**47.** (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa la Uchaguzi endapo:

(a) ataharibu orodha ya wapiga kura au nyaraka zozote zinazohusiana na Uchaguzi;

(b) atatoa taarifa za uongo ili aweze kupiga kura au kugombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa;

(c) atajiandikisha au kupiga kura zaidi ya mara moja kwa wagombea wa nafasi moja;

(d) atatishia wapiga kura au wagombea ili kuvuruga Uchaguzi;

(e) atafanya kampeni siku ya Uchaguzi;

(f) ataonyesha ishara au kuvaa mavazi yanayoashiria kumtambulisha mgombea au Chama cha Siasa katika eneo la mita mia mbili kutoka kwenye kituo cha kupigia kura;

(g) atamzuia Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Mjumbe wa Kamati ya Rufaa au mtumishi wa umma aliyeteuliwa kusimamia uchaguzi kutekeleza majukumu yake;

(h) atakiuka masharti ya kiapo chake chini ya Kanuni ya 46(1);

(i) atapatikana na karatasi za kupigia kura zaidi ya moja kwa nafasi moja inayogombewa;

(j) atavuruga ratiba ya mikutano ya kampeni ya Uchaguzi au atavunja masharti ya kampeni za Uchaguzi;

(k) atafanya jambo lolote kinyume cha Kanuni hizi;

(l) atakutwa na silaha kinyume cha Sheria kwenye eneo la uteuzi wa wagombea, mikutano ya kampeni, eneo la usikilizaji wa rufaa za wagombea, kituo cha kuandikisha wapiga kura au kituo cha kupigia na kuhesabu kura; au

(m) Mtu yeyote ambaye atatangaza matokeo ya Uchaguzi kabla hayajatangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kosa lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kinga

**48.** Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Wajumbe wa Kamati ya Rufaa au mtumishi yeyote wa umma aliyehusika na usimamizi wa Uchaguzi hatowajibika kwa jinai au madai

au kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kiutawala kwa jambo lolote alilolifanya au kuacha kufanya kwa nia njema wakati wa kutekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
MASUALA MENGINE

Waangalizi wa ndani wa uchaguzi

49. (1) Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi wataruhusiwa kuangalia uchaguzi baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

(2) Maombi ya kibali cha uangalizi wa Uchaguzi yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa ndani ya muda wa siku ishirini na moja baada ya Tangazo la Uchaguzi kutolewa.

(3) Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi watafanya shughuli za uangalizi kwa gharama zao wenyewe na watatakiwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi na miongozo itakayotolewa ikiwa ni pamoja na kutoingilia kwa namna yoyote shughuli ya Uchaguzi.

Taratibu za Maadili

50. Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi, kutakuwa na Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zilizoainishwa katika Jedwali la Sita la Kanuni hizi ambazo zitatakiwa kufuatwa na wadau wa Uchaguzi walioainishwa katika Taratibu hizo.

Miongozo

51. Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi, Waziri anaweza kutoa miongozo mbalimbali kuhusu Uchaguzi.

Elimu ya Mpiga Kura

52. (1) Taasisi yoyote inayotaka kutoa elimu ya mpiga kura katika Uchaguzi itatakiwa kuwasilisha maombi ya kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya serikali za mitaa kwa kuzingatia miongozo itakayotolewa.

(2) Taasisi zitakazotoa elimu ya mpiga kura zitatoa elimu hiyo kwa gharama zao.

Kufutwa kwa Kanuni za Uchaguzi Tangazo la Serikali Na. 322 la Mwaka 2014

53. (1) Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2014 zinafutwa.

(2) Bila kujali masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), matangazo, machapisho, miongozo, taratibu au kitu chochote kinachohusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambacho kilikuwa kinatumika kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, kitaendelea kutumika hadi pale kitakapofutwa na matangazo, machapisho, miongozo, taratibu au kitu chochote kitakachotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi isipokuwa tu kama machapisho, miongozo, taratibu au kitu hicho kinakinzana na Kanuni hizi.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 11(1))*

**FOMU Na. 1**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**ORODHA YA WAPIGA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2019**

**HALMASHAURI ..................................**
**KATA..............................................**
**MTAA.............................................**

| Na. | Jina la Mpiga Kura *(Majina matatu)* | Jinsi (Me/Ke) | Umri | Tarehe ya kuandikishwa | Saini/Dole gumba la aliyeandikishwa | Saini ya Mwandikishaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |
| 5. | | | | | | |
| 6.. | | | | | | |
| 7. | | | | | | |
| 8. | | | | | | |
| 9. | | | | | | |
| 10. | | | | | | |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 17 (5)*

**FOMU Na. II**

**FOMU YA MAOMBI YA UTEUZI KUGOMBEA UENYEKITI WA MTAA MWAKA 2019**

| NEMBO YA HALMASHAURI |
|---|

**HALMASHAURI ..........................................**
**KATA...........................................................**
**MTAA.........................................................**

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**
(*Ijazwe na anayeomba kugombea*)

1. Jina la Ukoo.....................................................

2. Jina la Kati......................................................

3. Jina la Mwanzo.................................................

4. Jinsi (Me/Ke)....................................................

5. Uraia ..............................................................

6. Tarehe ya kuzaliwa...........................................

7. Mahali unapoishi (a) Mtaa...........................

(b) Kata.................................

8. Namba ya Simu (kama ipo) ................................

9. Kazi/shughuli yako ..........................................

10. Uwezo wa Kusoma na Kuandika

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (a) | Kusoma Kiswahili | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |
| (b) | Kuandika Kiswahili | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |
| (c) | Kusoma Kiingereza | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |
| (d) | Kuandika Kiingereza | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |

11. Jina la Chama cha Siasa kinachomdhamini…………………………………..

12. Namba ya Kadi ya Uanachama……………………………………………….
    tarehe ilipotolewa…………………mahali ilipotolewa…………………

13. Nafasi anayoomba kugombea………………………………………………..

Nathibitisha kwamba taarifa zote zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo.

Saini ya Mgombea ………………………Tarehe ………………………………

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**
(*Ijazwe na Chama cha Siasa*)

**Hii** ni kuthibitisha kuwa ………………………………..(*Taja jina la Mgombea*) ni Mwanachama na amedhaminiwa na ……………………………………….(*Taja jina la Chama*)

1. Jina: ………………………………………..
2. Saini:…… ………………………………
3. Wadhifa: ………………………………..
4. Tarehe: …………………………………..
5. Anwani:…………………………………
6. Muhuri wa Chama cha Siasa:……………

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu……………………………………………
2. Muda ……………………………………………………………..
3. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………
4. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………..
5. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ……………………..

**SEHEMU D: UTEUZI**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa……………………………………kugombea nafasi

   ya ……………………………………………

2. Sababu……………………………………………………………………

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………………………

4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi …………………………

5. Tarehe……………………………………………………………………

6. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ………………………

**FOMU Na. III**

**FOMU YA UCHAGUZI**

**FOMU YA MAOMBI YA UTEUZI KUGOMBEA UJUMBE WA KAMATI YA MTAA KUNDI MCHANGANYIKO NA KUNDI LA WANAWAKE MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

**HALMASHAURI ..........................................**
**KATA.......................................................**
**MTAA......................................................**

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**
(*Ijazwe na anayeomba kugombea*)

1. Jina la Ukoo..................................................
2. Jina la Kati...................................................
3. Jina la Mwanzo..............................................
4. Jinsi (Me/Ke).................................................
5. Uraia ........................................................
6. Tarehe ya kuzaliwa.........................................
7. Mahali unapoishi (a) Mtaa..........................
   (b)Kata...............................
8. Namba ya Simu (kama ipo) ............................
9. Kazi/shughuli yako ........................................
10. Uwezo wa Kusoma na Kuandika

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) | Kusoma Kiswahili | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |
| (b) | Kuandika Kiswahili | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |
| (c) | Kusoma Kiingereza | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |
| (d) | Kuandika Kiingereza | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |

11. Jina la Chama cha Siasa kinachomdhamini.....................................
12. Namba ya Kadi ya Uanachama...................................................
    tarehe ilipotolewa........................mahali ilipotolewa.....................

13. Nafasi anayoomba kugombea……………………………………………..

Nathibitisha kwamba taarifa zote zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo.

Saini ya Mgombea ………………………Tarehe ……………………………

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

*(Ijazwe na Chama cha Siasa)*

Hii ni kuthibitisha kuwa ………………………………(*Taja jina la Mgombea)* ni Mwanachama na amedhaminiwa na ……………………………………………(*Taja jina la Chama*)

1. Jina: ………………………………………..
2. Saini:…… ………………………………..
3. Wadhifa: ……………………………….
4. Tarehe: ……………………………………..
5. Anwani:…………………………………
6. Muhuri wa Chama cha Siasa:……………

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

*(Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi)*

1. Tarehe ya kupokea fomu……………………………………………..
2. Muda ………………………………………………………………..
3. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………
4. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………..
5. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ……………………

**SEHEMU D: UTEUZI**

*(Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi)*

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa…………………………………kugombea nafasi

   ya ……………………………
2. Sababu…………………………………………………………………
3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………..

4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ...........................

5. Tarehe.......................................................................

6. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi .........................

**FOMU Na. IV**

**TAMKO LA MGOMBEA LA KUHESHIMU NA KUTEKELEZA TARATIBU ZA MAADILI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2019**

***(Fomu hii ijazwe na kurudishwa pamoja na Fomu ya Uteuzi )***

Mimi…………………………………………………ambaye ninatarajia kuwa mgombea wa nafasi ya………………………………………………………………………………niliyependekezwa na Chama cha………………………………………………………………… kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 ninatamka kuwa nitaheshimu na kutekeleza Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 wakati wote wa uchaguzi.

Ninatoa Tamko hili nikiamini kuwa yote niliyoeleza hapo juu ni kweli kwa kadri ya ufahamu wangu.

Saini ya Mgombea……………………………………
Anwani…………………………………………………
Namba ya Simu………………………………………

Tamko hili limetolewa mbele yangu saa……………………… Tarehe………… Mwezi…………
Mwaka 20………………..

Saini……………………………………………………
Jina…………………………………………………………
Wadhifa **MSIMAMIZI WA UCHAGUZI/MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI***
*futa isiyohitajika.

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 33)*

**FOMU Na. V**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA NAFASI YA MWENYEKITI WA MTAA**

**MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

**FOMU Na. VI**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA NAFASI YA MJUMBE WA KAMATI YA MTAA KUNDI MCHANGANYIKO MWAKA 2019**

| NEMBO YA HALMASHAURI |
|---|

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

**FOMU Na. VII**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA WAGOMBEA UJUMBE WA KAMATI YA MTAA KUNDI LA WANAWAKE MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenzwa chini ya Kanuni ya 39 na 40)*

**FOMU Na. VII**

**FOMU YA MATOKEO YA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA MTAA**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | CHAMA CHA SIASA | KURA ALIZOPATA | JINSI (KE/ME) | SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| 5. | | | | | |
| 6. | | | | | |
| 7. | | | | | |
| 8. | | | | | |
| 9. | | | | | |
| 10. | | | | | |

| | |
|---|---|
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | |
| Idadi ya waliopiga kura | |
| Idadi ya kura halali | |
| Idadi ya kura zilizoharibika | |
| Jina la Msimamizi wa Kituo | |

Saini.......................................................................................tarehe.......................
Muhuri wa Msimamizi wa Kituo

**FOMU Na. VIII**

**FOMU YA MATOKEO YA UCHAGUZI WA WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI MCHANGANYIKO/KUNDI LA WANAWAKE**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | CHAMA CHA SIASA | KURA ALIZOPATA | JINSI (KE/ME) | SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |

| | |
|---|---|
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | |
| Idadi ya waliopiga kura | |
| Idadi ya kura halali | |
| Idadi ya kura zilizoharibika/kukataliwa | |
| JUMLA | |
| Jina la Msimamizi wa Kituo | |

Saini…………………………………….tarehe…………………

Muhuri wa Msimamizi wa Kituo……………………………..

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 46(4))*

VIAPO

*(a) Kiapo cha Uaminifu*

"Mimi ……………………………. naapa/natamka kwa dhati kwamba nitaitumikia vyema na kwa moyo thabiti Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi yangu kama ………………………………katika Halmashauri ya …………………… na katika kutimiza wajibu wa nafasi hiyo nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kwa vyovyote vile sitatoa siri zinazohusu majukumu yangu isipokuwa kwa mujibu wa sheria. Ewe Mwenyezi Mungu, nisaidie."

Kiapo/Tamko hili limetolewa hapa: ……………………………………………………

na………………………………………………………………………………………………

Leo tarehe…………………… Mwezi wa…………………..Mwaka 20…………...

Mbele ya:

**Jina:**……………………………………………

**Saini:**……………………………………………

**Wadhifa:**…………………………………………

**Anuani**……………………………………………

*(b) Kiapo cha Utii na Uadilifu*

Mimi ……………………………………………………… naapa/natamka kwa dhati kwamba nitaitumikia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wadhifa wangu wa ……………………………………………. kwa uaminifu, kwa uwezo na moyo wangu wote na kwamba nitahifadhi, nitalinda na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria za Tanzania na Maadili ya Viongozi wa Umma kama yalivyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie"

Kiapo/Tamko hili limetolewa hapa: ………………………………………

na…………………………………………………………………………

Leo Tarehe…………………… Mwezi ……………………Mwaka 20……….

Mbele ya:…………………………………………

**Jina:……………………………………………**

**Cheo:…………………………………………**

**Saini:…………………………………………**

**Anuani………………………………………**

JEDWALI LA SITA

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 50)*

**TARATIBU ZA MAADILI**

**1.0 Jina, Matumizi, Wahusika wa Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019**

**1.1 Jina na Tarehe ya kuanza kutumika**

Taratibu hizi zitajulikana kama Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019.

**1.2 Wahusika wa Taratibu za Maadili**

Wahusika wa taratibu za Maadili hizi watakuwa wafuatao:-

(a) Vyama vya Siasa;

(b) Wagombea;

(c) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(d) Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi.

**2.0 Taratibu za Maadili**

**2.1 Wajibu wa Vyama vya Siasa na Wagombea**

Kila Chama cha Siasa na Wagombea watatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

(a) kuheshimu na kutekeleza Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi itakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni pamoja na kuzingatia matakwa ya Sheria nyingine za nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi;

(b) kuelimisha, kuhamasisha na kuwasisitiza wanachama na wafuasi wao kuheshimu Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi itakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni pamoja na Sheria nyingine za nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi;

(c) kuzingatia ratiba ya mikutano ya kampeni;

(d) kwa kushirikiana na wanachama na wafuasi wa Vyama vingine vya Siasa kuhakikisha kuwa wanachukua hatua za makusudi ili:-

(i) kufanya Uchaguzi uwe huru na wa haki;

(ii) kuzuia vitendo vya vurugu na vitisho;

(iii) kukataa aina yoyote ya ubaguzi katika misingi ya jinsia, maumbile, ulemavu, ukabila, dini au rangi; na

(iv) kueneza taarifa sahihi kuhusu mchakato wa Uchaguzi;

(e) kuchapisha vijitabu, vipeperushi, vitini, mabango na machapisho ya aina yoyote yanayoeleza sera zao baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa Uchaguzi;

(f) kutumia vyombo vya habari kutangaza sera zao kwa kuzingatia sheria zinazosimamia vyombo vya habari na Miongozo ya Uchaguzi;

(g) kujenga mazingira ambayo yatawezesha Uchaguzi kufanyika kwa uhuru na haki, ikiwa ni pamoja na kuwezesha makundi maalum kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi;

(h) kuhakikisha hifadhi na usafi wa mazingira katika kusambaza matangazo ya kampeni;

(i) kuondoa mabango, matangazo na machapisho ya aina yoyote ile yaliyotumika wakati wa kampeni katika sehemu za wazi baada ya Uchaguzi;

(j) kutoa taarifa mara moja kwa mamlaka husika wanapofahamu au wanapoona tukio linaloweza kusababisha vurugu au uvunjifu wa amani;

(k) kuhakikisha kuwa wanafanya kampeni kwa kuzingatia misingi inayolenga kutangaza sera za Vyama vyao pasipo kujenga chuki, kusababisha mifarakano na migawanyiko katika jamii;

(l) kuchukua hatua za lazima kuhakikisha kuwa hakuna migongano ya mikutano ya kampeni na Vyama vingine;

(m) kukataza wanachama au wafuasi kutamka kauli mbiu, kuonesha ishara za Vyama vyao, au kuvaa sare zenye rangi ya Chama chao katika mikutano ya hadhara ya Vyama vingine; na

(n) kuwaelekeza Mawakala wao watakaokuwepo katika Vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi.

**2.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Vyama vya Siasa na Wagombea**

Kila Chama cha Siasa au Mgombea hatatakiwa kufanya yafuatayo:-

(a) kusababisha au kufanya fujo au vurugu ya aina yoyote katika Mkutano wake au wa Chama kingine;

(b) kutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji na vitisho au lugha inayochochea uvunjifu wa amani au kuashiria ubaguzi wa kijinsia, dini, rangi, ulemavu au maumbile kwenye mikutano ya kampeni;

(c) kubeba sanamu, kinyago au kitu chochote ambacho kinaonyesha kudhalilisha, kukebehi, kufedhehesha au kukejeli Chama kingine cha Siasa au Mgombea au Kiongozi wa Chama kingine cha Siasa au Serikali katika mkutano wowote wa kampeni za Uchaguzi;

(d) kutumia vipaza sauti vya aina yoyote kwa shughuli za kisiasa mara baada ya muda wa kampeni za Uchaguzi kumalizika;

(e) kuchafua, kubandua au kuharibu kwa namna yoyote ile matangazo ya kampeni ya Vyama vingine vya Siasa na matangazo mengine yanayotolewa na Mamlaka za Uchaguzi;

(f) kubandika mabango ya kampeni, matangazo au michoro wowote kwenye nyumba, majengo au vyombo vya usafiri vya watu binafsi au taasisi mbalimbali bila idhini ya wamiliki husika;
(g) kubandika mabango ya kampeni, matangazo au michoro wowote kwenye nyumba za ibada, taasisi za dini na majengo ya Serikali na taasisi zake;
(h) kutoa rushwa ili kumshawishi mtu yeyote kupiga kura, kugombea au kujitoa katika kugombea nafasi ya uongozi;
(i) kuzuia mtu yeyote, watu au wafuasi wa vyama vingine kuhudhuria mikutano ya kampeni au kupiga kura;
(j) kukodi au kutumia usafiri wa aina yoyote kubeba na kusafirisha wapiga kura kwa madhumuni ya kushawishi kupigiwa kura.

**2.3 Maadili wakati wa kupiga, kuhesabu, kujumlisha kura na kutangaza matokeo ya Uchaguzi**

**2.3.1. Yanayotakiwa Kufanywa**

(a) Vyama vya Siasa na Wagombea watahakikisha kuwa Mawakala wao wanakula kiapo na kukiwasilisha kwa Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kabla ya siku ya Uchaguzi;
(b) Mawakala wa Vyama vya Siasa, Vyama vya Siasa na Wagombea watakuwa na wajibu wa kushirikiana na Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo katika vituo vya kupigia kura kwa kuzingatia Kanuni za Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi;
(c) Viongozi wa Vyama vya Siasa watakuwa na wajibu wa kuwaelimisha wanachama na wafuasi wao kuwa, watatakiwa kuondoka eneo la kupigia Kura mara tu wamalizapo kupiga kura na kama itawalazimu kubakia katika eneo hilo watatakiwa kukaa umbali wa mita mia mbili kutoka kituo cha kupigia kura.

**2.3.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa**

(a) Kampeni za uchaguzi haziruhusiwa siku ya upigaji kura. Hii ni pamoja na kuvaa vazi lolote au kuwa na kitu chochote kinachoashiria kushawishi watu kumpigia kura Mgombea fulani au utambuzi wa Mgombea fulani au matumizi ya chombo cha usafiri kinachoashiria utambuzi wa Chama au Mgombea wa Chama chochote;
(b) Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wagombea na wafuasi wao watatakiwa kujiepusha na vitendo vinavyoweza kusababisha fujo au vurugu katika vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura;
(c) Hakuna mtu atakayeruhusiwa kutumia simu ya kiganjani ndani ya kituo cha kuhesabu na kujumlishia kura isipokuwa Msimamizi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na mlinzi wa kituo cha kupigia kura ambao watatumia simu zao pale itakapobidi kwa shughuli za Uchaguzi

tu na simu hizo wakati wote ziwe zimeondolewa mlio na ziwe kwenye mtetemo;

(d) Kiongozi au Mtendaji au mwanachama au mfuasi wa Chama cha Siasa hatatakiwa:

(i) kuvamia au kukaa kwa nguvu ndani ya kituo cha kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura;

(ii) kuwahamasisha wanachama au wafuasi kupiga kura zaidi ya mara moja katika Uchaguzi mmoja;

(iii) kununua kura au kutoa rushwa au aina yoyote ya malipo ya fedha au vifaa kwa mpiga kura au Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(iv) kutumia lugha ya matusi kwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo katika kituo cha kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura.

**3.0 Wajibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Serikali itakuwa na Wajibu wa:**

(a) kutoa fursa sawa kwa wadau wote wa Uchaguzi hususan Vyama vya Siasa na Wagombea ili kuendesha shughuli zao za kisiasa wakati wa Uchaguzi kwa uhuru na kuzingatia sheria za nchi;

(b) kuhakikisha hali ya usalama, amani na utulivu wakati wote wa Uchaguzi;

(c) kuhakikisha kuwa viongozi na watendaji wake wanazingatia ipasavyo ukomo wa madaraka yao katika shughuli za Uchaguzi.

**4.0 Taratibu za Maadili kwa Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi**

**4.1 Mambo wanayotakiwa Kufanya**

Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi watakuwa na wajibu wa kupanga, kusimamia na kuendesha Uchaguzi katika misingi inayowezesha Uchaguzi kuwa huru na wa haki kwa kufanya yafuatayo:-

(a) kuzingatia Katiba ya Nchi, Kanuni za Uchaguzi na Sheria nyingine za nchi;

(b) kuvipatia Vyama vya Siasa ratiba na taarifa za Uchaguzi mapema;

(c) kutoa Elimu ya Mpiga Kura, kusimamia na kuratibu taasisi na watu wanaotoa Elimu ya Mpiga Kura;

(d) kutoa mafunzo kwa wanaohusika na Uchaguzi ili kuwawezesha kuendesha uchaguzi kwa ufanisi;

(e) kuvipatia Vyama vya Siasa Kanuni, Miongozo ya Uchaguzi na Nyaraka nyingine zinazohusiana na Uchaguzi;

(f) kukemea vitendo vyenye nia ya kuharibu Uchaguzi vinavyoweza kufanywa na Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wagombea au wafuasi wao;

(g) kuendesha na kuziwezesha Kamati za kusimamia Maadili ya Uchaguzi na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yanayotolewa na Kamati hizo;
(h) kukutana na Vyama vya Siasa pale inapobidi kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Kampeni za Uchaguzi na Uchaguzi wenyewe;
(i) kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote atakayefanyiwa uonevu au kukoseshwa haki wakati wa shughuli za Uchaguzi;
(j) kutambua majukumu ya Vyama vya Siasa, Wagombea na Mawakala wao;
(k) kuandaa na kupeleka kwa wakati vifaa kwenye vituo vya kupigia kura;
(l) kuendesha zoezi la Uchaguzi kwa uwazi, haki na uadilifu.

**4.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi**

(a) kupendelea Chama chochote cha Siasa au Mgombea yeyote;
(b) kubadili ratiba za Kampeni za Uchaguzi bila kuvishirikisha Vyama vya Siasa;
(c) kuchelewa au kupeleka vifaa pungufu katika vituo vya kupigia kura bila sababu za msingi;
(d) kuchelewa kutangaza Matokeo ya Uchaguzi bila sababu za msingi.

**5.0 Usimamizi wa Utekelezaji waTaratibu za Maadili ya Uchaguzi**

5.1 Kamati za Maadili za kusimamia Utekelezaji wa Taratibu za Maadili ya Uchaguzi Kutakuwa na Kamati za Maadili zifuatazo zitakazoundwa na Msimamizi wa Uchaguzi:-

(a) Kamati ya Maadili ya Halmashauri; na
(b) Kamati ya Maadili ya Kata.

**5.2 Muundo wa Kamati za Taratibu za Maadili ya Uchaguzi**

**5.2.1 Kamati ya Maadili ya Halmashauri**

Kamati ya Maadili ya Halmashauri itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi katika Halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
(b) Mjumbe mmoja kutoka kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi katika Halmashauri;
(c) Mjumbe mmoja atakayewakilisha Serikali ambaye atateuliwa kwa maandishi na Katibu Tawala wa Wilaya husika; na
(d) Afisa Uchaguzi ambaye atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi.

**5.2.2 Kamati ya Maadili ya Kata**

Kamati ya Maadili ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Msimamizi Msaidizi ngazi ya Kata husika ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;

(b) Mjumbe mmoja kutoka kila Chama cha Siasa kinachoshiriki katika Uchaguzi kwenye Kata;
(c) Mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali atakayeteuliwa kwa maandishi na Katibu Tawala wa Wilaya husika; na
(d) Katibu ambaye ni Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kijiji atakayeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

**5.2.3 Utoaji wa taarifa za Kamati za Maadili**

Itakuwa ni marufuku kwa mtu, mgombea, Chama cha Siasa au mjumbe wa Kamati ya Maadili ambaye sio Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili kutoa taarifa yoyote kuhusu maamuzi ya Kamati au suala lolote lililopo mbele ya Kamati.

**5.3 Uwasilishaji wa Malalamiko**

Mgombea yeyote, Wasimamizi au Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, Serikali au Chama chenye Mgombea kinachoamini kwamba Maadili ya Uchaguzi yamekiukwa kitawasilisha malalamiko kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Kata kwa maandishi.

**5.4 Muda wa kuwasilisha Malalamiko**

Malalamiko yoyote yatatakiwa kuwasilishwa ndani ya siku tatu tangu kutokea kwa tukio linalolalamikiwa.

**5.5 Kuitisha kikao cha Kamati ya Maadili ya Uchaguzi**

Mwenyekiti wa Kamati husika baada ya kupokea malalamiko na kujiridhisha kuwa Taratibu za Maadili zimekiukwa atatakiwa kuitisha kikao ndani ya siku mbili.

**5.6 Namna ya kushughulikia Malalamiko**

(a) Malalamiko yote yatajadiliwa na kuamuliwa katika kikao cha Kamati ya Maadili ya Kata husika;
(b) Kamati itashughulikia malalamiko na kutoa uamuzi wake mapema iwezekanavyo;
(c) Baada ya kupokea malalamiko, Kamati itamtaka aliyelalamikiwa kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku mbili tangu kupokea malalamiko;
(d) Katika kushughulikia malalamiko, Kamati inaweza kumwita mtu yeyote kutoa maelezo ili kusaidia Kamati kufikia maamuzi ya haki;
(e) Akidi ya Kikao cha Kamati husika itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa Kamati;
(f) Kamati ya Maadili ya Uchaguzi itaamua malalamiko yote baada ya kusikiliza au kupata maelezo ya utetezi kutoka kwa pande zote mbili ambazo ni mlalamikaji na mlalamikiwa ndani ya siku mbili isipokuwa kama upande unaolalamikiwa utashindwa kuwasilisha maelezo ya utetezi katika muda uliopangwa Kamati inaweza kufanya uamuzi;

(g) Maamuzi yatakayofikiwa na Kamati ya Maadili ya Kata yatatekelezwa na pande zinazohusika na maamuzi hayo;

(h) Ikitokea kuna umuhimu wa kufanya maamuzi kwa kupiga kura, wawakilishi wa Mlalamikaji na Mlalamikiwa hawataruhusiwa kupiga kura;

(i) Malalamiko yatakayoshughulikiwa na Kamati za Maadili ni yale tu yaliyotokea katika kipindi cha Kampeni;

(j) Malalamiko yatakayotokea siku ya Upigaji Kura yatashughulikiwa kwa kuzingatia Kanuni za Uchaguzi;

(k) Kamati itakuwa na mamlaka ya kuchunguza malalamiko yote yatakayowasilishwa kabla ya kufanya maamuzi;

(l) Kamati inaweza kuelekeza malalamiko mengine kwenye mamlaka zinazohusika kama itakavyoona inafaa kwa hatua zinazostahili.

**5.7 Rufaa Dhidi ya Maamuzi**

(a) Upande ambao hautaridhika na uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Kata, utakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Kamati ya Maadili ya Halmashauri ndani ya siku mbili tangu uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Kata ulipotolewa; na

(b) Uamuzi utakaotolewa na Kamati ya Maadili ya Halmashauri utakuwa ni wa mwisho.

**5.8 Malalamiko dhidi ya Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi**

(a) Pale ambapo malalamiko yaliyowasilishwa ni dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi, Msimamizi au Msimamizi Msaidizi, Msimamizi wa Uchaguzi hataendesha Kikao hicho, isipokuwa Katibu Tawala wa Mkoa atateua Afisa yeyote wa Umma Mwandamizi kutoka Sekretarieti ya Mkoa kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho;

(b) Iwapo Kamati itaona kuwa Msimamizi amekosea Kamati itamtaka Msimamizi wa Uchaguzi kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo.

**5.9.1 Malalamiko dhidi ya Serikali**

Kamati ya Maadili ya Kata itapokea malalamiko yatakayotolewa dhidi ya Serikali na iwapo Kamati itaona kuwa Serikali imekosea itaitaka Serikali kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo.

**5.10 Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Halmashauri na Kata katika kushughulikia Malalamiko na kutoa adhabu**

**Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Halmashauri na Kata zinaweza kuchukua hatua zifuatazo:-**

(a) kuagiza upande uliokiuka maadili kusahihisha kosa au makossa yaliyotendeka na iwapo italazimu, kuomba msamaha hadharani;


(b) kutoa onyo au karipio kwa maandishi;

(c) kutangaza jina la Chama au Mgombea aliyekiuka Maadili na kueleza kosa au makosa yake kwa njia za Taarifa kwa Umma, redio, televisheni, magazeti na njia nyingine za mawasiliano;

(d) Kamati inaweza kukisimamisha Chama au Mgombea kuendelea kufanya Kampeni za Uchaguzi kwa muda itakavyoona inafaa.

**5.11 Kushindwa Kutekeleza Maamuzi ya Kamati za Maadili**

Pale ambapo Mgombea au Chama kitashindwa kutekeleza maamuzi ya Kamati husika, Kamati ya Maadili ya Uchaguzi inaweza kukisimamisha Chama husika kufanya kampeni za Uchaguzi.



DODOMA
25/04/2019

SELEMANI S. JAFO (Mb)
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 373 la tarehe 26/04/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

SURA 287

# KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI, WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI NA MWENYEKITI WA KITONGOJI ZA MWAKA 2019

TANGAZO LA SERIKALI NA. 373 la tarehe 26/04/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

SURA 287

Zimetungwa chini ya Kifungu 201A

KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI, WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI NA MWENYEKITI WA KITONGOJI ZA MWAKA 2019

MPANGILIO WA KANUNI


| Kanuni | Jina | Uk |
|---|---|---|
| 1 | Jina | 91 |
| 2 | Eneo la matumizi na tarehe ya kuanza kutumika | 91 |
| 3 | Tafsiri | 91 |
| 4 | Tangazo la uchaguzi kwa umma | 93 |
| 5 | Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji | 93 |
| 6 | Mwenyekiti na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji | 93 |
| 7 | Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi | 93 |
| 8 | Kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo | 94 |
| 9 | Maelekezo kuhusu Uchaguzi | 94 |
| 10 | Orodha ya Wapiga Kura | 95 |
| 11 | Uandikishaji wa Wapiga Kura | 95 |
| 12 | Pingamizi kuhusu uandikishaji | 96 |
| 13 | Sifa za mpiga kura | 97 |
| 14 | Kupoteza sifa ya kupiga kura | 97 |
| 15 | Sifa za Mgombea | 97 |
| 16 | Kupoteza sifa ya kuwa Mgombea | 97 |
| 17 | Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi | 98 |
| 18 | Utaratibu wa uteuzi wa Wagombea | 99 |
| 19 | Kupita bila kupingwa | 99 |
| 20 | Kujitoa kwa Mgombea | 100 |
| 21 | Kufariki kwa Mgombea | 100 |

| | | |
|---|---|---|
| 22 | Ukomo wa kuwa madarakani | 100 |
| 23 | Pingamizi kuhusu uteuzi | 101 |
| 24 | Kamati ya Rufaa | 101 |
| 25 | Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Rufaa | 102 |
| 26 | Majukumu ya Kamati ya Rufaa | 102 |
| 27 | Kampeni za Uchaguzi | 102 |
| 28 | Wajibu wa Jeshi la Polisi | 103 |
| 29 | Mabadiliko ya ratiba | 103 |
| 30 | Masharti ya kampeni | 103 |
| 31 | Mahali, vituo na muda wa kupigia kura | 104 |
| 32 | Masanduku ya kura | 104 |
| 33 | Karatasi za kupigia kura | 104 |
| 34 | Utambulisho wa mpiga kura | 104 |
| 35 | Upigaji kura | 105 |
| 36 | Usaidizi kwa wenye mahitaji maalum | 106 |
| 37 | Kuahirisha upigaji kura | 106 |
| 38 | Kuhesabu kura | 107 |
| 39 | Matokeo ya Mwenyekiti wa Kitongoji | 107 |
| 40 | Matokeo ya Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji | 108 |
| 41 | Matokeo ya Mwenyekiti wa Kijiji | 109 |
| 42 | Taratibu za kurudia Uchaguzi | 109 |
| 43 | Masuala yasiyobatilisha matokeo | 110 |
| 44 | Malalamiko kuhusu uendeshaji wa uchaguzi | 110 |
| 45 | Nafasi wazi | 110 |
| 46 | Uchaguzi Mdogo | 111 |
| 47 | Kiapo | 111 |
| 48 | Makosa ya Uchaguzi | 112 |
| 49 | Kinga | 113 |
| 50 | Waangalizi wa Ndani wa Uchaguzi | 113 |
| 51 | Taratibu za Maadili | 113 |
| 52 | Miongozo | 113 |
| 53 | Elimu ya Mpiga Kura | 114 |
| 54 | Kufutwa kwa Kanuni za Uchaguzi Tangazo la Serikali Na.323 la Mwaka 2014. | 114 |

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za Mwaka 2019.

Eneo la matumizi na tarehe ya kuanza kutumika

2. Kanuni hizi zitatumika katika Vijiji na Vitongoji vyote vilivyomo katika maeneo ya Mamlaka za Wilaya na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi isipokuwa pale itakavyoelezwa vinginevyo:-

Sura 258

"Chama cha Siasa" maana yake ni Chama cha Siasa kilichopata usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa;

Sura 287

"Kijiji" maana yake ni Kijiji kilichomo katika eneo la Mamlaka za Wilaya na ambacho kimesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya);

"Kitongoji" maana yake ni sehemu ya eneo la utawala katika

Kijiji kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya); "Mamlaka ya Uchaguzi maana yake ni hazini mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa;"

Sura 287

"mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye anaishi kwenye eneo la Kijiji au Kitongoji na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Kijiji au Kitongoji;

"Msimamizi wa Uchaguzi" maana yake ni Mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa na Mamlaka ya Uchaguzi kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi;"

"Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi" maana yake ni Mtumishi yeyote wa umma aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi;

"Mtendaji wa Kijiji" maana yake ni mtendaji mkuu wa shughuli za Serikali katika Kijiji na ni pamoja na mtumishi

yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mtendaji wa Kijiji kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"mtumishi wa umma" maana yake ni mtu yeyote aliyeajiriwa katika utumishi wa umma;

"Orodha ya Wapiga Kura" maana yake ni orodha ya majina ya wapiga kura iliyoandaliwa chini ya Kanuni hizi;

"raia" maana yake ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia;

"sehemu ya matangazo ya uchaguzi" maana yake ni sehemu maalum iliyoteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa ajili ya kutolea matangazo, au taarifa mbalimbali za uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

Sura 357

"siku ya uteuzi" maana yake ni siku ya kutangaza majina ya wanaostahili na wasiostahili kugombea nafasi za uongozi chini ya Kanuni hizi;

"Uchaguzi" maana yake ni Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji;

"Uchaguzi Mdogo" maana yake ni uchaguzi ambao utafanyika baada ya kuwepo kwa nafasi wazi ya Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji au Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

"wakati wa uchaguzi" maana yake ni muda ambao uchaguzi wa kawaida au Uchaguzi Mdogo unafanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi na unaanzia tarehe ya tangazo la uchaguzi hadi matokeo ya uchaguzi yanapotangazwa;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

SEHEMU YA PILI
TANGAZO LA UCHAGUZI

Tangazo la uchaguzi kwa umma

4. (1) Kutakuwa na uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji ambao utafanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi baada ya Waziri kutoa Tangazo la Uchaguzi kwa umma.

(2) Tangazo la Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) litatolewa katika magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa nchi nzima na katika vyombo mbalimbali vya habari siku tisini kabla ya siku ya uchaguzi.

(3) Tangazo litakalotolewa na Waziri litaelekeza mambo yafuatayo:

(a) ratiba ya uchaguzi na shughuli zinazohusika; na

(b) masharti muhimu ya uchaguzi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi.

Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji

5. Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza katika sehemu ya matangazo ya Uchaguzi majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji vilivyomo katika eneo la Halmashauri husika kwa kuzingatia orodha ya Vijiji na Vitongoji iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali siku sabini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji.

Mwenyekiti na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji

6. (1) Halmashauri ya Kijiji itakuwa na Wajumbe ambao idadi yao haitazidi wajumbe ishirini na watano.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji watakuwa ni:

(a) Mwenyekiti wa Kijiji;

(b) Wenyeviti wa Vitongoji vilivyomo katika eneo la Kijiji; na

(c) Wajumbe watakaochaguliwa wakiwemo wanawake wasiopungua theluthi moja ya wajumbe wote wa Halmashauri ya Kijiji.

Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi

7. (1) Kutakuwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo au mtumishi wa umma atakayeteuliwa kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Mtu hatateuliwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo endapo ni:

(a) kiongozi wa chama cha siasa;

(b) Mgombea;

(c) Hakimu au Jaji;

(d) kiongozi wa dini;

(e) askari wa jeshi lolote;

(f) Katibu Tawala wa Wilaya ;

(g) Katibu Tawala wa Mkoa;

(h) Mkuu wa Wilaya; au

(i) Mkuu wa Mkoa.

Kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo

8. Kila Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Wajumbe wa Kamati ya Rufani au mtumishi wa umma atakayeteuliwa kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi atasimamia uchaguzi kwa kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo yatakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TATU
## MAELEKEZO YA UCHAGUZI

Maelekezo kuhusu uchaguzi

9. (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya Uchaguzi siku sitini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.

(2) Maelekezo ya Uchaguzi, kwa mujibu wa Kanuni hizi, yataelekeza mambo yafuatayo:

(a) tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi;

(b) muda na sehemu ya kuandikisha wapiga kura;

(c) muda na mahali pa kufanyia Uchaguzi;

(d) kuwataka wakazi wote wenye sifa za kupiga kura kushiriki uchaguzi;

(e) kuwataka wakazi wenye umri wa miaka ishirini na moja au zaidi wanaotaka kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji kuchukua fomu za kugombea zitakazopatikana kwenye ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(f) tarehe na muda wa kuchukua na kurudisha fomu za maombi ya kugombea uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(g) siku ambayo uteuzi utafanyika na sehemu ya matangazo ya uchaguzi ambapo fomu za wagombea zitabandikwa;
(h) muda wa kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi na kusikilizwa kwa pingamizi;
(i) tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(j) kipindi cha kuendesha mikutano ya kampeni za Uchaguzi; na
(k) masuala mengine yanayohusu uchaguzi.

Orodha ya Wapiga Kura

**10.** (1) Kutakuwa na Orodha ya Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni Ndogo ya (1), Msimamizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa watumishi wa umma watakaoandikisha na kuandaa Orodha ya Wapiga Kura katika Vitongoji siku hamsini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.

(3) Watendaji wa Vijiji na Kata hawatateuliwa wala hawataruhusiwa kuandikisha au kuandaa Orodha ya Wapiga Kura.

Uandikishaji wa Wapiga Kura

**11.** (1) Uandikishaji na uandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura utaanza siku ya arobaini na saba kabla ya siku ya Uchaguzi na utafanyika kwa muda wa siku saba kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi katika majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na Viongozi wa Vyama vya Siasa.

(2) Vituo vya uandikishaji wa wapiga kura vitafunguliwa saa mbili kamili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili kamili jioni.

(3) Chama cha Siasa kitaruhusiwa kuteua wakala wake kwa kila kituo cha uandikishaji wa wapiga kura wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.

(4) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika sehemu ya matangazo ya uchaguzi nakala ya Orodha ya Wapiga Kura siku moja baada ya kukamilika kwa uandikishaji wa wapiga kura na atatunza nakala halisi ya Orodha hiyo.

(5) Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya Wapiga Kura atakuwa na haki ya kukagua Orodha ya Wapiga Kura katika muda wa siku saba tangu tarehe ya Orodha hiyo kubandikwa sehemu ya matangazo ya uchaguzi ili:

(a) kuweka pingamizi kuhusu usahihi wa Orodha hiyo;
(b) kuomba Orodha irekebishwe kwa ili:-
   (i) kuongeza jina lake;
   (ii) kubadilisha taarifa zilizoko katika Orodha hiyo; au
   (iii) kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa amefariki.

Pingamizi kuhusu uandikishaji

**12.** (1) Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya Wapiga Kura anaweza kuweka pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura kabla ya kumalizika kwa muda wa kukagua Orodha ya Wapiga Kura.

(2) Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atatakiwa kutoa uamuzi kuhusu pingamizi lililowekwa ndani ya siku mbili tangu tarehe ya mwisho ya ukaguzi wa Orodha ya Wapiga Kura.

(3) Endapo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataridhika na pingamizi lililowekwa chini ya Kanuni hii, atarekebisha Orodha ya Wapiga Kura iliyotangazwa baada ya muda wa siku mbili isipokuwa kama uamuzi wake umekatiwa rufaa.

(4) Endapo mtu aliyeweka au aliyewekewa pingamizi hatoridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi lililowasilishwa kwake, mtu huyo atawasilisha rufaa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ndani ya muda wa siku mbili tangu kutolewa kwa uamuzi wa pingamizi.

(5) Msimamizi wa Uchaguzi, baada ya kupokea rufaa hiyo, ataishughulikia na kuitolea uamuzi ndani ya muda wa siku nne tangu siku ya kupokea rufaa hiyo.

(6) Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni Ndogo ya (4) utakuwa wa mwisho.

Sifa za mpiga kura

**13.** Mkazi yeyote atakuwa na haki ya kupiga kura endapo atakuwa na sifa zifuatazo:
(a) ni raia wa Tanzania;
(b) ana umri wa miaka kumi na nane au zaidi;
(c) ni mkazi wa eneo la Kitongoji;
(d) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu; na

(e) awe amejiandikisha kupiga kura katika Kitongoji husika.

Kupoteza sifa ya kupiga kura

14. Mtu hatakuwa na haki ya kupiga kura endapo:

(a) hana mojawapo ya sifa zilizoainishwa katika Kanuni ya 13; au
(b) amejiandikisha kupiga kura katika kituo zaidi ya kimoja.

Sifa za Mgombea

15. Mkazi yeyote wa Kitongoji anaweza kugombea uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji endapo:-

(a) ni raia wa Tanzania;
(b) ana umri wa miaka ishirini na moja au zaidi;
(c) ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
(d) ana shughuli halali ya kumwezesha kuishi;
(e) ni mkazi wa eneo la Kitongoji;
(f) ni mwanachama wa Chama cha Siasa na amedhaminiwa na Chama hicho;
(g) hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi; na
(h) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

Kupoteza sifa ya kuwa mgombea

16. (1) Mtu hatakuwa na sifa za kugombea nafasi ya au Uenyekiti wa Kijiji, Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au Uenyekiti wa Kitongoji endapo:

(a) amepoteza au hana sifa za mgombea zilizoainishwa katika Kanuni ya 15;
(b) amehukumiwa hukumu ya kifo na Mahakama za Tanzania au anatumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita jela;
(c) ana mkataba au maslahi kwenye kampuni ambayo ina mkataba na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo anagombea nafasi ya uongozi na hajatangaza kuwepo kwa mkataba au maslahi yake kupitia kwenye gazeti linalopatikana katika eneo husika au mbao za matangazo katika ofisi ya Kijiji;
(d) amepoteza sifa ya kupiga kura chini ya Kanuni hizi au kwa mujibu wa Sheria yeyote inayohusu makosa ya uchaguzi;
(e) hatojaza fomu ya tamko la kuheshimu taratibu za maadili; au

(f) ataajiriwa au kuteuliwa katika wadhifa wowote katika Utumishi wa Umma au kuchaguliwa katika nafasi ya udiwani, ubunge, uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umakamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni ya 16(1)(b):

(a) adhabu mbili au zaidi za kifungo zinazotakiwa kutumikiwa kwa kufuatana zitachukuliwa kuwa ni adhabu tofauti iwapo kati ya adhabu hizo hakuna inayozidi miezi sita jela lakini endapo kati ya adhabu hizo kuna inayozidi miezi sita jela itachukuliwa kuwa ni adhabu moja; au

(b) kifungo cha jela kilichosababishwa na kushindwa kulipa faini hakitohesabiwa kuwa ni adhabu ya kifungo.

SEHEMU YA NNE
UTEUZI WA WAGOMBEA

Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi

**17.** (1) Mtu yeyote anayekusudia kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji atatakiwa kuchukua fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi husika siku zisizopungua ishirini na sita kabla ya siku ya uchaguzi kwa kadri itakavyoelekezwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(2) Mtu aliyechukua fomu kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) atatakiwa kurejesha fomu husika ndani ya muda wa siku saba tangu siku ya kwanza ya uchukuaji wa fomu iliyotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(3) Fomu za uteuzi wa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji zitatolewa na kupokelewa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

(4) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hatoruhusiwa kupokea kutoka kwa mtu yeyote fomu za uteuzi zitakazowasilishwa baada ya saa kumi kamili jioni ya siku ya mwisho ya kurejesha fomu.

(5) Fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji itakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

Utaratibu wa uteuzi wa Wagombea

18. (1) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji siku kumi na tisa kabla ya tarehe ya Uchaguzi kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

(2) Baada ya uteuzi kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika majina ya wagombea wenye sifa na wasio na sifa za kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya kijiji au uenyekiti wa Kitongoji sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

(3) Endapo baada ya saa kumi kamili jioni ya siku ya mwisho ya kurejesha fomu za uteuzi kutakuwa hakuna mwombaji aliyejitokeza au kama waombaji wote waliojitokeza hawana sifa zinazostahili, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika siku iliyopangwa kwa ajili ya uteuzi atavitaarifu Vyama vya Siasa na wakazi wa Kijiji au Kitongoji kuhusu kukosekana kwa waombaji au kutokuwepo kwa waombaji wenye sifa.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni Ndogo ya (3), Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atavitaarifu Vyama vya Siasa na wakazi Kijiji au wa Kitongoji husika kuhusu kurudiwa kwa mchakato wa uchaguzi baada ya siku arobaini kuanzia tarehe ya uteuzi.

Kupita bila kupingwa

19. (1) Endapo siku ya uteuzi kutakuwa na mwombaji mmoja aliyejitokeza katika nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji na mwombaji huyo akateuliwa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mwombaji huyo kuwa ni mshindi wa nafasi aliyoomba kugombea kwa kupita bila kupingwa.

(2) Endapo idadi ya waombaji wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa kundi mchanganyiko yaani wanaume na wanawake au kwa kundi la wanawake waliojitokeza na kuteuliwa itakuwa sawa na idadi ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni ya 6 ya Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza waombaji hao kuwa ni washindi wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa kundi husika kwa kupita bila kupingwa.

(3) Endapo idadi ya waombaji wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji waliojitokeza kwa kundi

mchanganyiko yaani la wanaume na wanawake au kwa kundi la wanawake na kuteuliwa itakuwa chini ya idadi ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni ya 6 ya Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza waombaji hao kuwa ni washindi wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa kundi husika kwa kupita bila kupingwa na taratibu za kujaza nafasi zilizobaki zitaanza baada ya siku arobaini kuanzia tarehe ya uteuzi.

Kujitoa kwa mgombea

**20.** (1) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea aliyeteuliwa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au Kitongoji atajitoa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi wa mgombea huyo na wagombea waliobaki watapigiwa kura ili kupata mshindi.

(2) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea aliyeteuliwa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au Kitongoji atajitoa na kubaki mgombea mmoja wa nafasi hiyo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyebaki kuwa mshindi wa nafasi iliyoombwa kwa kupita bila kupingwa.

(3) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya kijiji atajitoa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi huo na wagombea waliobaki wataendelea na hatua ya uchaguzi ili kumpata mshindi.

Kufariki kwa mgombea

**21.** (1) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au Kitongoji atafariki, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha Uchaguzi wa nafasi hiyo na Chama cha Siasa kilichotoa mgombea aliyefariki kinaweza kuwasilisha jina la mwombaji mwingine ndani ya siku arobaini tangu kuahirishwa kwa Uchaguzi ili hatua za uteuzi wa mwombaji huyo zifanyike.

(2) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji atafariki, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha uchaguzi wa nafasi hiyo na Chama cha Siasa kilichotoa mgombea aliyefariki kinaweza kuwasilisha jina la mwombaji mwingine ndani ya siku arobaini tangu kuahirishwa kwa uchaguzi ili hatua ya uteuzi wa mwombaji huyo zifanyike.

Ukomo wa kuwa madarakani

**22.** Wenyeviti wa Vijiji, Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji watakoma kushika nafasi hizo siku saba kabla ya siku ya kuchukua fomu za kugombea uongozi chini ya Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TANO
## UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA PINGAMIZI NA RUFAA

Pingamizi kuhusu uteuzi

**23.** (1) Mtu yeyote aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au anapinga uteuzi wa mgombea yeyote, anaweza kuwasilisha pingamizi na kumwomba Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kupitia upya uamuzi uliofanyika ili amteue kuwa mgombea au atengue uteuzi anaoupinga na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kupitia pingamizi husika, anaweza kukubali au kuiikataa pingamizi hilo.

(2) Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) litawasilishwa kwa maandishi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika muda wa siku mbili tangu uamuzi au uteuzi ulipofanyika na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili kuanzia siku ya kupokea pingamizi hilo.

(3) Mwombaji au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufani iliyoanzishwa chini ya Kanuni ya 24 katika muda usiozidi siku nne kuanzia tarehe ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Kamati ya Rufaa

**24.** (1) Kutakuwa na Kamati ya Rufaa katika kila Wilaya ambayo itasikiliza mapingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea wa Uchaguzi katika Wilaya husika.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Rufaa watateuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa siku saba kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Kanuni ya 25.

(3) Kamati ya Rufaa itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Katibu Tawala wa Wilaya ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) watumishi wanne wa umma kutoka taasisi za umma zilizopo katika Wilaya husika; na

(c) mtumishi mmoja wa umma ambaye atakuwa Katibu na hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Rufaa

**25.** Mtu yeyote hatateuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Rufaa endapo:

(a) anahusika na uteuzi wa wagombea;

(b) ni Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo;

(c) ni mtumishi wa Halmashauri; au

(d) kiongozi wa Chama cha Siasa katika ngazi yoyote.

Majukumu ya Kamati ya Rufani

**26.** (1) Kamati ya Rufaa itakuwa na majukumu ya kupokea, kusikiliza na kutoa uamuzi wa rufaa iliyowasiiishwa chini ya Kanuni ya 23(3).

(2) Kamati ya Rufaa itatoa uamuzi wa rufaa ndani ya muda wa siku nne kuanzia siku ya kupokea rufaa na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(3) Mtu aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamati ya Rufaa atakuwa na haki ya kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya muda wa siku thelathini baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa.

SEHEMU YA SITA
KAMPENI ZA UCHAGUZI

Kampeni za Uchaguzi

**27.** (1) Kampeni za Uchaguzi zitafanyika siku saba kabla ya siku ya Uchaguzi.

(2) Kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi kitawasilisha ratiba yake ya mikutano ya kampeni ya Uchaguzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si chini ya siku saba kabla ya kuanza kwa kampeni.

(3) Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha ratiba za mikutano ya kampeni zilizowasilishwa na Vyama vya Siasa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (2) baada ya maridhiano na Vyama vya Siasa vinavyoshiriki Uchaguzi na atatakiwa kuwasilisha ratiba ya mikutano ya kampeni za Uchaguzi iliyounganishwa siku tatu kabla ya kampeni kuanza kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

(4) Endapo Vyama Vya Siasa vitashindwa kuridhiana wakati wa uunganishaji wa ratiba za mikutano ya kampeni, Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha ratiba za mikutano ya kampeni na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(5) Mgombea au mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kinaweza kuitisha na kuhutubia mikutano ya kampeni kwa mujibu wa ratiba ya mikutano ya kampeni iliyoandaliwa na kuwasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya na mikutano hiyo itaratibiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Wajibu wa Jeshi la Polisi

**28.** (1) Mkuu wa Polisi wa Wilaya atakuwa na wajibu wa kuhakikisha ulinzi na usalama katika mikutano ya kampeni.

(2) Ratiba ya mikutano ya kampeni za Uchaguzi itakayowasilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya chini ya Kanuni ya 27(3) itakuwa ni taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni na mgombea au Chama chake hakitowajibika kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi.

(3) Mikutano ya kampeni za uchaguzi kwa mujibu wa ratiba iliyopitishwa itaanza saa mbili asubuhi na itamalizika saa kumi na mbili kamili jioni ya kila siku ya kampeni.

Mabadiliko ya ratiba

**29.** (1) Endapo Mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kitakusudia kufanya mabadiliko ya ratiba ya mikutano ya kampeni,mgombea au chama hicho kitafanya hivyo baada ya kuwasilisha kwa maandishi mapendekezo ya mabadiliko hayo kwa Msimamizi wa Uchaguzi na mapendekezo hayo kuridhiwa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (2).

(2) Msimamizi wa Uchaguzi ataitisha kikao na Vyama vya Siasa vinavyoshiriki uchaguzi ili kujadili maombi ya mabadiliko ya ratiba na mabadiliko yatakayokubaliwa yatawasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya kwa ajili ya kupatiwa ulinzi siku ya mkutano wa kampeni.

Masharti ya kampeni

**30.** (1) Mgombea, mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kitatakiwa kuendesha mikutano ya kampeni za uchaguzi kwa mujibu wa ratiba na kwa kuzingatia muda uliowekwa chini ya Kanuni hizi.

(2) Mgombea au mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea hakitaruhusiwa kuendesha kampeni za uchaguzi kwa:

(a) kutumia rushwa;

(b) kutoa maneno ya kashfa au lugha za matusi;

(c) kufanya ubaguzi wa jinsia, maumbile,

ulemavu, dini, rangi, kabila au ubaguzi mwingine wa aina yoyote; au

(d) kutoa maneno ambayo yanaweza kusababisha uvunjifu wa amani au vurugu.

SEHEMU YA SABA
TARATIBU ZA UPIGAJI KURA

Mahali, vituo na muda wa kupigia kura

**31.** (1) Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji utafanyika katika Vitongoji vilivyomo katika Kijiji.

(2) Vituo vya kupigia kura vitakuwa katika majengo ya umma yaliyopo katika Kitongoji husika na endapo Kitongoji hakina majengo ya umma, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kushauriana na wagombea au vyama vya siasa vyenye wagombea, atateua eneo lingine kuwa kituo cha kupigia kura.

(3) Kura zitapigwa kuanzia saa mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi kamili jioni.

(4) Baada ya saa kumi kamili, askari atakaa nyuma ya mpiga kura wa mwisho ili kuzuia watu waliochelewa kupiga kura.

Masanduku ya kura

**32.** (1) Kutakuwa na sanduku maalum la kupigia kura lililotengenezwa kwa namna itakayomwezesha mpiga kura kutumbukiza kura yake kwa urahisi kwa kila ngazi itakayopigiwa kura bila ya kuruhusu kura hiyo kutolewa ndani ya sanduku hilo.

(2) Kabla ya kuanza kupiga kura, Msimamizi wa Kituo atawaonesha wapiga kura sanduku la kupigia kura lililo wazi na atalifunga kwa lakiri kwa namna ambayo itazuia kufunguliwa bila kukata lakiri.

Karatasi za kupigia kura

**33.** Kutakuwa na karatasi za kupigia kura kwa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia kundi la wanawake na uenyekiti wa Kitongoji ambazo zitakuwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Utambulisho wa mpiga kura

**34.** (1) Msimamizi wa Kituo atatakiwa, kabla ya kumpatia mpiga kura karatasi za kupigia kura, kujiridhisha kama jina la mpiga kura huyo limeorodheshwa katika Orodha ya Wapiga Kura.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni Ndogo ya (1), Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura aoneshe kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye Orodha ya Wapiga Kura.

(3) Aina ya kitambulisho ambacho Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura kuonesha ni pamoja na:

(a) kitambulisho cha mpiga kura;

(b) kitambulisho cha kazi;

(c) hati ya kusafiria;

(d) kadi ya bima ya afya;

(e) kitambulisho cha shule au chuo;

(f) kitambulisho cha mifuko ya hifadhi ya jamii;

(g) leseni ya udereva; au

(h) kitambulisho cha taifa.

(4) Endapo mpiga kura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote kati ya vilivyotajwa chini ya Kanuni Ndogo ya (3) lakini jina lake limo kwenye Orodha ya Wapiga Kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi wa Kituo atamruhusu mtu huyo kupiga kura baada ya kutambuliwa na wakazi wa eneo husika.

Upigaji kura

**35.** (1) Kura zitapigwa katika namna itakayozingatia usiri.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 34, Msimamizi wa Kituo atampatia mpiga kura karatasi nne za kupigia kura kwa nafasi zifuatazo:-

(a) mwenyekiti wa Kijiji;

(b) wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

(c) wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia kundi la wanawake; na

(d) mwenyekiti wa Kitongoji.

(3) Mpiga kura, baada ya kupewa karatasi za kupigia kura, atapiga kura kwa utaratibu ufuatao:

(a) kura moja kwa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji;

(b) kura moja kwa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji;

(c) kura kwa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa Idadi itakayoelekezwa naMsimamizi wa kituo; na

(d) kura kwa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia kundi la wanawake.

(4) Baada ya kupiga kura, mpiga kura atatakiwa kuchovya kidole cha mkono katika kidau cha wino.

(5) Wakati wa kupiga kura watu wafuatao wataruhusiwa kushuhudia kura zinavyopigwa:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;

(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(c) Askari au Afisa wa Polisi, Mgambo mwenye sare au afisa yeyote anayesimamia ulinzi ambaye atatambuliwa na Msimamizi wa uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(d) Wakala wa Chama cha Siasa chenye Mgombea; na

(e) Mwangalizi wa Uchaguzi mwenye kitambulisho.

(6) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, mtu yeyote hatoruhusiwa kubaki katika eneo la Kituo cha Kupigia Kura baada ya kupiga kura.

Usaidizi kwa wenye mahitaji maalum

**36.** (1) Mpiga kura ambaye:

(a) kwa sababu ya ulemavu wa macho au ulemavu mwingine wowote; au

(b) hajui kusoma na kuandika,

anaweza kumwomba mtu yeyote kumsaidia kupiga kura; isipokuwa mpiga kura huyo hataruhusiwa kumchagua Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, mgombea au wakala wake.

(2) Bila kuathiri masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), mtu mmoja hataruhusiwa kumsaidia mpiga kura zaidi ya mmoja.

Kuahirisha upigaji kura

**37.** Endapo siku ya kupiga kura kutatokea jambo lolote litakalozuia upigaji kura kuendelea kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada ya kuwasiliana na Msimamizi wa Uchaguzi ataahirisha upigaji kura hadi siku inayofuata au siku nyingine anayoona inafaa ambayo haitazidi siku saba tangu siku Uchaguzi ulipoahirishwa.

SEHEMU YA NANE
KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

Kuhesabu kura

**38.** (1) Kura zitahesabiwa na Msimamizi wa Kituo kwenye kituo cha kupigia kura mbele ya wagombea au mawakala wao.

(2) Msimamizi wa Kituo, kabla ya kuanza kuhesabu kura, atafanya yafuatayo mbele ya wagombea au mawakala wao:

(a) atahakiki idadi ya wakazi waliopiga kura;
(b) atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka katika bahasha maalum;
(c) atakagua lakiri na kuona kama haijafunguliwa;
(d) atakata lakiri; na
(e) atafungua sanduku la kupigia kura.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), wakati wa kuhesabu kura watu wafuatao wataruhusiwa kushuhudia kura zinavyohesabiwa:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;
(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(c) Askari au Afisa wa Polisi, Mgambo mwenye sare au afisa yeyote anayesimamia ulinzi; na
(d) Mwangalizi wa Uchaguzi mwenye kitambulisho.

(4) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hii, kura za wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji na ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji zitajumlishwa katika kituo cha kujumlishia kura kitakachokuwa katika ofisi ya Serikali ya Kijiji au mahali kwingine ambapo Msimamizi wa Uchaguzi ataelekeza.

(5) Kwa madhumuni ya Kifungu Kidogo cha (4), Mgombea au Wakala wake na watu waliotajwa katika kifungu kidogo cha (3) wanaweza kushuhudia kura zinavyojumlishwa.

Matokeo ya Mwenyekiti wa Kitongoji

**39.** (1) Msimamizi wa Kituo atamtangaza mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Kitongoji.

(2) Endapo idadi ya kura kwa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji italingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi wa Kituo atatangaza matokeo hayo na kuwasilisha taarifa ya Uchaguzi huo kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uchaguzi.

(3) Matokeo ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji yatajazwa kwenye fomu ya matokeo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi ambayo itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi wa Kituo na kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

Matokeo ya Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji

**40.** (1) Msimamizi wa Kituo atajaza matokeo ya Uchaguzi wa Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia kundi la wanawake kwenye fomu ya matokeo iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi ambayo itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi wa Kituo na nakala kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo ya uchaguzi na nakala halisi kuwasilishwa ofisi ya Serikali ya Kijiji.

(2) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kupokea nakala halisi ya fomu ya matokeo kutoka kwa Msimamizi wa Kituo, atajaza matokeo hayo katika fomu ya matokeo ya jumla iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi na kumtangaza mshindi au washindi wa kila nafasi iliyogombewa.

(3) Fomu ya matokeo ya jumla itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(4) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji wa kundi la wagombea mchanganyiko yaani wanawake na wanaume utakuwa kama ifuatavyo:

(a) endapo idadi ya wagombea ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

(b) endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea ambao wamepata kura nyingi kuwa washindi wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji; au

(c) endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea lakini anahitajika mgombea mmoja kati yao ili kupata idadi ya jumla ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo hayo na kupanga tarehe nyingine ya uchaguzi katika muda usiozidi siku kumi na nne tangu siku ya Uchaguzi.

(5) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa kundi la wagombea wa ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kundi la wanawake utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) endapo idadi ya wajumbe ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

(b) endapo idadi ya kura italingana kwa wagombea au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea ambao wamepata kura nyingi kuwa ni washindi wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji; au

(c) endapo idadi ya kura italingana kwa wagombea lakini anahitajika mgombea mmoja kati yao ili kupata idadi ya jumla ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo hayo na kupanga tarehe nyingine ya uchaguzi katika muda usiozidi siku kumi na nne tangu siku ya uchaguzi.

Matokeo ya Mwenyekiti wa Kijiji

**41.** (1) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kupokea fomu za matokeo ya kura za nafasi ya uenyekiti wa Kijiji kutoka kwa wasimamizi wa vituo vya kupigia kura, atajumlisha idadi ya kura kwa kila mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji na kujaza matokeo katika fomu ya matokeo ya jumla iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi na fomu hiyo itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(2) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Kijiji na kubandika matokeo hayo kwenye sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

(3) Endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo na kupanga tarehe nyingine ya uchaguzi wa marudio utakaofanyika ndani ya muda wa siku kumi na nne tangu tarehe ya Uchaguzi.

Taratibu za kurudia uchaguzi

**42.** (1) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, Uchaguzi wa marudio unaotokana na kulingana kwa idadi ya kura utahusisha wagombea ambao idadi ya kura zao zimelingana na itachukuliwa kuwa wagombea hao wameshateuliwa kuwa wagombea kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Wagombea wanaoshiriki katika Uchaguzi wa marudio au Vyama vyao vya Siasa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) havitaruhusiwa kufanya kampeni za Uchaguzi wa marudio.

Masuala yasiyobatilisha matokeo

43. Masuala yafuatayo hayatobatilisha matokeo ya Uchaguzi au utekelezaji wa shughuli yoyote ya Uchaguzi:

(a) kutokuwepo kwa mgombea au wakala wa mgombea wakati wa kupiga kura, kuhesabu kura au kutangaza matokeo; au
(b) mgombea au wakala wa mgombea kukataa kusaini fomu ya matokeo.

Malalamiko kuhusu uendeshaji wa uchaguzi

44. Mgombea yeyote ambaye hakuridhika na matokeo ya Uchaguzi au uendeshaji wa Uchaguzi anaweza kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya siku thelathini tangu siku ya kutangaza matokeo ya Uchaguzi.

## SEHEMU YA TISA
## NAFASI WAZI NA UCHAGUZI MDOGO

Nafasi wazi

45. (1) Nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itakuwa wazi endapo yatatokea mambo yafuatayo:

(a) kifo cha Mwenyekiti au Mjumbe;
(b) Mwenyekiti au Mjumbe kujiuzulu wadhifa wake;
(c) Mwenyekiti au Mjumbe kukosa sifa za kuwa mgombea;
(d) kubatilishwa kwa matokeo ya Uchaguzi;
(e) Mwenyekiti au Mjumbe kukoma kuwa mwanachama wa Chama cha Siasa kilichomdhamini;
(f) Mwenyekiti au Mjumbe kuhama Kijiji au Kitongoji kwa kadri itakavyokuwa;
(g) Mwenyekiti kutoitisha mikutano mitatu ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu za msingi;
(h) Mwenyekiti au Mjumbe kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya kawaida bila kuwa na sababu ya msingi;
(i) kugawanywa kwa Kijiji au Kitongoji; au
(j) Mwenyekiti au Mjumbe kuvuliwa madaraka kwa mujibu wa Sheria.

(2) Endapo litatokea jambo lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1), Mtendaji wa Kijiji atatoa taarifa kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika kipindi kisichozidi siku saba tangu kutokea kwa jambo hilo.

Uchaguzi Mdogo

**46.** (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza kuwepo kwa nafasi wazi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji juu ya kuwepo kwa nafasi wazi.

(2) Nafasi wazi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itajazwa kwa kufanya Uchaguzi Mdogo kwa utaratibu uliopo katika Kanuni hizi.

(3) Nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itajazwa katika muda wa siku sitini baada ya kutangazwa kuwa wazi.

(4) Uchaguzi Mdogo hautafanyika kwa nafasi yoyote ile chini ya Kanuni hizi endapo muda uliosalia kabla ya Uchaguzi wa kawaida ni miezi sita au pungufu yake.

## SEHEMU YA KUMI
## UTARATIBU WA KUAPISHWA

Kiapo

**47.** (1) Wafuatao watatakiwa kuapa kiapo cha uaminifu na kutunza siri mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao chini ya Kanuni hizi:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;
(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(c) Msimamizi wa Kituo;
(d) Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Rufaa;
(e) mawakala wa Vyama vya Siasa; na
(f) mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa kusimamia shughuli za uchaguzi chini ya Kanuni hizi.

(2) Endapo Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya hawezi kupatikana, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza kuwaapisha watu waliotajwa katika aya za (c), (d), (e) na (f) za Kanuni Ndogo ya (1).

(3) Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao, wataapa kiapo cha utii

na uadilifu mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya katika tarehe na sehemu itakayopangwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(4) Viapo vilivyotajwa katika Kanuni hii vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Tano la Kanuni hizi na watakaoapishwa watapewa nakala za viapo.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
MAKOSA NA ADHABU

Makosa ya uchaguzi

48. (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa la uchaguzi endapo:

(a) ataharibu Orodha ya Wapiga Kura au nyaraka zozote zinazohusiana na Uchaguzi;

(b) atatoa taarifa za uongo ili aweze kupiga kura au kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji;

(c) atajiandikisha au kupiga kura zaidi ya mara moja kwa wagombea wa nafasi moja;

(d) atatishia wapiga kura au wagombea ili kuvuruga Uchaguzi;

(e) atafanya kampeni siku ya Uchaguzi;

(f) ataonyesha ishara au kuvaa mavazi yanayoashiria kumtambulisha mgombea au Chama cha Siasa katika eneo la mita mia mbili kutoka kwenye kituo cha kupigia kura;

(g) atamzuia Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Mjumbe wa Kamati ya Rufaa au mtumishi wa umma aliyeteuliwa kusimamia Uchaguzi kutekeleza majukumu yake;

(h) atakiuka masharti ya kiapo chake chini ya Kanuni ya 47(1);

(i) atapatikana na karatasi za kupigia kura zaidi ya moja kwa nafasi moja inayogombewa;

(j) atavuruga ratiba ya mikutano ya kampeni ya Uchaguzi au atavunja masharti ya kampeni za Uchaguzi;

(k) atakutwa na silaha kinyume cha sheria kwenye eneo la uteuzi wa wagombea, mikutano ya kampeni, eneo la usikilizaji wa rufaa, kituo cha kuandikisha wapiga kura au kituo cha kupigia na kuhesabu kura;

(l) atafanya jambo lolote kinyume cha Kanuni hizi; au

(m) atatangaza matokeo ya Uchaguzi kabla hayajatangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kosa lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kinga

**49.** Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Wajumbe wa Kamati ya Rufaa au mtumishi yeyote wa umma aliyehusika na usimamizi wa uchaguzi hatowajibika kwa jinai au madai au kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kiutawala kwa jambo lolote alilolifanya au kuacha kufanya kwa nia njema wakati wa kutekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MASUALA MENGINE

Waangalizi wa ndani wa uchaguzi

**50.** (1) Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi wataruhusiwa kuangalia uchaguzi baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

(2) Maombi ya kibali cha uangalizi wa Uchaguzi yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa ndani ya muda wa siku ishirini na moja baada ya Tangazo la Uchaguzi kutolewa.

(3) Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi watafanya shughuli za uangalizi kwa gharama zao wenyewe na watatakiwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi na miongozo itakayotolewa ikiwa ni pamoja na kutoingilia kwa namna yoyote shughuli za Uchaguzi.

Taratibu za Maadili

**51.** Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi, kutakuwa na Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zilizoainishwa katika Jedwali la Sita la Kanuni hizi ambazo zitatakiwa kufuatwa na wadau wa uchaguzi walioainishwa katika Taratibu hizo.

Miongozo

**52.** Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi, Waziri anaweza kutoa miongozo mbalimbali kuhusu Uchaguzi.

Elimu ya Mpiga Kura

**53.** (1) Taasisi yoyote inayutaka kutoa elimu ya mpiga kura katika Uchaguzi itatakiwa kuwasilisha maombi ya kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya serikali za mitaa kwa kuzingatia miongozo itakayotolewa.

(2) Taasisi zitakazotoa elimu ya mpiga kura zitatoa elimu hiyo kwa gharama zao.

Kufutwa kwa Kanuni za Uchaguzi Tangazo la Serikali Na. 323 la Mwaka 2014

**54.** (1) Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya za Mwaka 2014 zinafutwa.

(2) Bila kujali masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), matangazo, machapisho, miongozo, taratibu au kitu chochote kinachohusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambacho kilikuwa kinatumika kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, kitaendelea kutumika hadi pale kitakapofutwa na matangazo, machapisho, miongozo, taratibu au kitu chochote kitakachotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi isipokuwa tu kama machapisho, miongozo, taratibu au kitu hicho kinakinzana na Kanuni hizi.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 11(1)*

**FOMU Na. I**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**ORODHA YA WAPIGA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2019**

**HALMASHAURI ..............................**
**KATA..............................................**
**KIJIJI............................................**
**KITONGOJI....................................**

| Na. | Jina la Mpiga Kura *(Majina matatu)* | Jinsi (Me/Ke) | Umri | Tarehe ya kuandikishwa | Saini/Dole gumba la aliyeandikishwa | Saini ya Mwandikishaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |
| 5. | | | | | | |
| 6.. | | | | | | |
| 7. | | | | | | |
| 8. | | | | | | |
| 9. | | | | | | |
| 10. | | | | | | |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 17 (5))*

**FOMU Na. II**

**FOMU YA MAOMBI YA UTEUZI KUGOMBEA UENYEKITI WA KITONGOJI/KIJIJI MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

**HALMASHAURI** ……………………………………
**KATA**……………………………………………………
**KIJIJI**……………………………………………………
**KITONGOJI** ……………………………………………

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**
(*Ijazwe na anayeomba kugombea*)

1. Jina la Ukoo……………………………………………

2. Jina la Kati……………………………………………

3. Jina la Mwanzo………………………………………

4. Jinsi (Me/Ke)…………………………………………

5. Uraia ……………………………………………………

6. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………

7. Mahali unapoishi (a) Kitongoji…………………………
(b)Kijiji………………………………
(c) Kata………………………………

8. Namba ya Simu (kama ipo) ……………………………

9. Kazi/shughuli yako ……………………………………

10.Uwezo wa Kusoma na Kuandika

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) | Kusoma Kiswahili | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |
| (b) | Kuandika Kiswahili | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |
| (c) | Kusoma Kiingereza | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |
| (d) | Kuandika Kiingereza | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |

11. Jina la Chama cha Siasa kinachomdhamini…………………………………..
12. Namba ya Kadi ya Uanachama………………………………………………
    tarehe ilipotolewa…………………mahali ilipotolewa…………………..
13. Nafasi anayoomba kugombea…………………………………………………

Nathibitisha kwamba taarifa zote zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kamu nijuavyo.

Saini ya Mgombea ………………………Tarehe ………………………………

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

(*Ijazwe na Chama cha Siasa*)

Hii ni kuthibitisha kuwa ………………………………(*Taja jina la Mgombea*) ni Mwanachama na amedhaminiwa na …………………………………………(*Taja jina la Chama*)

1. Jina: ………………………………………..
2. Saini:…… ………………………………
3. Wadhifa: …………………………………
4. Tarehe: ……………………………………
5. Anwani:……………………………………
6. Muhuri wa Chama cha Siasa:……………

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu…………………………………………………
2. Muda ………………………………………………………………………
3. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………
4. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………………………
5. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ……………………

**SEHEMU D: UTEUZI**

*(Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi)*

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa……………………………………kugombea nafasi

   ya ……………………………………………………………………

2. Sababu……………………………………………………………………

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………………………

4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi …………………………

5. Tarehe……………………………………………………………………

6. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ………………………

**FOMU Na. III**

**FOMU YA UCHAGUZI**

**FOMU YA MAOMBI YA UTEUZI KUGOMBEA UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI MCHANGANYIKO NA KUNDI LA WANAWAKE MWAKA 2019**

| **NEMBO YA HALMASHAURI** |
|---|

**HALMASHAURI ……………………………………**
**KATA…………………………………………………**
**KIJIJI………………………………………………**
**KITONGOJI ……………………………………….**

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**
(*Ijazwe na anayeomba kugombea*)

1. Jina la Ukoo………………………………………….
2. Jina la Kati…………………………………………..
3. Jina la Mwanzo………………………………………
4. Jinsi (Me/Ke)…………………………………………
5. Uraia ………………………………………………….
6. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………..
7. Mahali unapoishi (a) Kitongoji……………………….
   (b)Kijiji……………………………….
   (c) Kata……………………………….
8. Namba ya Simu (kama ipo) ………………………….
9. Kazi/shughuli yako ……………………………………

10.Uwezo wako wa Kusoma na Kuandika

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) | Kusoma Kiswahili | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |
| (b) | Kuandika Kiswahili | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |
| (c) | Kusoma Kiingereza | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |
| (d) | Kuandika Kiingereza | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |

11. Jina la Chama cha Siasa kinachomdhamini……………………………………

12. Namba ya Kadi ya Uanachama………………………………………………
tarehe ilipotolewa……………………mahali ilipotolewa……………………

13. Nafasi anayoomba kugombea…………………………………………………..

Nathibitisha kwamba taarifa zote zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo.

Saini ya Mgombea ………………………Tarehe ………………………………

## SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA

(*Ijazwe na Chama cha Siasa*)

Hii ni kuthibitisha kuwa ………………………………(*Taja jina la Mgombea)* ni Mwanachama na amedhaminiwa na …………………………………………..(*Taja jina la Chama*)

1. Jina: ………………………………………..
2. Saini:…… ………………………………..
3. Wadhifa: …………………………………..
4. Tarehe: ……………………………………..
5. Anwani:……………………………………
6. Muhuri wa Chama cha Siasa:……………

## SEHEMU C: KURUDISHA FOMU

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu…………………………………………………
2. Muda (saa)………………………………………………………………..
3. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………
4. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………..
5. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ……………………

**SEHEMU D: UTEUZI**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa.......................................kugombea nafasi ya ...................................
2. Sababu.........................................................................................
3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi...................................
4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ...............................
5. Tarehe...........................................................................................
6. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ...........................

**FOMU Na. IV**

**TAMKO LA MGOMBEA LA KUHESHIMU NA KUTEKELEZA TARATIBU ZA MAADILI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2019**

***(Fomu hii ijazwe na kurudishwa pamoja na Fomu ya Uteuzi )***

Mimi…......................................................ambaye ninatarajia kuwa mgombea wa nafasi ya ………………………………………………………………niliyependekezwa na Chama cha………………………………………………………………… kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 ninatamka kuwa nitaheshimu na kutekeleza Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 wakati wote wa uchaguzi.

Ninatoa Tamko hili nikiamini kuwa yote niliyoeleza hapo juu ni kweli kwa kadri ya ufahamu wangu.

Saini ya Mgombea………………………………
Anwani……………………………………………
Namba ya Simu……………………………………

Tamko hili limetolewa mbele yangu saa…………………. tarehe………. mwezi……….
Mwaka 20………………

Saini…………………………………………….
Jina……………………………………………….
Wadhifa **MSIMAMIZI WA UCHAGUZI/MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI***
*futa isiyohitajika.

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 33)*

**FOMU Na. V**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA NAFASI YA MWENYEKITI WA KIJIJI MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

**FOMU Na. VI**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA NAFASI YA MWENYEKITI WA KITONGOJI 2019**

| **NEMBO YA HALMASHAURI** |
|---|

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

**FOMU Na. VII**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA NAFASI YA UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI MCHANGANYIKO MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

**FOMU Na. VIII**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA NAFASI YA UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI LA WANAWAKE MWAKA 2019**

| NEMBO YA HALMASHAURI |
|---|

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenzwa chini ya Kanuni ya 39, 40 na 41)*

**FOMU Na. IX**

**FOMU YA MATOKEO YA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI/KITONGOJI**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | CHAMA CHA SIASA | KURA ALIZOPATA | JINSI(KE/ME) | SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| 5. | | | | | |
| 6. | | | | | |
| 7. | | | | | |
| 8. | | | | | |
| 9. | | | | | |
| 10 | | | | | |

| | |
|---|---|
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | |
| Idadi ya waliopiga kura | |
| Idadi ya kura halali | |
| Idadi ya kura zilizoharibika | |
| Jina la Msimamizi wa Kituo | |

Saini…………………………………………………………………Tarehe………………

Muhuri wa Msimamizi wa Kituo…………………………………………………………

**FOMU Na. X**

**FOMU YA MATOKEO YA UCHAGUZI WA WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI MCHANGANYIKO/KUNDI LA WANAWAKE**

| **NEMBO YA HALMASHAURI** |
|---|

| Na. | JINA LA MGOMBEA | CHAMA CHA SIASA | KURA ALIZOPATA | JINSI (KE/ME) | SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | | | | | |
| Idadi ya waliopiga kura | | | | | |
| Idadi ya kura halali | | | | | |
| Idadi ya kura zilizoharibika/kukataliwa | | | | | |
| JUMLA | | | | | |
| Jina la Msimamizi wa Kituo | | | | | |

Saini……………………………………Tarehe…………………

Muhuri wa Msimamizi wa Kituo………………… ……… ..

**FOMU Na. XI**

**FOMU YA MATOKEO YA JUMLA YA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI/KITONGOJI**

| |
|---|
| **NEMBO YA HALMASHAURI** |

| Na. | JINA LA MGOMBEA | CHAMA CHA SIASA | KURA ALIZOPATA | JINSI(KE/ME) | SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| 5. | | | | | |
| 6. | | | | | |
| 7. | | | | | |
| 8. | | | | | |
| 9. | | | | | |
| 10 | | | | | |

| | |
|---|---|
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | |
| Idadi ya waliopiga kura | |
| Idadi ya kura halali | |
| Idadi ya kura zilizoharibika | |
| Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi | |

Saini…………………………………………………………………tarehe………………

Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………………………………………

**FOMU Na. XII**

**FOMU YA MATOKEO YA JUMLA YA UCHAGUZI WA WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI MCHANGANYIKO/ KUNDI LA WANAWAKE**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | CHAMA CHA SIASA | KURA ALIZOPATA | JINSI (KE/ME) | SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| 5. | | | | | |

| | |
|---|---|
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | |
| Idadi ya waliopiga kura | |
| Idadi ya kura halali | |
| Idadi ya kura zilizoharibika/kukataliwa | |
| JUMLA | |
| Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi | |

Saini…………………………………….tarehe………. …. ….

Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………………..

## JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 47(4))*

### VIAPO

*(a) Kiapo cha Uaminifu*

"Mimi ……………………………… naapa/natamka kwa dhati kwamba nitaitumikia vyema na kwa moyo thabiti Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi yangu kama …………………………………katika Halmashauri ya …………………… na katika kutimiza wajibu wa nafasi hiyo nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kwa vyovyote vile sitatoa siri zinazohusu majukumu yangu isipokuwa kwa mujibu wa sheria. Ewe Mwenyezi Mungu, nisaidie."

Kiapo/Tamko hili limetolewa hapa: ………………………………………………….

na……………………………………………………………………………………

Leo tarehe…………………… Mwezi wa……………………Mwaka 20…………....

Mbele ya:

**Jina:**…………………………………………….

**Saini:**……………………………………………

**Wadhifa:**………………………………………..

**Anuani.**…………………………………………

*(b) Kiapo cha Utii na Uadilifu*

Mimi ………………………………………………………… naapa/natamka kwa dhati kwamba nitaitumikia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wadhifa wangu wa …………………………………………… kwa uaminifu, kwa uwezo na moyo wangu wote na kwamba nitahifadhi, nitalinda na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria za Tanzania na Maadili ya Viongozi wa Umma kama yalivyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie"

Kiapo/Tamko hili limetolewa hapa: …………………………………………………………

na……………………………………………………………………………………………

Leo tarehe……………..… Mwezi wa………………Mwaka 20………...

Mbele ya:…………………………………………………………………… …

**Jina:………………………………………………………………………………**

**Cheo:……………………………………………………………………………**

**Saini:……………………………………………………………………………**

**Anuani……………………………………………………………………………**

JEDWALI LA SITA

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 51)*

**TARATIBU ZA MAADILI**

**1.0 Jina, Mtumizi, Wahusika wa Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019**

**1.1 Jina na Tarehe ya kuanza kutumika**

Taratibu hizi zitajulikana kama Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019.

**1.2 Wahusika wa Taratibu za Maadili**

Wahusika wa taratibu za Maadili hizi watakuwa wafuatao:-

(a) Vyama vya Siasa;

(b) Wagombea;

(c) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(d) Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi.

**2.0 Taratibu za Maadili**

**2.1 Wajibu wa Vyama vya Siasa na Wagombea**

Kila Chama cha Siasa na Wagombea watatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

(a) kuheshimu na kutekeleza Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi itakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni pamoja na kuzingatia matakwa ya Sheria nyingine za nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi;

(b) kuelimisha, kuhamasisha na kuwasisitiza wanachama na wafuasi wao kuheshimu Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi itakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni pamoja na Sheria nyingine za nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi;

(c) kuzingatia ratiba ya mikutano ya kampeni;

(d) kwa kushirikiana na wanachama na wafuasi wa Vyama vingine vya Siasa kuhakikisha kuwa wanachukua hatua za makusudi ili:-

(i) kufanya Uchaguzi uwe huru na wa haki;

(ii) kuzuia vitendo vya vurugu na vitisho;

(iii) kukataa aina yoyote ya ubaguzi katika misingi ya jinsia, maumbile, ulemavu, ukabila, dini au rangi; na

(iv) kueneza taarifa sahihi kuhusu mchakato wa Uchaguzi;

(e) kuchapisha vijitabu, vipeperushi, vitini, mabango na machapisho ya aina yoyote yanayoelezea sera zao baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa Uchaguzi;

(f) kutumia vyombo vya habari kutangaza sera zao kwa kuzingatia sheria zinazosimamia vyombo vya habari na Miongozo ya Uchaguzi;

(g) kujenga mazingira ambayo yatawezesha Uchaguzi kufanyika kwa uhuru na haki, ikiwa ni pamoja na kuwezesha makundi maalum kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi;

(h) kuhakikisha hifadhi na usafi wa mazingira katika kusambaza matangazo ya kampeni;

(i) kuondoa mabango, matangazo na machapisho ya aina yoyote ile yaliyotumika wakati wa kampeni katika sehemu za wazi baada ya Uchaguzi;

(j) kutoa taarifa mara moja kwa mamlaka husika wanapofahamu au wanapoona tukio linaloweza kusababisha vurugu au uvunjifu wa amani;

(k) kuhakikisha kuwa wanafanya kampeni kwa kuzingatia misingi inayolenga kutangaza sera za Vyama vyao pasipo kujenga chuki, kusababisha mifarakano na migawanyiko katika jamii;

(l) kuchukua hatua za lazima kuhakikisha kuwa hakuna migongano ya mikutano ya kampeni na Vyama vingine;

(m) kukataza wanachama au wafuasi kutamka kauli mbiu, kuonesha ishara za Vyama vyao, au kuvaa sare zenye rangi ya Chama chao katika mikutano ya hadhara ya Vyama vingine; na

(n) kuwaelekeza Mawakala wao watakaokuwepo katika Vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi.

**2.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Vyama vya Siasa na Wagombea**

Kila Chama cha Siasa au Mgombea hatatakiwa kufanya yafuatayo:-

(a) kusababisha au kufanya fujo au vurugu ya aina yoyote katika Mkutano wake au wa Chama kingine;

(b) kutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji na vitisho au lugha inayochochea uvunjifu wa amani au kuashiria ubaguzi wa kijinsia, dini, rangi, ulemavu au maumbile kwenye mikutano ya kampeni;

(c) kubeba sanamu, kinyago au kitu chochote ambacho kinaonyesha kudhalilisha, kukebehi, kufedhehesha au kukejeli Chama kingine cha Siasa au Mgombea au Kiongozi wa Chama kingine cha Siasa au Serikali katika mkutano wowote wa kampeni za Uchaguzi;

(d) kutumia vipaza sauti vya aina yoyote kwa shughuli za kisiasa mara baada ya muda wa kampeni za Uchaguzi kumalizika;

(e) kuchafua, kubandua au kuharibu kwa namna yoyote ile matangazo ya kampeni ya Vyama vingine vya Siasa na matangazo mengine yanayotolewa na Mamlaka za Uchaguzi;

(f) kubandika mabango ya kampeni, matangazo au mchoro wowote kwenye nyumba, majengo au vyombo vya usafiri vya watu binafsi au taasisi mbalimbali bila idhini ya wamiliki husika;

(g) kubandika mabango ya kampeni, matangazo au mchoro wowote kwenye nyumba za ibada, taasisi za dini na majengo ya Serikali na taasisi zake;

(h) kutoa rushwa ili kumshawishi mtu yeyote kupiga kura, kugombea au kujitoa katika kugombea nafasi ya uongozi;

(i) kuzuia mtu yeyote, watu au wafuasi wa vyama vingine kuhudhuria mikutano ya kampeni au kupiga kura;

(j) kukodi au kutumia usafiri wa aina yoyote kubeba na kusafirisha wapiga kura kwa madhumuni ya kushawishi kupigiwa kura.

**2.3 Maadili wakati wa kupiga, kuhesabu, kujumlisha kura na kutangaza matokeo ya Uchaguzi**

**2.3.1. Yanayotakiwa Kufanywa**

(a) Vyama vya Siasa na Wagombea watahakikisha kuwa Mawakala wao wanakula kiapo na kukiwasilisha kwa Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kabla ya siku ya Uchaguzi;

(b) Mawakala wa Vyama vya Siasa, Vyama vya Siasa na Wagombea watakuwa na wajibu wa kushirikiana na Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo katika vituo vya kupigia kura kwa kuzingatia Kanuni za Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi;

(c) Viongozi wa Vyama vya Siasa watakuwa na wajibu wa kuwaelimisha wanachama na wafuasi wao kuwa, watatakiwa kuondoka eneo la kupigia Kura mara tu wamalizapo kupiga kura na kama itawalazimu kubakia katika eneo hilo watatakiwa kukaa umbali wa mita mia mbili kutoka kituo cha kupigia kura.

**2.3.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa**

(a) Kampeni za uchaguzi haziruhusiwa siku ya upigaji kura. Hii ni pamoja na kuvaa vazi lolote au kuwa na kitu chochote kinachoashiria kushawishi watu kumpigia kura Mgombea fulani au utambuzi wa

Mgombea fulani au matumizi ya chombo cha usafiri kinachoashiria utambuzi wa Chama au Mgombea wa Chama chochote;

(b) Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wagombea na wafuasi wao watatakiwa kujiepusha na vitendo vinavyoweza kusababisha fujo au vurugu katika vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura;

(c) Hakuna mtu atakayeruhusiwa kutumia simu ya kiganjani ndani ya kituo cha kuhesabu na kujumlishia kura isipokuwa Msimamizi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na mlinzi wa kituo cha kupigia kura ambao watatumia simu zao pale itakapobidi kwa shughuli za Uchaguzi tu na simu hizo wakati wote ziwe zimeondolewa mlio na ziwe kwenye mtetemo;

(d) Kiongozi au Mtendaji au mwanachama au mfuasi wa Chama cha Siasa hatatakiwa:

(i) kuvamia au kukaa kwa nguvu ndani ya kituo cha kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura;

(ii) kuwahamasisha wanachama au wafuasi kupiga kura zaidi ya mara moja katika Uchaguzi mmoja;

(iii)kununua kura au kutoa rushwa au aina yoyote ya malipo ya fedha au vifaa kwa mpiga kura au Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(iv)kutumia lugha ya matusi kwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo katika kituo cha kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura.

**3.0 Wajibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Serikali itakuwa na Wajibu wa:**

(a) kutoa fursa sawa kwa wadau wote wa Uchaguzi hususan Vyama vya Siasa na Wagombea ili kuendesha shughuli zao za kisiasa wakati wa Uchaguzi kwa uhuru na kuzingatia sheria za nchi;

(b) kuhakikisha hali ya usalama, amani na utulivu wakati wote wa Uchaguzi;

(c) kuhakikisha kuwa viongozi na watendaji wake wanazingatia ipasavyo ukomo wa madaraka yao katika shughuli za Uchaguzi.

**4.0 Taratibu za Maadili kwa Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi**

**4.1 Mambo wanayotakiwa Kufanya**

Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi watakuwa na wajibu wa kupanga, kusimamia na kuendesha Uchaguzi katika misingi inayowezesha Uchaguzi kuwa huru na wa haki kwa kufanya yafuatayo:-

(a) kuzingatia Katiba ya Nchi, Kanuni za Uchaguzi na Sheria nyingine za nchi;

(b) kuvipatia Vyama vya Siasa ratiba na taarifa za Uchaguzi mapema;

(c) kutoa Elimu ya Mpiga Kura, kusimamia na kuratibu taasisi na watu wanaotoa Elimu ya Mpiga Kura;

(d) kutoa mafunzo kwa wanaohusika na Uchaguzi ili kuwawezesha kuendesha uchaguzi kwa ufanisi;
(e) kuvipatia Vyama vya Siasa Kanuni, Miongozo ya Uchaguzi na Nyaraka nyingine zinazohusiana na Uchaguzi;
(f) kukemea vitendo vyenye nia ya kuharibu Uchaguzi vinavyoweza kufanywa na Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wagombea au wafuasi wao;
(g) kuendesha na kuziwezesha Kamati za kusimamia Maadili ya Uchaguzi na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yanayotolewa na Kamati hizo;
(h) kukutana na Vyama vya Siasa pale inapobidi kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Kampeni za Uchaguzi na Uchaguzi wenyewe;
(i) kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote atakayefanyiwa uonevu au kukoseshwa haki wakati wa shughuli za Uchaguzi;
(j) kutambua majukumu ya Vyama vya Siasa, Wagombea na Mawakala wao;
(k) kuandaa na kupeleka kwa wakati vifaa kwenye vituo vya kupigia kura;
(l) kuendesha zoezi la Uchaguzi kwa uwazi, haki na uadilifu.

**4.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi**

(a) kupendelea Chama chochote cha Siasa au Mgombea yeyote;
(b) kubadili ratiba za Kampeni za Uchaguzi bila kuvishirikisha Vyama vya Siasa;
(c) kuchelewa au kupeleka vifaa pungufu katika vituo vya kupigia kura bila sababu za msingi;
(d) kuchelewa kutangaza Matokeo ya Uchaguzi bila sababu za msingi.

**5.0 Usimamizi wa Utekelezaji waTaratibu za Maadili ya Uchaguzi**

**5.1 Kamati za Maadili za kusimamia Utekelezaji wa Taratibu za Maadili ya Uchaguzi**

Kutakuwa na Kamati za Maadili zifuatazo zitakazoundwa na Msimamizi wa Uchaguzi:-

(a) Kamati ya Maadili ya Halmashauri; na
(b) Kamati ya Maadili ya Kata.

**5.2 Muundo wa Kamati za Taratibu za Maadili ya Uchaguzi**

**5.2.1 Kamati ya Maadili ya Halmashauri**

Kamati ya Maadili ya Halmashauri itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi katika Halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
(b) Mjumbe mmoja kutoka kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi katika Halmashauri;
(c) Mjumbe mmoja atakayewakilisha Serikali ambaye atateuliwa kwa maandishi na Katibu Tawala wa Wilaya husika; na

(d) Afisa Uchaguzi ambaye atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi.

**5.2.2 Kamati ya Maadili ya Kata**

Kamati ya Maadili ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Msimamizi Msaidizi ngazi ya Kata husika ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
(b) Mjumbe mmoja kutoka kila Chama cha Siasa kinachoshiriki katika Uchaguzi kwenye Kata;
(c) Mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali atakayeteuliwa kwa maandishi na Katibu Tawala wa Wilaya husika; na
(d) Katibu ambaye ni Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kijiji atakayeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

**5.2.3 Utoaji wa taarifa za Kamati za Maadili**

Itakuwa ni marufuku kwa mtu, mgombea, Chama cha Siasa au mjumbe wa Kamati ya Maadili ambaye siyo Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili kutoa taarifa yoyote kuhusu maamuzi ya Kamati au suala lolote lililopo mbele ya Kamati.

**5.3 Uwasilishaji wa Malalamiko**

Mgombea yeyote, Wasimamizi au Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, Serikali au Chama chenye Mgombea kinachoamini kwamba Maadili ya Uchaguzi yamekiukwa kitawasilisha malalamiko kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Kata kwa maandishi.

**5.4 Muda wa kuwasilisha Malalamiko**

Malalamiko yoyote yatatakiwa kuwasilishwa ndani ya siku tatu tangu kutokea kwa tukio linalolalamikiwa.

**5.5 Kuitisha kikao cha Kamati ya Maadili ya Uchaguzi**

Mwenyekiti wa Kamati husika baada ya kupokea malalamiko na kujiridhisha kuwa Taratibu za Maadili zimekiukwa atatakiwa kuitisha kikao ndani ya siku mbili.

**5.6 Namna ya kushughulikia Malalamiko**

(a) Malalamiko yote yatajadiliwa na kuamuliwa katika kikao cha Kamati ya Maadili ya Kata husika;
(b) Kamati itashughulikia malalamiko na kutoa uamuzi wake mapema iwezekanavyo;
(c) Baada ya kupokea malalamiko, Kamati itamtaka aliyelalamikiwa kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku mbili tangu kupokea malalamiko;

(d) Katika kushughulikia malalamiko, Kamati inaweza kumwita mtu yeyote kutoa maelezo ili kusaidia Kamati kufikia maamuzi ya haki;

(e) Akidi ya Kikao cha Kamati husika itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa Kamati;

(f) Kamati ya Maadili ya Uchaguzi itaamua malalamiko yote baada ya kusikiliza au kupata maelezo ya utetezi kutoka kwa pande zote mbili ambazo ni mlalamikaji na mlalamikiwa ndani ya siku mbili isipokuwa kama upande unaolalamikiwa utashindwa kuwasilisha maelezo ya utetezi katika muda uliopainishwa Kamati inaweza kufanya uamuzi;

(g) Maamuzi yatakayofikiwa na Kamati ya Maadili ya Kata yatatekelezwa na pande zinazohusika na maamuzi hayo;

(h) Ikitokea kuna umuhimu wa kufanya maamuzi kwa kupiga kura, wawakilishi wa Mlalamikaji na Mlalamikiwa hawataruhusiwa kupiga kura;

(i) Malalamiko yatakayoshughulikiwa na Kamati za Maadili ni yale tu yaliyotokea katika kipindi cha Kampeni;

(j) Malalamiko yatakayotokea siku ya Upigaji Kura yatashughulikiwa kwa kuzingatia Kanuni za Uchaguzi;

(k) Kamati itakuwa na mamlaka ya kuchunguza malalamiko yote yatakayowasilishwa kabla ya kufanya maamuzi;

(l) Kamati inaweza kuelekeza malalamiko mengine kwenye mamlaka zinazohusika kama itakavyoona inafaa kwa hatua zinazostahili.

**5.7 Rufaa Dhidi ya Maamuzi**

(a) Upande ambao hautaridhika na uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Kata, utakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Kamati ya Maadili ya Halmashauri ndani ya siku mbili tangu uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Kata ulipotolewa; na

(b) Uamuzi utakaotolewa na Kamati ya Maadili ya Halmashauri utakuwa ni wa mwisho.

**5.8 Malalamiko dhidi ya Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi**

(a) Pale ambapo malalamiko yaliyowasilishwa ni dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi, Msimamizi au Msimamizi Msaidizi, Msimamizi wa Uchaguzi hataendesha Kikao hicho, isipokuwa Katibu Tawala wa Mkoa atateua Afisa yeyote wa Umma Mwandamizi kutoka Sekretarieti ya Mkoa kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho;

(b) Iwapo Kamati itaona kuwa Msimamizi amekosea Kamati itamtaka Msimamizi wa Uchaguzi kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo.

**5.9 Malalamiko dhidi ya Serikali**

Kamati ya Maadili ya Kata itapokea malalamiko yatakayotolewa dhidi ya Serikali na iwapo Kamati itaona kuwa Serikali imekosea itaitaka Serikali kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo.

**5.10 Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Halmashauri na Kata katika kushughulikia Malalamiko na kutoa adhabu**

Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Halmashauri na Kata zinaweza kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) kuagiza upande uliokiuka maadili kusahihisha kosa au makosa yaliyotendeka na iwapo italazimu, kuomba msamaha hadharani;

(b) kutoa onyo au karipio kwa maandishi;

(c) kutangaza jina la Chama au Mgombea aliyekiuka Maadili na kueleza kosa au makosa yake kwa njia za Taarifa kwa Umma, redio, televisheni, magazeti na njia nyingine za mawasiliano;

(d) Kamati inaweza kukisimamisha Chama au Mgombea kuendelea kufanya Kampeni za Uchaguzi kwa muda itakavyoona inafaa.

**5.11 Kushindwa Kutekeleza Maamuzi ya Kamati za Maadili**

Pale ambapo Mgombea au Chama kitashindwa kutekeleza maamuzi ya Kamati husika, Kamati ya Maadili ya Uchaguzi inaweza kukisimamisha Chama husika kufanya kampeni za Uchaguzi.

DODOMA
25/04/2019

SELEMANI S. JAFO (Mb)
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 374 la tarehe 26/04/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

SURA 288

# KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI, WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI NA MWENYEKITI WA KITONGOJI KATIKA MAMLAKA ZA MIJI ZA MWAKA 2019

TANGAZO LA SERIKALI NA. 374 la tarehe 26/04/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

SURA 288

Zimetungwa chini ya Kifungu 87A

KANUNI ZA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI, WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI NA MWENYEKITI WA KITONGOJI KATIKA MAMLAKA ZA MIJI ZA MWAKA 2019

MPANGILIO WA KANUNI

| Kanuni | Jina | Uk |
|---|---|---|
| 1 | Jina | 144 |
| 2 | Eneo la matumizi na tarehe ya kuanza kutumika | 144 |
| 3 | Tafsiri | 144 |
| 4 | Tangazo la uchaguzi kwa umma | 146 |
| 5 | Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji | 146 |
| 6 | Mwenyekiti na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji | 146 |
| 7 | Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi | 146 |
| 8 | Kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo | 147 |
| 9 | Maelekezo kuhusu uchaguzi | 147 |
| 10 | Orodha ya Wapiga Kura. | 148 |
| 11 | Uandikishaji wa Wapiga Kura | 148 |
| 12 | Pingamizi kuhusu uandikishaji | 149 |
| 13 | Sifa za mpiga kura. | 150 |
| 14 | Kupoteza sifa ya kupiga kura | 150 |
| 15 | Sifa za Mgombea | 150 |
| 16 | Kupoteza sifa ya kuwa Mgombea | 150 |
| 17 | Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi | 151 |
| 18 | Utaratibu wa uteuzi wa Wagombea | 152 |

*Tangazo la Serikali Na. 374 (Linaendelea)*


| | | |
|---|---|---|
| 19 | Kupita bila kupingwa | 152 |
| 20 | Kujitoa kwa Mgombea | 153 |
| 21 | Kufariki kwa Mgombea | 153 |
| 22 | Ukomo wa kuwa madarakani | 154 |
| 23 | Pingamizi kuhusu uteuzi | 154 |
| 24 | Kamati ya Rufaa | 155 |
| 25 | Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Rufaa | 155 |
| 26 | Majukumu ya Kamati ya Rufaa | 155 |
| 27 | Kampeni za Mchaguzi | 156 |
| 28 | Wajibu wa Jeshi la Polisi | 156 |
| 29 | Mabadiliko ya ratiba | 156 |
| 30 | Masharti ya kampeni | 157 |
| 31 | Mahali, vituo na muda wa kupigia kura | 157 |
| 32 | Masanduku ya kura | 158 |
| 33 | Karatasi za kupigia kura | 158 |
| 34 | Utambulisho wa mpiga kura | 158 |
| 35 | Upigaji kura | 159 |
| 36 | Usaidizi kwa wenye mahitaji maalum | 160 |
| 37 | Kuahirisha upigaji kura | 160 |
| 38 | Kuhesabu kura | 160 |
| 39 | Matokeo ya Mwenyekiti wa Kitongoji | 161 |
| 40 | Matokeo ya Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji | 161 |
| 41 | Matokeo ya Mwenyekiti wa Kijiji | 163 |
| 42 | Taratibu za kurudia Uchaguzi | 163 |
| 43 | Masuala yasiyobatilisha matokeo | 163 |
| 44 | Malalamiko kuhusu uendeshaji wa Mchaguzi | 163 |
| 45 | Nafasi wazi | 164 |
| 46 | Uchaguzi Mdogo | 164 |
| 47 | Kiapo | 165 |
| 48 | Makosa ya Mchaguzi | 165 |
| 49 | Kinga | 166 |
| 50 | Waangalizi wa ndani wa Mchaguzi | 167 |
| 51 | Taratibu za Maadili | 167 |
| 52 | Miongozo | 167 |
| 53 | Elimu ya Mpiga Kura | 167 |
| 54 | Kufutwa kwa Kanuni za Uchaguzi Tangazo la Serikali Na.321 la Mwaka 2014. | 167 |

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2019.

Eneo la matumizi na tarehe ya kuanza kutumika

2. Kanuni hizi zitatumika katika Vijiji na Vitongoji vyote vilivyomo katika maeneo ya Mamlaka za Miji na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi isipokuwa pale itakavyoelezwa vinginevyo:-

Sura 258

"Chama cha Siasa" maana yake ni Chama cha Siasa kilichopata usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa;

"Kijiji" maana yake ni Kijiji kilichomo katika eneo la Mamlaka za Miji;

"Kitongoji" maana yake ni sehemu ya eneo la utawala katika Kijiji kilichopo ndani ya Mamlaka za Miji;

"Mamlaka ya Uchaguzi" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

"mkazi" maana yake ni raia wa Tanzania ambaye anaishi kwenye eneo la Kijiji au Kitongoji na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Kijiji au Kitongoji;

"Msimamizi wa Uchaguzi" maana yake ni mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa na Mamlaka ya Uchaguzi kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi" maana yake ni mtumishi yeyote wa umma aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kuwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi chini ya Kanuni hizi;

"Mtendaji wa Kijiji" maana yake ni mtendaji mkuu wa shughuli za Serikali katika Kijiji na ni pamoja na mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mtendaji wa Kijiji kwa mujibu wa Kanuni hizi;

katika utumishi wa umma;

"Orodha ya Wapiga Kura" maana yake ni orodha ya majina ya wapiga kura iliyoandaliwa chini ya Kanuni hizi;

Sura 357

"raia" maana yake ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia;

"sehemu ya matangazo ya uchaguzi" maana yake ni sehemu maalum iliyoteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa ajili ya kutolea matangazo au taarifa mbalimbali za uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"siku ya uteuzi" maana yake ni siku ya kutangaza majina ya wanaostahili na wasiostahili kugombea nafasi za uongozi chini ya Kanuni hizi;

"Uchaguzi" maana yake ni Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji;

"Uchaguzi Mdogo" maana yake ni uchaguzi ambao utafanyika baada ya kuwepo kwa nafasi wazi ya Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji au Mjumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

"wakati wa uchaguzi" maana yake ni muda ambao uchaguzi wa kawaida au Uchaguzi Mdogo unafanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi na unaanzia tarehe ya tangazo la uchaguzi hadi matokeo ya uchaguzi yanapotangazwa;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

SEHEMU YA PILI
TANGAZO LA UCHAGUZI

Tangazo la uchaguzi kwa umma

**4.** (1) Kutakuwa na uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji ambao utafanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi baada ya Waziri kutoa Tangazo la Uchaguzi kwa umma.

(2) Tangazo la Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) litatolewa katika magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa nchi nzima na katika vyombo mbalimbali vya habari siku tisini kabla ya siku ya uchaguzi.

(3) Tangazo litakalotolewa na Waziri litaelekeza mambo yafuatayo:

(a) ratiba ya uchaguzi na shughuli zinazohusika na; na

(b) masharti muhimu ya uchaguzi kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi.

Majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji

**5.** Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza katika sehemu ya matangazo ya Uchaguzi majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji vilivyomo katika eneo la Halmashauri husika kwa kuzingatia orodha ya Vijiji na Vitongoji iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali siku sabini na mbili kabla ya siku ya

Uchaguzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji.

Mwenyekiti na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji

**6.** (1) Halmashauri ya Kijiji itakuwa na Wajumbe ambao idadi yao haitazidi wajumbe ishirini na watano.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji watakuwa ni:

(a) Mwenyekiti wa Kijiji;

(b) Wenyeviti wa Vitongoji vilivyomo katika eneo la Kijiji; na

(c) Wajumbe watakaochaguliwa wakiwemo wanawake wasiopungua theluthi moja ya wajumbe wote wa Halmashauri ya Kijiji.

Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi

7. (1) Kutakuwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo au mtumishi wa umma atakayeteuliwa kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Mtu hatateuliwa kuwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo endapo ni:

(a) Kiongozi wa chama cha siasa;
(b) Mgombea;
(c) Hakimu au Jaji;
(d) Kiongozi wa dini;
(e) Askari wa jeshi lolote;
(f) Katibu Tawala wa Wilaya ;
(g) Katibu Tawala wa Mkoa;
(h) Mkuu wa Wilaya; au
(i) Mkuu wa Mkoa.

Kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo

8. Kila Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Wajumbe wa Kamati ya Rufani au mtumishi wa umma atakayeteuliwa kusimamia Uchaguzi kwa mujibu wa Kanuni hizi atasimamia Uchaguzi kwa kuzingatia sheria, kanuni, maelekezo na matangazo yatakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TATU
## MAELEKEZO YA UCHAGUZI

Maelekezo kuhusu uchaguzi

9. (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatoa maelekezo ya Uchaguzi siku sitini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.

(2) Maelekezo ya Uchaguzi, kwa mujibu wa Kanuni hizi, yataelekeza mambo yafuatayo:

(a) tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi;
(b) muda na sehemu ya kuandikisha wapiga kura;
(c) muda na mahali pa kufanyia Uchaguzi;
(d) kuwataka wakazi wote wenye sifa za kupiga kura kushiriki Uchaguzi;
(e) kuwataka wakazi wenye umri wa miaka ishirini na moja au zaidi wanaotaka kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji kuchukua fomu za kugombea

zitakazopatikana kwenye ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(f) tarehe na muda wa kuchukua na kurudisha fomu za maombi ya kugombea uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(g) siku ambayo uteuzi utafanyika na sehemu ya matangazo ya uchaguzi ambapo fomu za wagombea zitabandikwa;

(h) muda wa kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi na kusikilizwa kwa pingamizi;

(i) tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(j) kipindi cha kuendesha mikutano ya kampeni za uchaguzi; na

(k) masuala mengine yanayohusu Uchaguzi.

Orodha ya Wapiga Kura

**10.** (1) Kutakuwa na Orodha ya Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni Ndogo ya (1), Msimamizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa watumishi wa umma watakaoandikisha na kuandaa Orodha ya Wapiga Kura katika Vitongoji siku hamsini na mbili kabla ya siku ya Uchaguzi.

(3) Watendaji wa Vijiji na Kata hawatateuliwa wala hawataruhusiwa kuandikisha au kuandaa Orodha ya Wapiga Kura.

Uandikishaji wa Wapiga Kura

**11.** (1) Uandikishaji na uandaaji wa Orodha ya Wapiga Kura utaanza siku ya arobaini na saba kabla ya siku ya Uchaguzi na utafanyika kwa muda wa siku saba kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi katika majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika kwenye sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na Viongozi wa Vyama vya Siasa.

(2) Vituo vya uandikishaji wa wapiga kura vitafunguliwa saa mbili kamili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili kamili jioni.

(3) Chama cha Siasa kitaruhusiwa kuteua wakala wake kwa kila kituo cha uandikishaji wa wapiga kura wakati wa uandikishaji wa wapiga kura.

(4) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika sehemu ya matangazo ya uchaguzi nakala ya Orodha ya Wapiga Kura siku moja baada ya

kukamilika kwa uandikishaji wa wapiga kura na atatunza nakala halisi ya Orodha hiyo.

(5) Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya Wapiga Kura atakuwa na haki ya kukagua Orodha ya Wapiga Kura katika muda wa siku saba tangu tarehe ya Orodha hiyo kubandikwa sehemu ya matangazo ya uchaguzi ili:

(a) kuweka pingamizi kuhusu usahihi wa Orodha hiyo;

(b) kuomba Orodha irekebishwe kwa:-

(i) kuongeza jina lake;

(ii) kubadilisha taarifa zilizoko katika Orodha hiyo; au

(iii) kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa amefariki.

Pingamizi kuhusu uandikishaji

**12.** (1) Mkazi ambaye amejiandikisha katika Orodha ya Wapiga Kura anaweza kuweka pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura kabla ya kumalizika kwa muda wa kukagua Orodha ya Wapiga Kura.

(2) Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atatakiwa kutoa uamuzi kuhusu pingamizi lililowekwa ndani ya siku mbili tangu tarehe ya mwisho ya ukaguzi wa Orodha ya Wapiga Kura.

(3) Endapo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataridhika na pingamizi lililowekwa chini ya Kanuni hii, atarekebisha Orodha ya Wapiga Kura iliyotangazwa baada ya muda wa siku mbili isipokuwa kama uamuzi wake umekatiwa rufaa.

(4) Endapo mtu aliyeweka au aliyewekewa pingamizi hatoridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi lililowasilishwa kwake, mtu huyo atawasilisha rufaa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ndani ya muda wa siku mbili tangu kutolewa kwa uamuzi wa pingamizi.

(5) Msimamizi wa Uchaguzi, baada ya kupokea rufaa hiyo, ataishughulikia na kuitolea uamuzi ndani ya muda wa siku nne tangu siku ya kupokea rufaa hiyo.

(6) Uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni Ndogo ya (4) utakuwa wa mwisho.

Sifa za mpiga kura

13. Mkazi yeyote atakuwa na haki ya kupiga kura endapo atakuwa na sifa zifuatazo:
 (a) ni raia wa Tanzania;
 (b) ana umri wa miaka kumi na nane au zaidi;
 (c) ni mkazi wa eneo la Kitongoji;
 (d) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu; na
 (e) awe amejiandikisha kupiga kura katika Kitongoji husika.

Kupoteza sifa ya kupiga kura

14. Mtu hatakuwa na haki ya kupiga kura endapo:
 (a) hana mojawapo ya sifa zilizoainishwa katika Kanuni ya 13; au
 (b) amejiandikisha kupiga kura katika kituo zaidi ya kimoja.

Sifa za Mgombea

15. Mkazi yeyote wa Kitongoji anaweza kugombea uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji endapo:-
 (a) ni raia wa Tanzania;
 (b) ana umri wa miaka ishirini na moja au zaidi;
 (c) ana uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;
 (d) ana shughuli halali ya kumwezesha kuishi;
 (e) ni mkazi wa eneo la Kitongoji;
 (f) ni mwanachama wa Chama cha Siasa na amedhaminiwa na Chama hicho;
 (g) hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya Uchaguzi; na
 (h) hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na Daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya Utabibu.

Kupoteza sifa ya kuwa mgombea

16. (1) Mtu hatakuwa na sifa za kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji endapo:
 (a) amepoteza au hana sifa za mgombea zilizoainishwa katika Kanuni ya 15;
 (b) amehukumiwa hukumu ya kifo na Mahakama za Tanzania au anatumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita jela;
 (c) ana mkataba au maslahi kwenye kampuni

ambayo ina mkataba na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambayo anagombea nafasi ya uongozi na hajatangaza kuwepo kwa mkataba au maslahi yake kupitia kwenye gazeti linalopatikana katika eneo husika au mbao za matangazo katika ofisi ya Kijiji;

(d) amepoteza sifa ya kupiga kura chini ya Kanuni hizi au kwa mujibu wa Sheria yeyote inayohusu makosa ya uchaguzi;

(e) hatojaza fomu ya tamko la kuheshimu taratibu za maadili; au

(f) ataajiriwa au kuteuliwa katika wadhifa wowote katika Utumishi wa Umma au kuchaguliwa katika nafasi ya udiwani, ubunge, uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umakamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni ya 16(1)(b):

(a) adhabu mbili au zaidi za kifungo zinazotakiwa kutumikiwa kwa kufuatana zitachukuliwa kuwa ni adhabu tofauti iwapo kati ya adhabu hizo hakuna inayozidi miezi sita jela lakini endapo kati ya adhabu hizo kuna inayozidi miezi sita jela itachukuliwa kuwa ni adhabu moja; au

(b) kifungo cha jela kilichosababishwa na kushindwa kulipa faini hakitohesabiwa kuwa ni adhabu ya kifungo.

## SEHEMU YA NNE
## UTEUZI WA WAGOMBEA

Muda wa kuchukua na kurudisha fomu za uteuzi

**17.** (1) Mtu yeyote anayekusudia kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji atatakiwa kuchukua fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi husika siku zisizopungua ishirini na sita kabla ya siku ya uchaguzi kwa kadri itakavyoelekezwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(2) Mtu aliyechukua fomu kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) atatakiwa kurejesha fomu husika ndani ya muda wa siku saba tangu siku ya kwanza ya uchukuaji wa fomu iliyotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(3) Fomu za uteuzi wa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji zitatolewa na kupokelewa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

(4) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi hataruhusiwa kupokea kutoka kwa mtu yeyote fomu za uteuzi zitakazowasilishwa baada ya saa kumi kamili jioni ya siku ya mwisho ya kurejesha fomu.

(5) Fomu ya uteuzi wa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itakuwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

**Utaratibu wa uteuzi wa Wagombea**

**18.** (1) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji na uenyekiti wa Kitongoji siku kumi na tisa kabla ya tarehe ya Uchaguzi kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

(2) Baada ya uteuzi kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika majina ya wagombea wenye sifa na wasio na sifa za kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya kijiji au uenyekiti wa Kitongoji sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

(3) Endapo baada ya saa kumi kamili jioni ya siku ya mwisho ya kurejesha fomu za uteuzi kutakuwa hakuna mwombaji aliyejitokeza au kama waombaji wote waliojitokeza hawana sifa zinazostahili, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika siku iliyopangwa kwa ajili ya uteuzi atavitaarifu Vyama vya Siasa na wakazi wa Kijiji au Kitongoji kuhusu kukosekana kwa waombaji au kutokuwepo kwa waombaji wenye sifa.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni Ndogo ya (3), Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atavitaarifu Vyama vya Siasa na wakazi wa Kijiji au Kitongoji husika kuhusu kurudiwa kwa mchakato wa uchaguzi baada ya siku arobaini kuanzia tarehe ya uteuzi.

**Kupita bila kupingwa**

**19.** (1) Endapo siku ya uteuzi kutakuwa na mwombaji mmoja aliyejitokeza katika nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji na mwombaji huyo akateuliwa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mwombaji huyo kuwa ni mshindi wa

nafasi aliyoomba kugombea kwa kupita bila kupingwa.

(2) Endapo idadi ya waombaji wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa kundi mchanganyiko yaani wanaume na wanawake au kwa kundi la wanawake waliojitokeza na kuteuliwa itakuwa sawa na idadi ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni ya 6 ya Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza waombaji hao kuwa ni washindi wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa kundi husika kwa kupita bila kupingwa.

(3) Endapo idadi ya waombaji wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji waliojitokeza kwa kundi mchanganyiko yaani la wanaume na wanawake au kwa kundi la wanawake na kuteuliwa itakuwa chini ya idadi ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni ya 6 ya Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza waombaji hao kuwa ni washindi wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa kundi husika kwa kupita bila kupingwa na taratibu za kujaza nafasi zilizobaki zitaanza baada ya siku arobaini kuanzia tarehe ya uteuzi.

Kujitoa kwa mgombea

20.(1) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea aliyeteuliwa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au Kitongoji atajitoa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi wa mgombea huyo na wagombea waliobaki watapigiwa kura ili kupata mshindi.

(2) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea aliyeteuliwa kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au Kitongoji atajitoa na kubaki mgombea mmoja wa nafasi hiyo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyebaki kuwa mshindi wa nafasi iliyoombwa kwa kupita bila kupingwa.

(3) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya kijiji atajitoa, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatengua uteuzi huo na wagombea waliobaki wataendelea na hatua ya uchaguzi ili kumpata mshindi.

Kufariki kwa mgombea

21.(1) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au Kitongoji atafariki, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha Uchaguzi wa nafasi hiyo na Chama cha Siasa kilichotoa mgombea aliyefariki kinaweza kuwasilisha

jina la mwombaji mwingine ndani ya siku arobaini tangu kuahirishwa kwa Uchaguzi ili hatua za uteuzi wa mwombaji huyo zifanyike.

(2) Endapo, baada ya uteuzi kufanyika, mgombea wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji atafariki, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataahirisha uchaguzi wa nafasi hiyo na Chama cha Siasa kilichotoa mgombea aliyefariki kinaweza kuwasilisha jina la mwombaji mwingine ndani ya siku arobaini tangu kuahirishwa kwa Uchaguzi ili hatua ya uteuzi wa mwombaji huyo zifanyike.

Ukomo wa kuwa madarakani

**22.** Wenyeviti wa Vijiji, Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji watakoma kushika nafasi hizo siku saba kabla ya siku ya kuchukua fomu za kugombea uongozi chini ya Kanuni hizi.

## SEHEMU YA TANO
## UTARATIBU WA KUSHUGHULIKIA PINGAMIZI NA RUFAA

Pingamizi kuhusu uteuzi

**23.** (1) Mtu yeyote aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au anapinga uteuzi wa mgombea yeyote, anaweza kuwasilisha pingamizi na kumwomba Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kupitia upya uamuzi uliofanyika ili amteue kuwa mgombea au atengue uteuzi anaoupinga na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kupitia pingamizi husika, anaweza kukubali au kulikataa pingamizi hilo.

(2) Pingamizi chini ya Kanuni Ndogo ya (1) litawasilishwa kwa maandishi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika muda wa siku mbili tangu uamuzi au uteuzi ulipofanyika na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi katika muda usiozidi siku mbili kuanzia siku ya kupokea pingamizi hilo.

(3) Mwombaji au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufaa iliyoanzishwa chini ya Kanuni ya 24 katika muda usiozidi siku nne kuanzia tarehe ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Kamati ya Rufaa

**24.** (1) Kutakuwa na Kamati ya Rufaa katika kila Wilaya ambayo itasikiliza mapingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea wa Uchaguzi katika Wilaya husika.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Rufaa watateuliwa na Katibu Tawala wa Mkoa siku saba kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Kanuni ya 25.

(3) Kamati ya Rufaa itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Katibu Tawala wa Wilaya ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) watumishi wanne wa umma kutoka taasisi za umma zilizopo katika Wilaya husika; na

(c) mtumishi mmoja wa umma ambaye atakuwa Katibu na hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Sifa za Wajumbe wa Kamati ya Rufaa

**25.** Mtu yeyote hatateuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Rufaa endapo:

(a) anahusika na uteuzi wa wagombea;

(b) ni Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo;

(c) ni mtumishi wa Halmashauri; au

(d) kiongozi wa Chama cha Siasa katika ngazi yoyote.

Majukumu ya Kamati ya Rufaa

**26.** (1) Kamati ya Rufaa itakuwa na majukumu ya kupokea, kusikiliza na kutoa uamuzi wa rufaa iliyowasilishwa chini ya Kanuni ya 23(3).

(2) Kamati ya Rufaa itatoa uamuzi wa rufaa ndani ya muda wa siku nne kuanzia siku ya kupokea rufaa na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(3) Mtu aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Kamati ya Rufaa atakuwa na haki ya kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya muda wa siku thelathini baada ya matokeo ya uchaguzi kutangazwa.

SEHEMU YA SITA
KAMPENI ZA UCHAGUZI

Kampeni za Uchaguzi

**27.** (1) Kampeni za Uchaguzi zitafanyika siku saba kabla ya siku ya Uchaguzi.

(2) Kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi kitawasilisha ratiba yake ya mikutano ya kampeni ya uchaguzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si chini ya siku saba kabla ya kuanza kwa kampeni.

(3) Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha ratiba za mikutano ya kampeni zilizowasilishwa na Vyama vya Siasa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (2) baada ya maridhiano na Vyama vya Siasa vinavyoshiriki Uchaguzi na atatakiwa kuwasilisha ratiba ya mikutano ya kampeni za Uchaguzi iliyounganishwa siku tatu kabla ya kampeni kuanza kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya.

(4) Endapo Vyama Vya Siasa vitashindwa kuridhiana wakati wa uunganishaji wa ratiba za mikutano ya kampeni, Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha ratiba za mikutano ya kampeni na uamuzi wake utakuwa wa mwisho.

(5) Mgombea au mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kinaweza kuitisha na kuhutubia mikutanu ya kampeni kwa mujibu wa ratiba ya mikutano ya kampeni iliyoandaliwa na kuwasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya na mikutano hiyo itaratibiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Wajibu wa Jeshi la Polisi

**28.** (1) Mkuu wa Polisi wa Wilaya atakuwa na wajibu wa kuhakikisha ulinzi na usalama katika mikutano ya kampeni.

(2) Ratiba ya mikutano ya kampeni za Uchaguzi itakayowasilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya chini ya Kanuni ya 27(3) itakuwa ni taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni na mgombea au Chama chake hakitowajibika kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi.

(3) Mikutano ya kampeni za Uchaguzi kwa mujibu wa ratiba iliyopitishwa itaanza saa mbili asubuhi na itamalizika saa kumi na mbili kamili jioni ya kila siku ya kampeni.

Mabadiliko ya ratiba

**29.** (1) Endapo Mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kitakusudia kufanya mabadiliko ya ratiba ya mikutano ya kampeni, mgombea au Chama hicho kitafanya hivyo baada ya kuwasilisha kwa

maandishi mapendekezo ya mabadiliko hayo kwa Msimamizi wa Uchaguzi na mapendekezo hayo kuridhiwa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (2).

(2) Msimamizi wa Uchaguzi ataitisha kikao na Vyama vya Siasa vinavyoshiriki uchaguzi ili kujadili maombi ya mabadiliko ya ratiba na mabadiliko yatakayokubaliwa yatawasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya kwa ajili ya kupatiwa ulinzi siku ya mkutano wa kampeni.

Masharti ya kampeni

30. (1) Mgombea, mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea kitatakiwa kuendesha mikutano ya kampeni za uchaguzi kwa mujibu wa ratiba na kwa kuzingatia muda uliowekwa chini ya Kanuni hizi.

(2) Mgombea au mwakilishi wa mgombea au Chama cha Siasa chenye mgombea hakitaruhusiwa kuendesha kampeni za uchaguzi kwa:

(a) kutumia rushwa;
(b) kutoa maneno ya kashfa au lugha za matusi;
(c) kufanya ubaguzi wa jinsia, maumbile, ulemavu, dini, rangi, kabila au ubaguzi mwingine wa aina yoyote; au
(d) kutoa maneno ambayo yanaweza kusababisha uvunjifu wa amani au vurugu.

## SEHEMU YA SABA
## TARATIBU ZA UPIGAJI KURA

Mahali, vituo na muda wa kupigia kura

31. (1) Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyeklti wa Kitongoji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji utafanyika katika Vitongoji vilivyomo katika Kijiji.

(2) Vituo vya kupigia kura vitakuwa katika majengo ya umma yaliyopo katika Kitongoji husika na endapo Kitongoji hakina majengo ya umma, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kushauriana na wagombea au vyama vya siasa vyenye wagombea, atateua eneo lingine kuwa kituo cha kupigia kura.

(3) Kura zitapigwa kuanzia saa mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi kamili jioni.

(4) Baada ya saa kumi kamili, askari atakaa nyuma ya mpiga kura wa mwisho ili kuzuia watu waliochelewa kupiga kura.

Masanduku ya kura

**32.** (1) Kutakuwa na sanduku maalum la kupigia kura lililotengenezwa kwa namna itakayomwezesha mpiga kura kutumbukiza kura yake kwa urahisi kwa kila ngazi itakayopigiwa kura bila ya kuruhusu kura hiyo kutolewa ndani ya sanduku hilo.

(2) Kabla ya kuanza kupiga kura, Msimamizi wa Kituo atawaonesha wapiga kura sanduku la kupigia kura lililo wazi na atalifunga kwa lakiri kwa namna ambayo itazuia kufunguliwa bila kukata lakiri.

Karatasi za kupigia kura

**33.** Kutakuwa na karatasi za kupigia kura kwa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia kundi la wanawake na uenyekiti wa Kitongoji ambazo zitakuwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Utambulisho wa mpiga kura

**34.** (1) Msimamizi wa Kituo atatakiwa, kabla ya kumpatia mpiga kura karatasi za kupigia kura, kujiridhisha kama jina la mpiga kura huyo limeorodheshwa katika Orodha ya Wapiga Kura.

(2) Kwa madhumuni ya Kanuni Ndogo ya (1), Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura aoneshe kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye Orodha ya Wapiga Kura.

(3) Aina ya kitambulisho ambacho Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura kuonesha ni pamoja na:

(a) kitambulisho cha mpiga kura;

(b) kitambulisho cha kazi;

(c) hati ya kusafiria;

(d) kadi ya bima ya afya;

(e) kitambulisho cha shule au chuo;

(f) kitambulisho cha mifuko ya hifadhi ya jamii;

(g) leseni ya udereva; au

(h) kitambulisho cha taifa.

(4) Endapo mpiga kura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote kati ya vilivyotajwa chini ya Kanuni Ndogo ya (3) lakini jina lake limo kwenye Orodha ya Wapiga Kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi wa Kituo atamruhusu mtu huyo kupiga kura baada ya kutambuliwa na wakazi wa eneo husika.

Upigaji kura

**35.** (1) Kura zitapigwa katika namna itakayozingatia usiri.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 34, Msimamizi wa Kituo atampatia mpiga kura karatasi nne za kupigia kura kwa nafasi zifuatazo:-
- (a) mwenyekiti wa Kijiji;
- (b) wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;
- (c) wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia kundi la wanawake; na
- (d) mwenyekiti wa Kitongoji.

(3) Mpiga kura, baada ya kupewa karatasi za kupigia kura, atapiga kura kwa utaratibu ufuatao:
- (a) kura moja kwa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji;
- (b) kura moja kwa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji;
- (c) kura kwa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa idadi itakayoelekezwa na Msimamizi wa kituo; na
- (d) kura kwa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia kundi la wanawake.

(4) Baada ya kupiga kura, mpiga kura atatakiwa kuchovya kidole cha mkono katika kidau cha wino.

(5) Wakati wa kupiga kura watu wafuatao wataruhusiwa kushuhudia kura zinavyopigwa:-
- (a) Msimamizi wa Uchaguzi;
- (b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
- (c) Askari au Afisa wa Polisi, Mgambo mwenye sare au afisa yeyote anayesimamia ulinzi ambaye atatambuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
- (d) Wakala wa Chama cha Siasa chenye Mgombea; na
- (e) Mwangalizi wa uchaguzi mwenye kitambulisho.

(6) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, mtu yeyote hatoruhusiwa kubaki katika eneo la Kituo cha Kupigia Kura baada ya kupiga kura.

Usaidizi kwa wenye mahitaji maalum

**36.** (1) Mpiga kura ambaye:

(a) kwa sababu ya ulemavu wa macho au ulemavu mwingine wowote; au

(b) hajui kusoma na kuandika,

anaweza kumwomba mtu yeyote kumsaidia kupiga kura; isipokuwa mpiga kura huyo hataruhusiwa kumchagua Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, mgombea au wakala wake.

(2) Bila kuathiri masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), mtu mmoja hataruhusiwa kumsaidia mpiga kura zaidi ya mmoja.

Kuahirisha upigaji kura

**37.** Endapo siku ya kupiga kura kutatokea jambo lolote litakalozuia upigaji kura kuendelea kufanyika, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi baada ya kuwasiliana na Msimamizi wa Uchaguzi ataahirisha upigaji kura hadi siku inayofuata au siku nyingine anayoona inafaa ambayo haitazidi siku saba tangu siku Uchaguzi ulipoahirishwa.

## SEHEMU YA NANE
## KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

Kuhesabu kura

**38.** (1) Kura zitahesabiwa na Msimamizi wa Kituo kwenye kituo cha kupigia kura mbele ya wagombea au mawakala wao.

(2) Msimamizi wa Kituo, kabla ya kuanza kuhesabu kura, atafanya yafuatayo mbele ya wagombea au mawakala wao:

(a) atahakiki idadi ya wakazi waliopiga kura;

(b) atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka katika bahasha maalum;

(c) atakagua lakiri na kuona kama haijafunguliwa;

(d) atakata lakiri; na

(e) atafungua sanduku la kupigia kura.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), wakati wa kuhesabu kura watu wafuatao wataruhusiwa kushuhudia kura zinavyohesabiwa:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;

(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(c) Askari au Afisa wa Polisi, Mgambo mwenye sare au afisa yeyote anayesimamia ulinzi; na

(d) Mwangalizi wa Uchaguzi mwenye kitambulisho.

(4) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hii, kura za wagombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji na ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji zitajumlishwa katika kituo cha kujumlishia kura kitakachokuwa katika ofisi ya Serikali ya Kijiji au mahali kwingine ambapo Msimamizi wa Uchaguzi ataelekeza.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (4), Mgombea au Wakala wake na watu waliotajwa katika kifungu kidogo cha (3) wanaweza kushuhudia kura zinavyojumlishwa.

Matokeo ya Mwenyekiti wa Kitongoji

**39.** (1) Msimamizi wa Kituo atamtangaza mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Kitongoji.

(2) Endapo idadi ya kura kwa nafasi ya uenyekiti wa Kitongoji italingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi wa Kituo atatangaza matokeo hayo na kuwasilisha taarifa ya uchaguzi huo kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atapanga tarehe nyingine ya Uchaguzi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya Uchaguzi.

(3) Matokeo ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kitongoji yatajazwa kwenye fomu ya matokeo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi ambayo itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi wa Kituo na kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

Matokeo ya Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji

**40.** (1) Msimamizi wa Kituo atajaza matokeo ya Uchaguzi wa Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kupitia kundi la wanawake kwenye fomu ya matokeo iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi ambayo itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi wa Kituo na nakala kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo ya uchaguzi na nakala halisi kuwasilishwa ofisi ya Serikali ya Kijiji.

(2) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kupokea nakala halisi ya fomu ya matokeo kutoka kwa Msimamizi wa Kituo, atajaza matokeo hayo katika fomu ya matokeo ya jumla iliyoainishwa

katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi na kumtangaza mshindi au washindi wa kila nafasi iliyogombewa.

(3) Fomu ya matokeo ya jumla itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(4) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji wa kundi la wagombea mchanganyiko yaani wanawake na wanaume utakuwa kama ifuatavyo:

(a) endapo idadi ya wagombea ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

(b) endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea ambao wamepata kura nyingi kuwa washindi wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji; au

(c) endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea lakini anahitajika mgombea mmoja kati yao ili kupata idadi ya jumla ya wajumbe wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo hayo na kupanga tarehe nyingine ya uchaguzi katika muda usiozidi siku kumi na nne tangu siku ya Uchaguzi.

(5) Utaratibu wa kutangaza matokeo ya Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa kundi la wagombea wa ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji kundi la wanawake utakuwa kama ifuatavyo:-

(a) endapo idadi ya wajumbe ni kubwa kuliko idadi ya nafasi za ujumbe zilizopo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea waliopata kura nyingi kuwa Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;

(b) endapo idadi ya kura italingana kwa wagombea au kwa baadhi yao, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atawatangaza wagombea ambao wamepata kura nyingi kuwa ni washindi wa nafasi ya ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji; au

(c) endapo idadi ya kura italingana kwa wagombea lakini anahitajika mgombea mmoja kati yao ili kupata idadi ya jumla ya wajumbe

wanaohitajika kwa mujibu wa Kanuni hizi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo hayo na kupanga tarehe nyingine ya uchaguzi katika muda usiozidi siku kumi na nne tangu siku ya Uchaguzi.

Matokeo ya Mwenyekiti wa Kijiji

**41.** (1) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, baada ya kupokea fomu za matokeo ya kura za nafasi ya uenyekiti wa Kijiji kutoka kwa wasimamizi wa vituo vya kupigia kura, atajumlisha idadi ya kura kwa kila mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa Kijiji na kujaza matokeo katika fomu ya matokeo ya jumla iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Kanuni hizi na fomu hiyo itasainiwa na wagombea au mawakala wao pamoja na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(2) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyepata kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa Kijiji na kubandika matokeo hayo kwenye sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

(3) Endapo idadi ya kura inalingana kwa wagombea wanaoongoza, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza matokeo na kupanga tarehe nyingine ya uchaguzi wa marudio utakaofanyika ndani ya muda wa siku kumi na nne tangu tarehe ya Uchaguzi.

Taratibu za kurudia uchaguzi

**42.** (1) Bila kuathiri masharti ya Kanuni hizi, Uchaguzi wa marudio unaotokana na kulingana kwa idadi ya kura utahusisha wagombea ambao idadi ya kura zao zimelingana na itachukuliwa kuwa wagombea hao wameshateuliwa kuwa wagombea kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Wagombea wanaoshiriki katika Uchaguzi wa marudio au Vyama vyao vya Siasa kwa mujibu wa Kanuni Ndogo ya (1) havitaruhusiwa kufanya kampeni za Uchaguzi wa marudio.

Masuala yasiyobatilisha matokeo

**43.** Masuala yafuatayo hayatobatilisha matokeo ya Uchaguzi au utekelezaji wa shughuli yoyote ya Uchaguzi:

(a) kutokuwepo kwa mgombea au wakala wa mgombea wakati wa kupiga kura, kuhesabu kura au kutangaza matokeo; au

(b) mgombea au wakala wa mgombea kukataa kusaini fomu ya matokeo.

Malalamiko kuhusu uendeshaji wa uchaguzi

**44.** Mgombea yeyote ambaye hakuridhika na matokeo ya Uchaguzi au uendeshaji wa Uchaguzi anaweza kufungua shauri katika Mahakama ya Wilaya ndani ya siku thelathini tangu siku ya kutangaza matokeo ya Uchaguzi.

SEHEMU YA TISA
NAFASI WAZI NA UCHAGUZI MDOGO

Nafasi wazi

45. (1) Nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itakuwa wazi endapo yatatokea mambo yafuatayo:
(a) kifo cha Mwenyekiti au Mjumbe;
(b) Mwenyekiti au Mjumbe kujiuzulu wadhifa wake;
(c) Mwenyekiti au Mjumbe kukosa sifa za kuwa mgombea;
(d) kubatilishwa kwa matokeo ya Uchaguzi;
(e) Mwenyekiti au Mjumbe kukoma kuwa mwanachama wa Chama cha Siasa kilichomdhamini;
(f) Mwenyekiti au Mjumbe kuhama Kijiji au Kitongoji kwa kadri itakavyokuwa;
(g) Mwenyekiti kutoitisha mikutano mitatu ya kawaida mfululizo bila kuwa na sababu za msingi;
(h) Mwenyekiti au Mjumbe kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya kawaida bila kuwa na sababu ya msingi;
(i) kugawanywa kwa Kijiji au Kitongoji; au
(j) Mwenyekiti au Mjumbe kuvuliwa madaraka kwa mujibu wa Sheria.

(2) Endapo litatokea jambo lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1), Mtendaji wa Kijiji atatoa taarifa kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika kipindi kisichozidi siku saba tangu kutokea kwa jambo hilo.

Uchaguzi Mdogo

46. (1) Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza kuwepo kwa nafasi wazi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji juu ya kuwepo kwa nafasi wazi.

(2) Nafasi wazi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itajazwa kwa kufanya Uchaguzi Mdogo kwa utaratibu uliopo katika Kanuni hizi.

(3) Nafasi ya uenyekiti wa Kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji itajazwa katika muda wa siku sitini baada ya kutangazwa kuwa wazi.

(4) Uchaguzi Mdogo hautafanyika kwa nafasi yoyote ile chini ya Kanuni hizi endapo muda uliosalia kabla ya Uchaguzi wa kawaida ni miezi sita au pungufu yake.

## SEHEMU YA KUMI
## UTARATIBU WA KUAPISHWA

Kiapo

47. (1) Wafuatao watatakiwa kuapa kiapo cha uaminifu na kutunza siri mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao chini ya Kanuni hizi:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi;
(b) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;
(c) Msimamizi wa Kituo;
(d) Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Rufaa;
(e) mawakala wa Vyama vya Siasa; na
(f) mtumishi yeyote wa umma atakayeteuliwa kusimamia shughuli za uchaguzi chini ya Kanuni hizi.

(2) Endapo Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya hawezi kupatikana, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anaweza kuwaapisha watu waliotajwa katika aya za (c), (d), (e) na (f) za Kanuni Ndogo ya (1).

(3) Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao, wataapa kiapo cha utii na uadilifu mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo au ya Wilaya katika tarehe na sehemu itakayopangwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

(4) Viapo vilivyotajwa katika Kanuni hii vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Tano la Kanuni hizi na watakaoapishwa watapewa nakala za viapo.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa ya uchaguzi

48. (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa la Uchaguzi endapo:

(a) ataharibu Orodha ya Wapiga Kura au nyaraka zozote zinazohusiana na Uchaguzi;
(b) atatoa taarifa za uongo ili aweze kupiga kura au kugombea nafasi ya uenyekiti wa Kijiji au ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji au uenyekiti wa Kitongoji;

(c) atajiandikisha au kupiga kura zaidi ya mara moja kwa wagombea wa nafasi moja;

(d) atatishia wapiga kura au wagombea ili kuvuruga Uchaguzi;

(e) atafanya kampeni siku ya Uchaguzi;

(f) ataonyesha ishara au kuvaa mavazi yanayoashiria kumtambulisha mgombea au Chama cha Siasa katika eneo la mita mia mbili kutoka kwenye kituo cha kupigia kura;

(g) atamzuia Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Mjumbe wa Kamati ya Rufani au mtumishi wa umma aliyeteuliwa kusimamia uchaguzi kutekeleza majukumu yake;

(h) atakiuka masharti ya kiapo chake chini ya Kanuni ya 47(1);

(i) atapatikana na karatasi za kupigia kura zaidi ya moja kwa nafasi moja inayogombewa;

(j) atavuruga ratiba ya mikutano ya kampeni ya Uchaguzi au atavunja masharti ya kampeni za Uchaguzi;

(k) atakutwa na silaha kinyume cha sheria kwenye eneo la uteuzi wa wagombea, mikutano ya kampeni, eneo la usikilizaji wa rufaa, kituo cha kuandikisha wapiga kura au kituo cha kupigia na kuhesabu kura;

(l) atafanya jambo lolote kinyume cha Kanuni hizi; au

(m) atatangaza matokeo ya Uchaguzi kabla hayajatangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(2) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kosa lolote chini ya Kanuni Ndogo ya (1) atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kinga

49. Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Wajumbe wa Kamati ya Rufaa au mtumishi yeyote wa umma aliyehusika na usimamizi wa Uchaguzi hatowajibika kwa jinai au madai au kuchukuliwa hatua za kinidhamu au kiutawala kwa jambo lolote alilolifanya au kuacha kufanya kwa nia njema wakati anatekeleza majukumu yake chini ya Kanuni hizi.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI
MASUALA MENGINE

Waangalizi wa ndani wa uchaguzi

**50.** (1) Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi wataruhusiwa kuangalia Uchaguzi baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

(2) Maombi ya kibali cha uangalizi wa Uchaguzi yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya Serikali za Mitaa ndani ya muda wa siku ishirini na moja baada ya Tangazo la Uchaguzi kutolewa.

(3) Waangalizi wa ndani wa Uchaguzi watafanya shughuli za uangalizi kwa gharama zao wenyewe na watatakiwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi na miongozo itakayotolewa ikiwa ni pamoja na kutoingilia kwa namna yoyote shughuli za Uchaguzi.

Taratibu za Maadili

**51.** Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi, kutakuwa na Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zilizoainishwa katika Jedwali la Sita la Kanuni hizi ambazo zitatakiwa kufuatwa na wadau wa Uchaguzi walioainishwa katika Taratibu hizo.

Miongozo

**52.** Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi, Waziri anaweza kutoa miongozo mbalimbali kuhusu Uchaguzi.

Elimu ya Mpiga Kura

**53.** (1) Taasisi yoyote inayotaka kutoa elimu ya mpiga kura katika Uchaguzi itatakiwa kuwasilisha maombi ya kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kwa Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya serikali za mitaa kwa kuzingatia miongozo itakayotolewa.

(2) Taasisi zitakazotoa elimu ya mpiga kura zitatoa elimu hiyo kwa gharama zao.

Kufutwa kwa Kanuni za Uchaguzi Tangazo la Serikali Na. 321 la Mwaka 2014

**54.** (1) Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Miji za Mwaka 2014 zinafutwa.

(2) Bila kujali masharti ya Kanuni Ndogo ya (1), matangazo, machapisho, miongozo, taratibu au kitu chochote kinachohusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambacho kilikuwa kinatumika kabla ya kuanza kutumika kwa Kanuni hizi, kitaendelea kutumika hadi pale kitakapofutwa na matangazo, machapisho, miongozo, taratibu au kitu chochote

kitakachotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi isipokuwa tu kama machapisho, miongozo, taratibu au kitu hicho kinakinzana na Kanuni hizi.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 11(1))*

**FOMU Na. 1**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**ORODHA YA WAPIGA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2019**

**HALMASHAURI ……………………………**
**KATA……………………………………….**
**KIJIJI……………………………………...**
**KITONGOJI……………………………….**

| Na. | Jina la Mpiga Kura *(Majina matatu)* | Jinsi (Me/Ke) | Umri | Tarehe ya kuandikishwa | Saini/Dole gumba la aliyeandikishwa | Saini ya Mwandikishaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | | |
| 2. | | | | | | |
| 3. | | | | | | |
| 4. | | | | | | |
| 5. | | | | | | |
| 6.. | | | | | | |
| 7. | | | | | | |
| 8. | | | | | | |
| 9. | | | | | | |
| 10. | | | | | | |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 17 (5)*

**FOMU Na. II**

**FOMU YA MAOMBI YA UTEUZI KUGOMBEA UENYEKITI WA KITONGOJI/KIJIJI MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

**HALMASHAURI .............................................**
**KATA.......................................................**
**KIJIJI.......................................................**
**KITONGOJI ..............................................**

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**
*(Ijazwe na anayeomba kugombea)*

1. Jina la Ukoo...................................................
2. Jina la Kati....................................................
3. Jina la Mwanzo..............................................
4. Jinsi (Me/Ke)..................................................
5. Uraia ..............................................................
6. Tarehe ya kuzaliwa..........................................
7. Mahali unapoishi (a) Kitongoji...........................
   (b)Kijiji.................................
   (c) Kata.................................
8. Namba ya Simu (kama ipo) ................................
9. Kazi/shughuli yako ..........................................
10.Uwezo wa Kusoma na Kuandika

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (a) | Kusoma Kiswahili | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |
| (b) | Kuandika Kiswahili | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |
| (c) | Kusoma Kiingereza | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |
| (d) | Kuandika Kiingereza | Ndiyo ☐ | Hapana ☐ |

11. Jina la Chama cha Siasa kinachomdhamini.......................................

12. Namba ya Kadi ya Uanachama..................................................
 tarehe ilipotolewa.........................mahali ilipotolewa.......................

13. Nafasi anayoomba kugombea....................................................

Nathibitisha kwamba taarifa zote zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo.

Saini ya Mgombea ............................Tarehe ....................................

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**

(*Ijazwe na Chama cha Siasa*)

Hii ni kuthibitisha kuwa ....................................(*Taja jina la Mgombea)* ni Mwanachama na amedhaminiwa na .................................................(*Taja jina la Chama*)

1. Jina: ...............................................
2. Saini:...... ........................................
3. Wadhifa: .........................................
4. Tarehe: ............................................
5. Anwani:..........................................
6. Muhuri wa Chama cha Siasa:................

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu.......................................................
2. Muda (saa)..........................................................................
3. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi................................
4. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi..................................
5. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ..........................

**SEHEMU D: UTEUZI**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa…………………………………..kugombea nafasi ya ……………………………………………

2. Sababu……………………………………………………………………

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………..

4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi …………………………

5. Tarehe……………………………………………………………………

6. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ……………………..

**FOMU Na. III**

**FOMU YA UCHAGUZI**

**FOMU YA MAOMBI YA UTEUZI KUGOMBEA UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI MCHANGANYIKO NA KUNDI LA WANAWAKE MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

**HALMASHAURI** ............................................
**KATA**......................................................
**KIJIJI**.....................................................
**KITONGOJI** ...............................................

**SEHEMU A: MAELEZO YA MGOMBEA**
(*Ijazwe na anayeomba kugombea*)

1. Jina la Ukoo.................................................
2. Jina la Kati..................................................
3. Jina la Mwanzo.............................................
4. Jinsi (Me/Ke).................................................
5. Uraia ..............................................................
6. Tarehe ya kuzaliwa...........................................
7. Mahali unapoishi (a) Kitongoji...........................
(b)Kijiji................................
(c) Kata................................
8. Namba ya Simu (kama ipo) ...............................
9. Kazi/shughuli yako ...........................................
10.Uwezo wa Kusoma na Kuandika

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (e) | Kusoma Kiswahili | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |
| (f) | Kuandika Kiswahili | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |
| (g) | Kusoma Kiingereza | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |
| (h) | Kuandika Kiingereza | Ndiyo | ☐ | Hapana | ☐ |

11. Jina la Chama cha Siasa kinachomdhamini……………………………………

12. Namba ya Kadi ya Uanachama……………………………………………….
    tarehe ilipotolewa…………………….mahali ilipotolewa…… …. ……….

13. Nafasi anayoomba kugombea………………………………………………...

Nathibitisha kwamba taarifa zote zilizoandikwa hapo juu ni sahihi kama nijuavyo.

Saini ya Mgombea ………………………Tarehe ………………………………

**SEHEMU B: UDHAMINI WA CHAMA CHA SIASA**
(*Ijazwe na Chama cha Siasa*)

Hii ni kuthibitisha kuwa ………………………………..(*Taja jina la Mgombea*) ni Mwanachama na amedhaminiwa na …………………………………………..(*Taja jina la Chama*)

1. Jina: ………………………………………..
2. Saini:…… ………………………………..
3. Wadhifa: ………………………………….
4. Tarehe: ……………………………………
5. Anwani:…………………………………..
6. Muhuri wa Chama cha Siasa:……………

**SEHEMU C: KURUDISHA FOMU**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi*)

1. Tarehe ya kupokea fomu……………………………………………………
2. Muda (saa)………………………………………………………………...
3. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………………………………
4. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi……………………………..
5. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ……………………….

**SEHEMU D: UTEUZI**

(*Ijazwe na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku ya uteuzi*)

1. Mgombea ameteuliwa/hakuteuliwa……………………………………kugombea nafasi

   ya ……………………………….

2. Sababu……………………………………………………………………….

3. Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………...

4. Saini ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ………………………...

5. Tarehe………………………………………………………………...

6. Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi …………………….

**FOMU Na. IV**

**TAMKO LA MGOMBEA LA KUHESHIMU NA KUTEKELEZA TARATIBU ZA MAADILI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2019**

***(Fomu hii ijazwe na kurudishwa pamoja na Fomu ya Uteuzi )***

Mimi..........................................................ambaye ninatarajia kuwa mgombea wa nafasi ya ………………...................................................niliyependekezwa na Chama cha.,,............................................................................. kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 ninatamka kuwa nitaheshimu na kutekeleza Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 wakati wote wa uchaguzi.

Ninatoa Tamko hili nikiamini kuwa yote niliyoeleza hapo juu ni kweli kwa kadri ya ufahamu wangu.

Saini ya Mgombea.......................................
Anwani.....................................................
Namba ya Simu……………………………………

Tamko hili limetolewa mbele yangu saa.......................... tarehe............. mwezi............
Mwaka 20....................

Saini...................................................
Jina.......................................................
Wadhifa **MSIMAMIZI WA UCHAGUZI/MSIMAMIZI MSAIDIZI WA UCHAGUZI***
*futa isiyohitajika.

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 33)*

**FOMU Na. V**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA NAFASI YA MWENYEKITI WA KIJIJI MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

**FOMU Na. VI**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA KWA NAFASI YA MWENYEKITI WA KITONGOJI 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

**FOMU Na. VII**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA NAFASI YA UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI MCHANGANYIKO MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

**FOMU Na. VIII**

**KARATASI YA KUPIGIA KURA NAFASI YA UJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI LA WANAWAKE MWAKA 2019**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | JINA LA CHAMA CHA MGOMBEA | NEMBO YA CHAMA CHA SIASA | WEKA ALAMA YA VEMA KWA MGOMBEA UNAYEMTAKA (√) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |
| 7. | | | | |
| 8. | | | | |
| 9 | | | | |
| 10. | | | | |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenzwa chini ya Kanuni ya 39, 40 na 41)*

**FOMU Na. IX**

**FOMU YA MATOKEO YA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI/KITONGOJI**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | CHAMA CHA SIASA | KURA ALIZOPATA | JINSI(KE/ME) | SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| 5. | | | | | |
| 6. | | | | | |
| 7. | | | | | |
| 8. | | | | | |
| 9. | | | | | |
| 10. | | | | | |

| | |
|---|---|
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | |
| Idadi ya waliopiga kura | |
| Idadi ya kura halali | |

| | |
|---|---|
| Idadi ya kura zilizoharibika | |
| Jina la Msimamizi wa Kituo | |

Saini………………………………………………………………tarehe………………

Muhuri wa Msimamizi wa Kituo…………………………………………………………

**FOMU Na. X**

**FOMU YA MATOKEO YA UCHAGUZI WA WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI MCHANGANYIKO/KUNDI LA WANAWAKE**

| NEMBO YA HALMASHAURI |
|---|

| Na. | JINA LA MGOMBEA | CHAMA CHA SIASA | KURA ALIZOPATA | JINSI (KE/ME) | SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | | | | | |
| Idadi ya waliopiga kura | | | | | |
| Idadi ya kura halali | | | | | |
| Idadi ya kura zilizoharibika/kukataliwa | | | | | |
| JUMLA | | | | | |
| Jina la Msimamizi wa Kituo | | | | | |

Saini……………………………………tarehe…………………

Muhuri wa Msimamizi wa Kituo………………………………

**FOMU Na. XI**

**EOMU YA MATOKEO YA JUMLA YA UCHAGUZI WA MWENYEKITI WA KIJIJI/KITONGOJI**

| NEMBO YA HALMASHAURI |
|---|

| Na. | JINA LA MGOMBEA | CHAMA CHA SIASA | KURA ALIZOPATA | JINSI(KE/ME) | SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| 5. | | | | | |
| 6. | | | | | |
| 7. | | | | | |
| 8. | | | | | |
| 9. | | | | | |
| 1.0 | | | | | |

| | |
|---|---|
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | |
| Idadi ya waliopiga kura | |
| Idadi ya kura halali | |
| Idadi ya kura zilizoharibika | |
| Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi | |

Saini……………………………………………………………………tarehe………………
Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi…………………………………………

**FOMU Na. XII**

**FOMU YA MATOKEO YA JUMLA YA UCHAGUZI WA WAJUMBE WA HALMASHAURI YA KIJIJI KUNDI MCHANGANYIKO/ KUNDI LA WANAWAKE**

**NEMBO YA HALMASHAURI**

| Na. | JINA LA MGOMBEA | CHAMA CHA SIASA | KURA ALIZOPATA | JINSI (KE/ME) | SAINI YA MGOMBEA AU MWAKILISHI WAKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| 5. | | | | | |

| | |
|---|---|
| Idadi ya waliojiandikisha kupiga kura | |
| Idadi ya waliopiga kura | |
| Idadi ya kura halali | |
| Idadi ya kura zilizoharibika/kukataliwa | |
| JUMLA | |
| Jina la Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi | |

Saini……………………………………tarehe…………………

Muhuri wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi………………..

JEDWALI LA TANO

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 47(4))*

VIAPO

*(a) Kiapo cha Uaminifu*

"Mimi ……………………………. naapa/natamka kwa dhati kwamba nitaitumikia vyema na kwa moyo thabiti Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi yangu kama ………………………………..katika Halmashauri ya …………………… na katika kutimiza wajibu wa nafasi hiyo nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kwa vyovyote vile sitatoa siri zinazohusu majukumu yangu isipokuwa kwa mujibu wa sheria. Ewe Mwenyezi Mungu, nisaidie."

Kiapo/Tamko hili limetolewa hapa: ……………………………………………………

na………………………………………………………………………………………………

Leo tarehe…………………… Mwezi wa…………………..Mwaka 20……………

Mbele ya:

**Jina:**…………………………………………………

**Saini:**…………………………………………………

**Wadhifa:**……………………………………………

**Anuani**………………………………………………

*(b) Kiapo cha Utii na Uadilifu*

Mimi …………………………………………………………… naapa/natamka kwa dhati kwamba nitaitumikia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wadhifa wangu wa …………………………………………… kwa uaminifu, kwa uwezo na moyo wangu wote na kwamba nitahifadhi, nitalinda na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria za Tanzania na Maadili ya Viongozi wa Umma kama yalivyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Ewe Mwenyezi Mungu nisaidie"

Kiapo/Tamko hili limetolewa hapa: ...............................................

na.........................................................................................

**Leo tarehe............ Mwezi wa................Mwaka 20.........................**

Mbele ya:................................................

**Jina:.....................................................**

**Cheo:..................................................**

**Saini:..................................................**

**Anuani...............................................**

JEDWALI LA SITA

*(Limetengenezwa chini ya Kanuni ya 51)*

**TARATIBU ZA MAADILI**

**1.0 Jina, Matumizi, Wahusika wa Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019**

**1.1 Jina na Tarehe ya kuanza kutumika**

Taratibu hizi zitajulikana kama Taratibu za Maadili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019.

**1.2 Wahusika wa Taratibu za Maadili**

Wahusika wa taratibu za Maadili hizi watakuwa wafuatao:-

(a) Vyama vya Siasa;

(b) Wagombea;

(c) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(d) Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi.

**2.0 Taratibu za Maadili**

**2.1 Wajibu wa Vyama vya Siasa na Wagombea**

**Kila Chama cha Siasa na Wagombea watatakiwa kuzingatia yafuatayo:-**

(a) kuheshimu na kutekeleza Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi itakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni pamoja na kuzingatia matakwa ya Sheria nyingine za nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi;

(b) kuelimisha, kuhamasisha na kuwasisitiza wanachama na wafuasi wao kuheshimu Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi itakayotolewa kwa mujibu wa Kanuni pamoja na Sheria nyingine za nchi katika kipindi chote cha Uchaguzi;

(c) kuzingatia ratiba ya mikutano ya kampeni;

(d) kwa kushirikiana na wanachama na wafuasi wa Vyama vingine vya Siasa

(e) kuhakikisha kuwa wanachukua hatua za makusudi ili:-

(i) kufanya Uchaguzi uwe huru na wa haki;

(ii) kuzuia vitendo vya vurugu na vitisho;

(iii) kukataa aina yoyote ya ubaguzi katika misingi ya jinsia, maumbile, ulemavu, ukabila, dini au rangi; na

(iv)kueneza taarifa sahihi kuhusu mchakato wa Uchaguzi;

(f) kuchapisha vijitabu, vipeperushi, vilini, mabango na machapisho ya aina yoyote yanayoelezea sera zao baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa Uchaguzi;

(g) kutumia vyombo vya habari kutangaza sera zao kwa kuzingatia sheria zinazosimamia vyombo vya habari na Miongozo ya Uchaguzi;

(h) kujenga mazingira ambayo yatawezesha Uchaguzi kufanyika kwa uhuru na haki, ikiwa ni pamoja na kuwezesha makundi maalum kushiriki kikamilifu katika Uchaguzi;

(i) kuhakikisha hifadhi na usafi wa mazingira katika kusambaza matangazo ya kampeni;

(j) kuondoa mabango, matangazo na machapisho ya aina yoyote ile yaliyotumika wakati wa kampeni katika sehemu za wazi baada ya Uchaguzi;

(k) kutoa taarifa mara moja kwa mamlaka husika wanapofahamu au wanapoona tukio linaloweza kusababisha vurugu au uvunjifu wa amani;

(l) kuhakikisha kuwa wanafanya kampeni kwa kuzingatia misingi inayolenga kutangaza sera za Vyama vyao pasipo kujenga chuki, kusababisha mifarakano na migawanyiko katika jamii;

(m)kuchukua hatua za lazima kuhakikisha kuwa hakuna migongano ya mikutano ya kampeni na Vyama vingine;

(n) kukataza wanachama au wafuasi kutamka kauli mbiu, kuonesha ishara za Vyama vyao, au kuvaa sare zenye rangi ya Chama chao katika mikutano ya hadhara ya Vyama vingine; na

(o) kuwaelekeza Mawakala wao watakaokuwepo katika Vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi, Taratibu za Maadili ya Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi.

**2.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Vyama vya Siasa na Wagombea**

Kila Chama cha Siasa au Mgombea hatatakiwa kufanya yafuatayo:-

(a) kusababisha au kufanya fujo au vurugu ya aina yoyote katika Mkutano wake au wa Chama kingine;

(b) kutumia lugha ya matusi, kashfa, kejeli, udhalilishaji na vitisho au lugha inayochochea uvunjifu wa amani au kuashiria ubaguzi wa kijinsia, dini, rangi, ulemavu au maumbile kwenye mikutano ya kampeni;
(c) kubeba sanamu, kinyago au kitu chochote ambacho kinaonyesha kudhalilisha, kukebehi, kufedhehesha au kukejeli Chama kingine cha Siasa au Mgombea au Kiongozi wa Chama kingine cha Siasa au Serikali katika mkutano wowote wa kampeni za Uchaguzi;
(d) kutumia vipaza sauti vya aina yoyote kwa shughuli za kisiasa mara baada ya muda wa kampeni za Uchaguzi kumalizika;
(e) kuchafua, kubandua au kuharibu kwa namna yoyote ile matangazo ya kampeni ya Vyama vingine vya Siasa na matangazo mengine yanayotolewa na Mamlaka za Uchaguzi;
(f) kubandika mabango ya kampeni, matangazo au mchoro wowote kwenye nyumba, majengo au vyombo vya usafiri vya watu binafsi au taasisi mbalimbali bila idhini ya wamiliki husika;
(g) kubandika mabango ya kampeni, matangazo au mchoro wowote kwenye nyumba za ibada, taasisi za dini na majengo ya Serikali na taasisi zake;
(h) kutoa rushwa ili kumshawishi mtu yeyote kupiga kura, kugombea au kujitoa katika kugombea nafasi ya uongozi;
(i) kuzuia mtu yeyote, watu au wafuasi wa vyama vingine kuhudhuria mikutano ya kampeni au kupiga kura;
(j) kukodi au kutumia usafiri wa aina yoyote kubeba na kusafirisha wapiga kura kwa madhumuni ya kushawishi kupigiwa kura.

**2.3 Maadili wakati wa kupiga, kuhesabu, kujumlisha kura na kutangaza matokeo ya Uchaguzi**

**2.3.1. Yanayotakiwa Kufanywa**

(a) Vyama vya Siasa na Wagombea watahakikisha kuwa Mawakala wao wanakula kiapo na kukiwasilisha kwa Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kabla ya siku ya Uchaguzi;
(b) Mawakala wa Vyama vya Siasa, Vyama vya Siasa na Wagombea watakuwa na wajibu wa kushirikiana na Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo katika vituo vya kupigia kura kwa kuzingatia Kanuni za Uchaguzi na Miongozo ya Uchaguzi;
(c) Viongozi wa Vyama vya Siasa watakuwa na wajibu wa kuwaelimisha wanachama na wafuasi wao kuwa, watatakiwa kuondoka eneo la kupigia Kura mara tu wamalizapo kupiga kura na kama itawalazimu kubakia katika eneo hilo watatakiwa kukaa umbali wa mita mia mbili kutoka kituo cha kupigia kura.

**2.3.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa**

(a) Kampeni za uchaguzi hazitaruhusiwa siku ya upigaji kura. Hii ni pamoja na kuvaa vazi lolote au kuwa na kitu chochote kinachoashiria kushawishi watu kumpigia kura Mgombea fulani au utambuzi wa Mgombea fulani au matumizi ya chombo cha usafiri kinachoashiria utambuzi wa Chama au Mgombea wa Chama chochote;

(b) Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wagombea na wafuasi wao watatakiwa kujiepusha na vitendo vinavyoweza kusababisha fujo au vurugu katika vituo vya kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura;

(c) Hakuna mtu atakayeruhusiwa kutumia simu ya kiganjani ndani ya kituo cha kuhesabu na kujumlishia kura isipokuwa Msimamizi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na mlinzi wa kituo cha kupigia kura ambao watatumia simu zao pale itakapobidi kwa shughuli za Uchaguzi tu na simu hizo wakati wote ziwe zimeondolewa mlio na ziwe kwenye mtetemo;

(d) Kiongozi au Mtendaji au mwanachama au mfuasi wa Chama cha Siasa hatatakiwa;

(i) kuvamia au kukaa kwa nguvu ndani ya kituo cha kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura;

(ii) kuwahamasisha wanachama au wafuasi kupiga kura zaidi ya mara moja katika Uchaguzi mmoja;

(iii)kununua kura au kutoa rushwa au aina yoyote ya malipo ya fedha au vifaa kwa mpiga kura au Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(iv)kutumia lugha ya matusi kwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Kituo katika kituo cha kupigia, kuhesabia na kujumlishia kura.

**3.0 Wajibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Serikali itakuwa na Wajibu wa:**

(a) kutoa fursa sawa kwa wadau wote wa Uchaguzi hususan Vyama vya Siasa na Wagombea ili kuendesha shughuli zao za kisiasa wakati wa Uchaguzi kwa uhuru na kuzingatia sheria za nchi;

(b) kuhakikisha hali ya usalama, amani na utulivu wakati wote wa Uchaguzi;

(c) kuhakikisha kuwa viongozi na watendaji wake wanazingatia ipasavyo ukomo wa madaraka yao katika shughuli za Uchaguzi.

**4.0 Taratibu za Maadili kwa Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi**

**4.1 Mambo wanayotakiwa Kufanya**

Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi watakuwa na wajibu wa kupanga, kusimamia na kuendesha Uchaguzi katika misingi inayowezesha Uchaguzi kuwa huru na wa haki kwa kufanya yafuatayo:-

(a) kuzingatia Katiba ya Nchi, Kanuni za Uchaguzi na Sheria nyingine za nchi;
(b) kuvipatia Vyama vya Siasa ratiba na taarifa za Uchaguzi mapema;
(c) kutoa Elimu ya Mpiga Kura, kusimamia na kuratibu taasisi na watu wanaotoa Elimu ya Mpiga Kura;
(d) kutoa mafunzo kwa wanaohusika na Uchaguzi ili kuwawezesha kuendesha uchaguzi kwa ufanisi;
(e) kuvipatia Vyama vya Siasa Kanuni, Miongozo ya Uchaguzi na Nyaraka nyingine zinazohusiana na Uchaguzi;
(f) kukemea vitendo vyenye nia ya kuharibu Uchaguzi vinavyoweza kufanywa na Viongozi wa Vyama vya Siasa, Wagombea au wafuasi wao;
(g) kuendesha na kuziwezesha Kamati za kusimamia Maadili ya Uchaguzi na kusimamia utekelezaji wa maamuzi yanayotolewa na Kamati hizo;
(h) kukutana na Vyama vya Siasa pale inapobidi kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Kampeni za Uchaguzi na Uchaguzi wenyewe;
(i) kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote atakayefanyiwa uonevu au kukoseshwa haki wakati wa shughuli za Uchaguzi;
(j) kutambua majukumu ya Vyama vya Siasa, Wagombea na Mawakala wao;
(k) kuandaa na kupeleka kwa wakati vifaa kwenye vituo vya kupigia kura;
(l) kuendesha zoezi la Uchaguzi kwa uwazi, haki na uadilifu.

**4.2 Mambo yasiyotakiwa kufanywa na Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi**

(a) kupendelea Chama chochote cha Siasa au Mgombea yeyote;
(b) kubadili ratiba za Kampeni za Uchaguzi bila kuvishirikisha Vyama vya Siasa;
(c) kuchelewa au kupeleka vifaa pungufu katika vituo vya kupigia kura bila sababu za msingi;
(d) kuchelewa kutangaza Matokeo ya Uchaguzi bila sababu za msingi.

**5.0 Usimamizi wa Utekelezaji waTaratibu za Maadili ya Uchaguzi**

**5.1 Kamati za Maadili za kusimamia Utekelezaji wa Taratibu za Maadili ya Uchaguzi**

**Kutakuwa na Kamati za Maadili zifuatazo zitakazoundwa na Msimamizi wa Uchaguzi:-**

(a) Kamati ya Maadili ya Halmashauri; na
(b) Kamati ya Maadili ya Kata.

**5.2 Muundo wa Kamati za Taratibu za Maadili ya Uchaguzi**

**5.2.1 Kamati ya Maadili ya Halmashauri**

Kamati ya Maadili ya Halmashauri itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Msimamizi wa Uchaguzi katika Halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;

(b) Mjumbe mmoja kutoka kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi katika Halmashauri;
(c) Mjumbe mmoja atakayewakilisha Serikali ambaye atateuliwa kwa maandishi na Katibu Tawala wa Wilaya husika; na
(d) Afisa Uchaguzi ambaye atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Maadili ya Uchaguzi.

**5.2.2 Kamati ya Maadili ya Kata**

**Kamati ya Maadili ya Kata itakuwa na wajumbe wafuatao:-**

(a) Msimamizi Msaidizi ngazi ya Kata husika ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;
(b) Mjumbe mmoja kutoka kila Chama cha Siasa kinachoshiriki katika Uchaguzi kwenye Kata;
(c) Mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali atakayeteuliwa kwa maandishi na Katibu Tawala wa Wilaya husika; na
(d) Katibu ambaye ni Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kijiji atakayeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

**5.2.3 Utoaji wa taarifa za Kamati za Maadili**

Itakuwa ni marufuku kwa mtu, mgombea, Chama cha Siasa au mjumbe wa Kamati ya Maadili ambaye sio Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili kutoa taarifa yoyote kuhusu maamuzi ya Kamati au suala lolote lililopo mbele ya Kamati.

**5.3 Uwasilishaji wa Malalamiko**

Mgombea yeyote, Wasimamizi au Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, Serikali au Chama chenye Mgombea kinachoamini kwamba Maadili ya Uchaguzi yamekiukwa kitawasilisha malalamiko kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya Kata kwa maandishi.

**5.4 Muda wa kuwasilisha Malalamiko**

Malalamiko yoyote yatatakiwa kuwasilishwa ndani ya siku tatu tangu kutokea kwa tukio linalolalamikiwa.

**5.5 Kuitisha kikao cha Kamati ya Maadili ya Uchaguzi**

Mwenyekiti wa Kamati husika baada ya kupokea malalamiko na kujiridhisha kuwa Taratibu za Maadili zimekiukwa atatakiwa kuitisha kikao ndani ya siku mbili.

**5.6 Namna ya kushughulikia Malalamiko**

(a) Malalamiko yote yatajadiliwa na kuamuliwa katika kikao cha Kamati ya Maadili ya Kata husika;
(b) Kamati itashughulikia malalamiko na kutoa uamuzi wake mapema iwezekanavyo;

(c) Baada ya kupokea malalamiko, Kamati itamtaka aliyelalamikiwa kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku mbili tangu kupokea malalamiko;

(d) Katika kushughulikia malalamiko, Kamati inaweza kumwita mtu yeyote kutoa maelezo ili kusaidia Kamati kufikia maamuzi ya haki;

(e) Akidi ya Kikao cha Kamati husika itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa Kamati;

(f) Kamati ya Maadili ya Uchaguzi itaamua malalamiko yote baada ya kusikiliza au kupata maelezo ya utetezi kutoka kwa pande zote mbili ambazo ni mlalamikaji na mlalamikiwa ndani ya siku mbili isipokuwa kama upande unaolalamikiwa utashindwa kuwasilisha maelezo ya utetezi katika muda ulioainishwa Kamati inaweza kufanya uamuzi;

(g) Maamuzi yatakayofikiwa na Kamati ya Maadili ya Kata yatatekelezwa na pande zinazohusika na maamuzi hayo;

(h) Ikitokea kuna umuhimu wa kufanya maamuzi kwa kupiga kura, wawakilishi wa Mlalamikaji na Mlalamikiwa hawataruhusiwa kupiga kura;

(i) Malalamiko yatakayoshughulikiwa na Kamati za Maadili ni yale tu yaliyotokea katika kipindi cha Kampeni;

(j) Malalamiko yatakayotokea siku ya Upigaji Kura yatashughulikiwa kwa kuzingatia Kanuni za Uchaguzi;

(k) Kamati itakuwa na mamlaka ya kuchunguza malalamiko yote yatakayowasilishwa kabla ya kufanya maamuzi;

(l) Kamati inaweza kuelekeza malalamiko mengine kwenye mamlaka zinazohusika kama itakavyoona inafaa kwa hatua zinazostahili.

**5.7 Rufaa Dhidi ya Maamuzi**

(a) Upande ambao hautaridhika na uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Kata, utakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Kamati ya Maadili ya Halmashauri ndani ya siku mbili tangu uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Kata ulipotolewa; na

(b) Uamuzi utakaotolewa na Kamati ya Maadili ya Halmashauri utakuwa ni wa mwisho.

**5.8 Malalamiko dhidi ya Msimamizi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi**

(a) Pale ambapo malalamiko yaliyowasilishwa ni dhidi ya Msimamizi wa Uchaguzi, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili`ya Uchaguzi, Msimamizi au Msimamizi Msaidizi, Msimamizi wa Uchaguzi hataendesha Kikao hicho, isipokuwa Katibu Tawala wa Mkoa atateua Afisa yeyote wa Umma Mwandamizi kutoka Sekretarieti ya Mkoa kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho;

(b) Iwapo Kamati itaona kuwa Msimamizi amekosea Kamati itamtaka Msimamizi wa Uchaguzi kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo.

**5.9 Malalamiko dhidi ya Serikali**

Kamati ya Maadili ya Kata itapokea malalamiko yatakayotolewa dhidi ya Serikali na iwapo Kamati itaona kuwa Serikali imekosea itaitaka Serikali kurekebisha tatizo linalolalamikiwa mapema iwezekanavyo.

**5.10 Mamlaka ya Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Halmashauri na Kata katika kushughulikia Malalamiko na kutoa adhabu**

Kamati za Maadili ya Uchaguzi ngazi ya Halmashauri na Kata zinaweza kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) kuagiza upande uliokiuka maadili kusahihisha kosa au makosa yaliyotendeka na iwapo italazimu, kuomba msamaha hadharani;

(b) kutoa onyo au karipio kwa maandishi;

(c) kutangaza jina la Chama au Mgombea aliyekiuka Maadili na kueleza kosa au makosa yake kwa njia za Taarifa kwa Umma, redio, televisheni, magazeti na njia nyingine za mawasiliano;

(d) Kamati inaweza kukisimamisha Chama au Mgombea kuendelea kufanya Kampeni za Uchaguzi kwa muda itakavyoona inafaa.

**5.11 Kushindwa Kutekeleza Maamuzi ya Kamati za Maadili**

Pale ambapo Mgombea au Chama kitashindwa kutekeleza maamuzi ya Kamati husika, Kamati ya Maadili ya Uchaguzi inaweza kukisimamisha Chama husika kufanya kampeni za Uchaguzi.

DODOMA
25/04/2019

SELEMANI S. JAFO (Mb)
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*